

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Tano – Tarehe 6 Aprili, 2020

(Mkutano Ulianaza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Mheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

(i) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019;

(ii) Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2020;

(iii) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019;

(iv) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019;

(v) Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi yaliyotolewa Mwaka 2016;

(vi) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Shughuli za Manunuzi ya Umma;

(vii) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Utekelezaji wa Jitihada za Kitaifa za Kupambana na Utakasishaji wa Fedha nchini;

(viii) Majumuisho ya majibu ya Hoja na Mpango wa Kutekeleza Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):

(i) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019;

(ii) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Ubora wa Shughuli za Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Lami Mijini;

(iii) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Ukusanyaji Mapato toka vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iv) Taarifa ya Majibu ya Serikali na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioshia tarehe 30 Juni, 2019;

(v) Taarifa ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Hesabu za Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Makusanyo ya Mapato kutoka kwa Kampuni za Simu.

WAZIRI WA KILIMO:

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi wa Maghala na Vihenge vya Kutunzia Mazao.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Shughuli za Kinga na Chanjo.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo.

WAZIRI WA NISHATI:

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Upatikanaji wa Umeme na Uhakika wa Utoaji Huduma za Umeme.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

(i) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji usioridhisha wa Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi yenye ubora kwa Watanzania;

(ii) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Utoaji Programu za Kuwajengea Uwezo Walimu – Kazini.

SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 35

Uhaba wa Watumishi wa Sekta ya Afya

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Sekta ya Afya nchini inakabiliwa na uhaba wa Watumishi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuziba pengo hili?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri wataalam wa kada mbalimbali za Sekta ya Afya nchini ambapo kuanzia Mei, 2017 hadi Julai, 2019 jumla ya watumishi 8,994 wameajiriwa na kupangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepewa kibali cha kuajiri Madaktari 610 ambaao watapangwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto.

Na. 36

Kuboresha Zahanati ya Bassotu – Hanang

MHE. ROSE K. SUKUM aliuliza:-

Kutokana na wingi wa watu na shughuli za kiuchumi zilizopo katika Kata ya Bassotu kama vile uchimbaji madini, uvuvi, kilimo, ufugaji na biashara na hivyo kuwa na hatari ya milipuko ya magonjwa:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya Watoto, Wanawake, Wanaume na nyumba za watumishi wa Zahanati ya Bassotu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukumu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na Mwongozo unaosimamia utoaji wa huduma za afya, zahanati hazina Wodi ya Watoto, Wanawake na Wanaume. Hata hivyo, kutokana na umbali uliopo kati ya zahanati hiyo na Hospitali ambaao ni kilometra 55, Serikali itafanya tathmini ili kuboresha miundombinu iliyopo na kuifanya Zahanati ya Bassotu kuwa na hadhi ya Kituo cha Afya.

Na. 37

Kuboresha Huduma za Afya Tunduru

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI aliuliza:-

(a) Je serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma za Afya katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru na Katika Vituo vya Afya Nakapanya na Matemanga?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Vituo vya Afya na Zahanati katika Kata na Vijiji ili kuendana na Sera ya Afya na Ilani ya CCM?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer Ramo Mataala Makani*, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wa uboreshaji wa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru ambapo wodi mbili ziko katika hatua ya ukamilishaji kwa gharama ya Shilingi milioni 140. Aidha, Hospitali imewezeshwa kufungua duka la dawa na kupatiwa mashine ya *Ultrasound*. Serikali imetumia shilingi milioni 500 kukarabati Kituo cha Afya Matemanga na Shilingi milioni 200 kujenga wodi ya mama na mtoto na jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Nakapanya?

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa ujenzi wa Vituo vya Afya kwa awamu na tayari imekamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vitatu Wilayani Tunduru kwa gharama ya shilingi biloni 1.3 na inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Afya Nakapanya kwa gharama ya shilingi milioni 200. Majengo mengine yaliyobaki yataendelea kupewa kipaumbele ili kufikia azima ya kusogea huduma karibu na wananchi.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, je, ni lini Serikali itaifanyia ukarabati miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Tunduru yakiwemo majengo yake (wodi, vyumba vya upasuaji, majengo ya mapokezi na kadhalika kwani miundombinu hiyo ni chakavu kutokana na umri mrefu tangu uhuru?)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Sera ya Afya inafafanua kuhusu hitaji la uwepo wa Kituo cha Afya kwa kila Kata. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Nampungu ambayo ni mojawapo ya kata tatu za Tarafa ya Nampungu yenye kata tatu na hakuna Kituo cha Afya hata kimoja?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kama niliyoyibju kwenye swalii la msingi kuwa, Serikali inaendelea na mpango wa uboreshaji wa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru ambapo wodi mbili ziko katika hatua ya ukamilishaji kwa gharama ya Shilingi milioni 140 na Hospitali imewezeshwa kufungua duka la dawa na kupatiwa mashine ya *Ultrasound*. Serikali itaendelea kuikarabati, kuipanua na kuiboresha Hospitali ya Halmashauri ya Tunduru kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Aidha katika Hotuba itakayowasilishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutatoa ufanuzi kuhusu mpango wa ujenzi na ukarabati wa hospitali kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Mheshimiwa Mbunge anaombwa kuvuta subira mpaka wakati wa uwasilishaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ya msingi nchini kwa kukarabati miundombinu iliyopo, kukamilisha maboma na kujenga miundombinu mipyaa. Hadi Machi, 2020 vituo vya kutolea huduma za afya 400 ikiwemo Hospitali za Halmashauri mpya 98 zimepokea fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hili, Serikali imetoea kipaumbele kwa maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa wa huduma za afya kwa kuzingatia vigezo vya wingi wa watu, umbali na maeneo ambayo ni magumu kufikika. Serikali inaendelea kutekeleza Sera na Mpango huu kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Na. 38

Barabara ya Kutoka Mbulu - Haydom Kilometra 50

MHE. ZACHARIA P. ISSAY aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mbulu mpaka Haydom kilometra 50 kama ilivyopitishwa kwenye bajeti ya 2019/2020?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbulu – Haydom kilometra 50 ni sehemu ya barabara ya Karatu, Mbulu, Haydom, Sibiti, Lalago – Maswa kilomita 389 ijulikanayo kama *Serengeti Southern Bypass*. Barabara hii inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) kuititia Mikoa ya Arusha, Manyara, Singida na Simiyu. Kazi ya upembuzi yakinfu na usanifu wa awali wa mradi wa Serengeti *Southern Bypass* iko katika hatua za mwisho. Mara baada ya upembuzi yakinfu na usanifu wa awali kukamilika hatua itakayofuata ni usanifu wa kina wa maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu unahuishisha barabara ndefu yenye urefu wa kilometra 389, ili kurahisisha utekelezaji wake wakati wa ujenzi, mradi huu umegawanywa katika sehemu saba ambazo ni Karatu – Mbulu kilometra 79; Mbulu - Haydom kilometra 70.5; Haydom - Chemicchemi kilometra 67; Chemicchemi - Mwanhuzi kilometra 80; Mwanhuzi – Lalago - Maswa kilometra 83; Haydom - Kadash kilometra 67 na Lalago - Kolandoto kilometra 62.

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii utaanza baada ya kukamilisha usanifu wa kina.

Na. 39

Ahadi ya Visima 30 Vya Maji – Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza: -

Wilaya ya Urambo inakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji hadi Serikali ikaingiza Wilaya hii katika mpango mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria, wakati wananchi wa Urambo wakisubiri mpango huo wa maji kutoka Ziwa Victoria:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya kuchimba visima 30 katika Wilaya ya Urambo?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na uhaba wa maji, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilisaini Mkataba na uliokuwa Wakala wa Uchimbaji Visima (*DDCA*) tarehe 26 Machi, 2018 wa ghamama ya Shilingi milioni 620.9 kwa ajili ya kuchimba visima 30 katika Vijiji vya Ussoke Mjini viwii; Itundu viwili; Kasisi viwili; Kiloleni viwili; Tulieni kimoja; Machinjioni kimoja; Ulassa B kimoja; Ifuta viwili; Ugalla viwili; Uyogo viwili; Nsenda viwili; Unzali viwili; Vumilia viwili; Kalembela viwili; Ussoke Mlimani viwili; Katunguru viwili; na Kapilula kimoja.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa maeneo ya uchimbaji wa visima hivyo umekamilika na mradi huu utatekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*) ambapo unatarajwa kufanyika mwezi Mei, 2020.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wilaya ya Urambo kupitia Mpango wa Matokeo (*PforR*) imepanga kuchimba visima virefu 18 ili kupunguza tatizo la uhaba wa maji katika Vijiji vya Isongwa, Kichangani, Milambo, Ulassa A, Kamalendi, Mtakuja, Sipungu, Tumaini, Ukwanga, Itegamatwi, MotoMoto,

Kalembela, Usoke Mlimani, Usoke Mjini, Itebulanda, Tebelia, Kasisi na Vumilia. Utekelezaji wa kazi hiyo unatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2020.

Na. 40

Serikali Kutoa Ruzuku kwa Mazao Yanayonunuliwa na NFRA

MHE. ANATROPIA L. THEONEST aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali inawazuia wakulima wanaoshirikiana na sekta binafsi, kuuza mazao yao ya biashara hasa kahawa, mahindi na korosho nje ya nchi kwa lengo la kujipatia faida?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isiongeze ruzuku ya *NFRA* ili inunue mazao hayo pindi bei zinaposhuka?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Anatropia Lweikila Theonest – Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imekuwa na inaendelea kutoa vibali kwa wakulima na wafanyakishara mbalimbali wanaosafirisha mazao ya kilimo hususan mahindi nje ya nchi au kuingiza ndani ya nchi. Vibali vitolewavyo na Wizara ya Kilimo ni vya kuingiza mazao ya kilimo nchini au kusafirisha mazao ya kilimo nje ya nchi (*Import and Export Permits*) pamoja na cheti cha Usafi wa Mazao yanayosafirishwa (*Phytosanitary Certificate*).

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa aina yoyote wa kuwazuia wakulima kushirikiana na sekta binafsi kuuza mazao yao nje ya nchi na Serikali inaendelea kuhimiza wakulima waendelee kujunga katika vikundi ili waweze kuwa na nguvu ya pamoja katika kuuza mazao yao na kuweza kuongezea thamani mazao yao ili waweze kujiongezea kipato zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*NFRA*) ni kununua na kuweka akiba ya chakula cha Taifa, kudhibiti mfumuko wa bei wa vyakula vya nafaka kwa kuingiza nafaka sokoni ya bei nafuu pamoja na kutoa chakula cha msaada kwa maelekezo ya Mfuko wa Maafa wa Taifa pindi Taifa linapopatwa na majanga ya maafa. Kwa kuzingatia majukumu hayo, Wakala umekuwa kimbilio la wakulima kwa kuwa umekuwa ukinunua nafaka kwa bei nzuri katika masoko inayozingatia gharama za uzalishaji za mkulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali hutenga ruzuku kwa ajili ya ununuzi wa nafaka kila mwaka. Kwa kuzingatia majukumu ya Wakala, ununuzi huu hauhusishi mazao yasiyo ya nafaka. Aidha, Wakala hutumia vyanzo vingine vya mapato kununua nafaka zikiwemo mauzo ya nafaka na mikopo kutoka taasisi za fedha, mikopo ambayo hurejeshwa kwa kutumia fedha za mauzo ya nafaka.

Na. 41

Mabwana na Mabibi Misitu

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN aliuliza:-

Je, Tanzania ina Mabwana na Mabibi Misitu wangapi wenye elimu ya Cheti na Diploma?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taaluma ya Misitu kwa ngazi ya cheti na *diploma* hapa Tanzania hutolewa na Chuo cha Misitu Olmotonyi kilichopo Arusha. Baada ya uhuru mwaka 1961 hadi 2019, Serikali kuititia Chuo cha Misitu, Olmotonyi imetoa jumla ya wataalam 4,063 wa misitu. Kati ya hao, ngazi ya diploma ni 1,788 wanaume 1,239 na wanawake 549 na

katika ngazi ya cheti wataalam ni 2,275 wanaume 1,544 na wanawake 731.

Mheshimiwa Spika, aidha, Chuo cha Viwanda nya Misitu (*FITI*) kilichopo Mjini Moshi hutoa wataalam wa kusimamia viwanda nya mazao ya misitu katika ngazi ya cheti (astashahada) na diploma (stashahada). Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1975, Chuo kimetoa jumla ya wataalam 627, kati ya hao, wangazi ya astashahada ni 510 na stashahada ni 117.

Mheshimiwa Spika, baada ya wahitimu kumaliza masomo yao huajiriwa ama na sekta binafsi, Serikali Kuu, mathalani Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake zikiwemo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*TFS*), Serikali za Mitaa na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (*TAFORI*).

Mheshimiwa Spika, kwa sasa jumla ya Mabwana na Mabibi Misitu 1,227 wenyе diploma na cheti wameajiriwa ambapo 770 wapo katika taasisi za Wizara (Wakala wa Huduma za Misitu (*TFS*) 748, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (*TAFORI*) 16, Chuo cha Misitu Olmotonyi wanne na Chuo cha Viwanda nya Misitu wawili) na 457 wameajiriwa na Serikali za Mitaa. Hata hivyo, ni vigumu kujua kwa usahihi ni wangapi kati ya waliokwishahitim ufunzo wanaitumikia taaluma yao katika maeneo mbalimbali kutokana na ukweli kwamba baadhi yao wameshastaafu na wengine huenda wanafanya kazi tofauti na taaluma waliyosomea.

Na. 42

Wakulima Waliopewa Leseni Kupitia Mradi wa Msitu wa Nishati Ruvu

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Mwaka 2000 Serikali kupitia Mradi wa Msitu wa Nishati Ruvu ilitoa leseni ya wakulima zaidi ya 300 kutoka katika Kata za Msangani, Kongowe na Mkuza kulima kwenye hifadhi hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwamilikisha wakulima hao walioendeleza kilimo kwa takribani miaka 19?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kaskazini umehifadhiwa kisheria kwa Tangazo la Serikali Na. 309 la mwaka 1957. Mwaka 1999/2000 Serikali ikishirikiana na *Norwegian Agency for Development Cooperation (NORAD)* ilibuni mradi wa kuinua kipato cha wananchi wanaozunguka eneo la Hifadhi ya Msitu wa Ruvu Kaskazini kwa kupitia kilimo mseto ambapo mazao ya chakula pamoja na miti yalipandwa katika eneo moja. Katika kufanikisha hilo, jumla ya wakulima takribani 300 kutoka Kata za Msangani, Mwendapole, Mkuza na Kongowe walipewa eneo la ekari saba kila mmoja kufanya shughuli za kilimo kwa masharti maalum ikiwa ni pamoja na utunzaji misitu.

Mheshimiwa Spika, kutopteka na uharibifu uliokithiri pamoja na wakulima wengi kushindwa kutimiza masharti ya leseni walizopewa, mwaka 2015, Serikali iliamua kuachana na utaratibu huo na kuamua kuanzisha mradi mkubwa wa upandaji miti katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kumilikisha sehemu ya msitu huo kwa mtu au taasisi yeoyote. Kwa sasa, umefanyika uwekezaji mkubwa wa kupanda miti mbalimbali kibiashara. Kupitia uwekezaji huo, ajira takribani 2,000 zimezalishwa na zinaendelea kuongezeka kufuatia kuanzishwa pia viwanda vya kuchakata mazao ya misitu, hususan bidhaa za mimea ya bamboo.

Aidha, ili kukabiliana na mahitaji ya ardhi kwa wale wenye uhitaji, Serikali inatoa fursa ya kulima kwa mfumo wa kilimo mseto (*taungya system*), ambapo wakulima

wataruhusiwa kulima mazao kwenye maeneo yanayolimwa au kuvunwa miti kwa kibali maalum.

Na. 43

Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Mbogwe

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Mbogwe wanapata changamoto kubwa katika kupata huduma za kimahakama kwa kuzifuata Wilaya za jirani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya Mbogwe?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa majengo ni moja ya changamoto inayoikabili Mahakama ya Tanzania. Mahitaji ya Majengo ya kuendeshea shughuli za Mahakama hapa nchini ni makubwa. Kwa msingi huo, Mahakama imejiwekea utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na mpango wa ujenzi na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Mbogwe ni miongoni mwa Majengo ya Mahakama za Wilaya 33 yaliyopangwa kuanza kujengwa mwezi Juni na kukamilika mwezi Disemba, 2020 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Kwa sasa Mahakama ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za awali ili ujenzi wa majengo hayo uanze kwa muda kama ilivyotaka katika mpango wa Mahakama. Tayari Mshauri Elekezi amefanya mapitio ya michoro na ujenzi unatarajiwa kuanza kama ilivyopangwa.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza; kwa kuwa uendeshaji wa mashauri yaliyofunguliwa katika Mahakama ya Wilaya ya Bukombe kutokea Wilaya ya Mbogwe yanakuwa yakikabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo mashahidi kutofika kutoa ushahidi kutokana na umbali, je, Serikali inaonaje ikianzisha *Chamber Court* Wilayani Mbogwe ili kukabiliana na changamoto hii?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama za Mwanzo katika Tarafa za Masumbwe na llolangulu na kuifanyia ukarabati Mahakama ya Mwanzo Mbogwe?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama yalivyo majibu yangu kwenye swalii la msingi, ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya 33 nchini umepangwa kukamilika ndani ya miezi sita, kuanzia mwezi Juni na kukamilika mwezi Disemba, 2020. Hivyo, naendelea kumwomba Mheshimiwa Mbunge kuwa na uvumilivu ili jengo hili likamiliike ambalo litatatua changamoto alizozitaja kwenye swalii lake la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania imojiwekeea Mpango wa kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama kwa awamu. Aidha, Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo katika Tarafa za Masumbwe na llolangulu utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha. Ujenzi wa Majengo ya Mahakama 33 za Wilaya nchini utajumuisha Mahakama za Mwanzo katika jengo moja. Kwa mpango huo, Mahakama ya Mwanzo Mbogwe itakuwa ni sehemu ya Jengo la Mahakama ya Wilaya Mbogwe.

Na. 44

Miradi ya Uzalishaji Umeme wa Maji - Ileje

MHE. JANET Z. MBENE aliuliza:-

Ileje ina miradi iliyobuniwa kwa ajili ya kuzalisha umeme wa maji Mradi wa Luswisi na Ibaba, umeme huu ukizalishwa utaiwezesha lleje kuwa na umeme wa kutosha kwa mahitaji yake yote na ziada na kuuza:-

- (a) Je, Serikali itawasaidia vipi wananchi wa lleje katika kukamilisha miradi hii?; na
- (b) Je, Serikali itawasaidia vipi kuhakikisha usambazwaji wa umeme lleje unaharakishwa?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa lleje, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuzalisha umeme wenye uwezo wa Megawati 4.7 katika eneo la Luswisi Wilayani lleje. Gharama za mradi ni Shilingi Bilioni 19.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme Ibaba unafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kuitia Kanisa la Moraviani – Tukuyu ambapo mradi huu ulibuniwa kuzalisha umeme kuitia jua na kusambaza kwa wanakijiji. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi ulisusua kutokana na Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kupeleka umeme wa *grid* katika Kijiji hicho mwaka 2017. Kwa sasa mradi huo unasambaza nishati ya umeme katika maeneo ya Shule ya Msingi Ibaba na Kituo cha Afya Ibaba.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijiini (*REA*) inaendelea kuhakikisha Vijiji vyote vya Wilaya ya Ileje vinapata huduma ya umeme kupitia Miradi ya Wakala wa Umeme Vijijiini (*REA*) awamu ya pili na awamu ya tatu inayoendelea. Utekelezaji wa miradi ya *REA* awamu ya tatu utakamilika mwezi Juni, 2021.

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka
wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Kama mnavyojua, leo hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itahitimishwa baadaye na itahitimishwa kwa kupiga kura na zoezi hili linawahusu Waheshimiwa Wabunge wote tulimo humu kwenye ukumbi, lakini pamoja na Waheshimiwa Wabunge walioko katika kumbi nyingine ikiwemo ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, zoezi la kupiga kura Makadirio na Mapato ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sasa linaanza rasmi.

Utaratibu wa kupiga kura hatua kwa hatua ni kama inavyoonekana kwenye nyaraka iliyotumwa kwenu wiki iliyopita yenye kichwa, "Namna ya Kupiga Kura Katika Bajeti ya Wizara Kupitia Mfumo" ambayo ipo kwenye sanduku la taarifa za kiofisi kwenye *tablets* zenu.

Zoezi la kupiga kura litafungwa mara tu baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kumaliza kuhitimisha hoja yake. Yaani kuanzia sasa unapiga kura, una uhuru wa kuchelewa chelewa kidogo kwa kadiri unavyoona, lakini kuanzia sasa na kuendelea. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaposimama na kusema sasa anahitimisha hoja yake na Mawaziri

wakamuunga mkono hapa, maana yake ndiyo zoezi la kupiga kura linapoishia. Kwa sababu baada ya pale lazima tutamke matokeo ya kura zetu.

Kwa hiyo, unapiga kura kwenye kitufe kile kwenye *tablets* zetu, utakiona baadaye, chenye rangi ya kijani kwa anayesema ndiyo, rangi nyekundu kwa anayesema hapana na chenye rangi ya *blue* kwa yule ambaye hana uamuzi wa ndiyo au hapana. Mimi hapa nitapata moja kwa moja kura yako popote pale ulipo katika mazingira ya Bunge *including* jina na kila kitu. Wakati wa kutangaza, nitatangaza kama ni kura nyingi au zipi ambazo zimeshinda, lakini tunakuwa na *record/zote* zinazohusiana na upigaji kura kwa uhakika kabisa.

Kwa hiyo, sasa tunaendelea na hoja hiyo; na kwa kuwa muda ni mdogo, inanibidi nichunge muda. Ninao wachanglaji wachache watakaotuanzishia siku ya leo halafu tutakuja upande wa wachangiaji wengine ambaao ni Waheshimiwa Mawaziri. Baada ya hapo ndipo tutamkaribisha mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika wachangiaji wa leo, tunaanza na Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbewe na atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba. Mheshimiwa Mbewe. (*Makofii*)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji mchana huu, nami nitazungumza mambo mawili tu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu au kwa kipindi hiki tunakabiliwa na mambo mawili makubwa sana katika nchi yetu, janga la maambukizi ya virusi vya Corona na baadaye mwaka huu Uchaguzi Mkuu na haya ni mambo mawili makuu sana katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanzা nizungumze suala la *Corona*. Nazungumza kama mtu ambaye kwa bahati mbaya nime-experience tatizo hili katika familia yangu. Kwa hiyo, nalizungumza kama mtu ambaye nina uhakika na ninachokizungumza ni nini. Kwa sababu nilikuwa katika

isolation mpaka leo nilipotoka rasmi, namshukuru Mungu kwa hilo, ninapenda nishirikishe viongozi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kitu ambacho nafikiri pengine hatujakipa uzito wa kutosha katika kukabiliana na janga la Corona.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo ni *real*, wala Watanzania wasifikiri kwamba hili tatizo linaweza likazuiwa na mipaka ya nchi yetu. Kwa hiyo, ni wajibu kabisa wa Serikali na wadau wengine wote kushirikiana katika kuhakikisha jambo hili linapewa uzito unaostahili kama ambavyo Mataifa mengine ambayo yame-experience tatizo hili yanavyopitia.

Mheshimiwa Spika, mbali na tahadhari mbalimbali ambazo zimetolewa na Serikali bado kuna uzembe mkubwa sana mionganini mwetu, aidha kwa kujuu ama kutokujua, ama kufikiri tatizo liko mbali na haliko mikononi mwetu. Kwa upande wa Serikali, naomba nishauri kitu kimoja; itakuwa ni dhana ya bahati mbaya sana kufikiria jambo hili ni kazi ya Serikali peke yake. Jambo hili ni lazima lishirikishe wadau wote, lakini kwa vyovyote itakavyokuwa, lazima Serikali *i-take a leading role* na Serikali nina hakika ina wajibu wa *ku-take a leading role*. Hili ni jambo ambalo linahusu taasisi binafsi, sekta binafsi, Mashirika ya Umma, nyumba zetu za imani na ibada, tunahitaji *effort* ya Kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushauri mkubwa ambao napenda kuutoa katika Bunge lako ni kuunda *a National Taskforce* ambayo itasimamia masuala yote yanayohusu Corona. Serikali iongeze hii *taskforce*, lakini ishirikishe wadau wengine, wanazuoni, madaktari, hospitali binafsi na taasisi mbalimbali za nchi ili jambo hili lipewe uzito wa Kitaifa. Lisiachiwe Serikali peke yake kwa sababu Serikali ni sehemu ya uongozi, lakini kuna wadau wengine huku nje ambao ili nao wakielimika wanaweza wakajua na wakaisaidia Serikali katika kufikia malengo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili tatizo la Corona ni kubwa sana na watu wengine mpaka sasa hivi wanalionia kwamba kwetu halijawa kubwa kwa sababu pengine watu wengi

wakaathirika na wakapata maafa, lakini ukweli maafa ya *Corona* tayari yameshaingia katika uchumi wetu. Nilitegemea sana katika bajeti ya mwaka huu Serikali ingekuja na mpango maalum kabisa wa kibajeti na kutoa taarifa katika Bunge hili kwamba hivi tuna athari kiasi gani za kiuchumi zinazotokana na janga la *Corona*? Ukiangalia mipango ya Serikali mpaka sasa hivi, labda yatabadilika baadaye, bado mipango iko kama *business as usual*, bajeti ziko pale pale, hatuja-foresee kushuka kwa mapato makubwa sana ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Sekta ya Utalii ambayo ni sekta inayoingiza mapato makubwa ya fedha za kigeni, hii sekta imeanguka kabisa, yaani hii kwa asilimia 99. Hoteli zimefungwa, kampuni za *tourzimefungwa*, *facilitieszote* za kitalii zimefungwa, mashirika ya ndege ya Kitaifa na Kimataifa haya-*operate*. Hali hii halta-*recoverbaada* ya wilki mbili, hili anguko la kibiashara kwenye upande wa utalii, *impact* yake ni mwaka mzima, kwa sababu wageni wame-*cancel booking* mpaka Desemba, mpaka *new year*. Kwa hiyo hili siyo jambo la leo au kesho. Ni lazima Serikali iweze ku-*foresee* haya mambo.

Mheshimiwa Spika, tunapojadiliana bajeti hapa, mpaka sasa hivi katika bajeti za nchi utaona kwa kiwango kikubwa sana utekelezaji wa mipango mingi ya Serikali ulikwama njiani kwa sababu ya mapato kuwa kidogo. Sasa bado tunakwenda kuangusha mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, biashara zinaanguka, *foreign direct investments* sasa hivi zitakuwa *almost suspended* kwa mwaka mwengine mmoja, misaada kutoka nchi mbalimbali ambazo zilikuwa zinatusaidia nina hakika zitapunguza misaada kwa sababu ya hali yao wenyewe katika nchi zao; uwekezaji wa ndani vilevile sasa hivi umeingia katika mashaka makubwa; uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za nje ambao unachangia kwa kiwango kikubwa sana mapato ya Serikali, unaanguka; mashirika na makampuni mengi yatafunga kazi na wafanyakazi watakuwa *retrenched*, lakini siaona hili

jambo likichukuliwa uzito wa kutosha kwenye bajeti yetu ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kama tunaendelea na kufanya mipango yetu ya bajeti vile vile kama vile hakuna tatizo lilitotokea, wakati tuna-*expect* mapato ya Serikali yataweza kupungua *almost by 40%* katika kipindi cha miezi sita ijayo, tunawezaje kutekeleza bajeti zetu za kiserikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo nilitamani sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie, Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie tuwe na mipango ya pamoja na wala tusione aibu katika kukabiliana na janga la *Corona*. Ni vyema tukajiandaa mapema kwa kutafuta *mitigation factors* gani zifanyike ili kujaribu kupunguza hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, inawezekana tukalazimika kuacha baadhi ya miradi yetu mikubwa ambayo tunaipenda. Tunaipenda sana na tungetamani ikamilike, lakini inawezekana kabisa kabisa tukashindwa ku-*fund* miradi hii kwa sababu mapato ya Serikali ni lazima yatashuka. Kama tunadanganyana kwamba mapato ya Serikali hayatashuka, siyo kosa la mtu yejote, ni kosa la ugonjwa huu na ni lazima tukabiliane na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo tukichukua tahadhari hizo, ni lazima tuongeze fungu kubwa la fedha kwenda katika *facilities* mbalimbali zinazotoa huduma kwa wananchi hasa mambo ya kiafya. Kuwaambia watu wanawe tu mikono; tunaona *information* ambazo ni *contradictory*. Wakuu wa Mikoa wanatoa matamko mbalimbali na maelekezo mbalimbali, watu waendelee kukusanyika na kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajiliza, Serikali mbona inakuwa na kauli mbili mbili! Kuna mikusanyiko tunaiona kwamba haifai, siyo ya lazima kwa tafsiri ya Serikali, lakini kuna mikusanyiko ya ghafla, Wakuu wa Mikoa wenyewe wanafanya majumuiko ya watu, wanakusanya watu, wanahutubia watu, wanawaambia watu *Corona* iko mbali.

Haya ni mambo ya hatari. Sasa Serikali inasema nini? Tumsikilize nani?

Mheshimiwa Spika, natamani tumsikilize Mheshimiwa Rais wa nchi, ningetamani tumsikilieze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Afya. Hawa ndio mamlaka ambazo tumeambiwa zitatoa kauli kuhusiana na ugonjwa wa *Corona*. Sasa kila Mkuu wa Mkoa na kila Mkuu wa Wilaya anakazana kutafuta kutoa maelezo katika maeneo yake. Mimi nafikiri hii nchi tukienda hivi huu ugonjwa utatupeleka mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Spika, katika hili la Corona, ni bora tujiandae hata kama tunaona janga liko mbali ili janga likifika tukute tumejiandaa kuliko kutokajiandaa tukafikiri liko mbali halafu likafika, litakuwa fedhea kwa nchi. Na lazima tujifunze kwa nchi za wenzetu, jamani sisi hatuishi wkenye mipaka na siyo vibaya kujifunza kwa wenzetu siyo siri hili tatizo limekumba dunia, hebu angalieni wenzetu wa Rwanda wanafanya nini, tuangalie wenzetu wa Kenya wanafanya nini, hawa wenzetu siyo wajinga na mipaka yetu sisi ni ya jamii hiyo moja Kenya na Tanzania jamii ni hiyo hiyo moja na Uganda na Rwanda. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sasa nitake nisisite kwamba hili jambo linahitajiwa kuundiwa *national task force* tuanze kuangalia athari za kiuchumi, athari za kijamii, tufanye nini tuache nini, hatuwezi kuendelea na mipango yote kama tunavyofanya siku zote hiki ni kipindi cha *prioritize*, yaani tuamue *priority* za Taifa katika kipindi hiki cha corona ni nini, lazima tu *suspend* baadhi ya mipango ya Serikali ili kuwezesha kukabaliana na tatizo ambalo linajitokeza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ningependa nizungumze kuhusiana na uchaguzi, leo tuna kama miezi tu *actual process* za uchaguzi zimeasha, lakini ukiangalia tumekuwa tunadai kwa muda mrefu sana, jamani tutengenezeeni maridhiano katika nchi tutengeneze Tume huru ya Uchaguzi. Uchaguzi ni *process* na hii *process* ni ndefu, uwandikishaji ni sehemu ya *process*, upatikanaji vifaa ni

sehemu ya *process*, kurekebisha Sheria bali tunavyokidhi na matatizo ni sehemu ya *process*, lakini siye umekuwa tunadai *minimum reform* kwa sababu moja tu, kwamba tunaamini kwamba ili nchi iweze kuendelea vizuri, lazima ipate viongozi wanaopatikana kwa misingi ya kidemokrasia, tunaimani kwamba wawakilishi wananchi lazima wapatikane kwa misingi ya kidemokrasia. Ili jambo linahitaji *political will* wala siyo kushindana kupiga kelele. (*Makofii*)

Mheshimwa Spika, nimemwandikia Mheshimiwa Rais, tumesema mara nyingi tumezungumza mara nyingi katika *forum mbalimbali*, kwamba jamani tunaposema tunataka *minimum reforms*, marekebisho machache ya Sheria kwa sababu mtakumbuka 2015 wakati mchakato huu wa Katiba mpya unashindikana makubaliano na Mheshimiwa Rais wakati ule Mheshimiwa Jakaya Kikwete yalikuwa tuende basi angalau kwenye *minimum reform* mpaka tutakopomaliza mchakato mzima wa Katiba. Bahati mbaya ile *process* haijarudia mpaka leo.

Kifungu namba 74 na namba 75 katika Katiba yetu vinahitaji marekebisho machache, na haya mambo kama kuna *political will* upande wa Serikali haya mambo yanawezekana, tukaenda kwenye uchaguzi watu tumeridhiana, tumekubaliana, uchaguzi haki akichaguliwa huyo, akichaguliwa yule basi tupate viongozi ambao wamepatikana kwa ridhaa ya wananchi na siyo kwa giliba za mifumo ya kiuchaguzi. (*Makofii*)

Mheshimwa Spika, sasa Katiba ina matatizo yake mapungufu, ambayo marekebisho yake ya kufanya kwa sabau zamani *minimum reforms* ni machache, kifungu cha 74 na 75, halafu kuna masuala ya Sheria za uchaguzi tumeainisha Sheria mbalimbali tumeshapeleka taarifa hizi Serikalini bwana mkubwa mwenyewe kwamba kuna maeneo mbalimbali yana *criminalize process* zima ya uchaguzi. Kuna watu wengine wanaenguliwa kwenye *process* ya uchaguzi kwa sababu tu eti amekosea kuweka nukta hapa vitu kama hivyo ambavyo vinavuruga ile dhana ya kupaya viongozi bora.

Mheshimwa Spika, kwa hiyo, tunachosema sisi ni kama tunahitaji hizi *minimum reform* zifanyike, na nina hakika bado huo muda tunao, hata Bunge hili kabla halijaifa, kama kuna *willingness* na *political will* ya kutafuta mwafaka katika Taifa, kutafuta amani ya kudumu na maridhiano katika Taifa haya mambo bado yanaweza kufanya siyo mambo magumu ya kuhitaji bajeti maalum hapana, ni mambo ambayo yanawezekana, tumeainisha mambo chungu mzima katika Sheria ya uchaguzi na Katiba ambayo yanafaa kufanyiwa *reforms* ili kuwezesha jambo hili kufanyika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge, nilikutaja Mheshimiwa Jumanne Kibera Kishimba na atafuatiwa Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimwa Spika, yeah, ahsante sana, naungana na Wabunge wenzangu kuchangia Wizara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza nichukue nafasi hii kumpata pole Mheshimiwa Mboge kwa ugonjwa wa mtoto wake huu wa corona ambao ulimpata. Nampongeza Mheshimiwa kwa busara kubwa sana aliyotumia kupambana na hili janga la corona, hasa kwa kuzingatia watu wetu ni matabaka mbalimbali, tuna wafugaji, tuna wakulima, tuna wavuvi, tuna wafanyabiashara, na tuna watu wa hali ya chini sana, Mheshimiwa Rais alichotumia kama asingetumia hekima leo nchi yetu ingekuwa na *disaster* kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo tu kwa sisi wafugaji au wakulima ukiambiwa kwamba usimtoe ng'ombe kwenda kuchunga ingekuwa kazi ngumu sana maana yake ng'ombe hata kama wewe mwenyewe umefariki ng'ombe lazima waende wakale. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimwa Spika, sisi tunalima mpunga...

SPIKA: Mheshimiwa Kishimba unavunja kanuni kumfikiria kwamba Spika amefariki. (*Kicheko*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimwa Spika, hapania. (*Kicheko*)

SPIKA: Endelea kuchangia Mheshimiwa.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimwa Spika, tuna wakulima wa mpunga, wa mtama ambaa lazima waende shambani kwenda kuangalia ndege ingawaje kama watu hawataruhiwa kutoka basi chakula chote kitakuwa sikukuu ya ndege. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tunaishukuru sana Serikali kwa kuondoa tozo la maiti kwenye hospitali wakati mtu amefariki akiwa anadaiwa, ingawaje baadhi ya hospitali bado wanakataa wakisema kwamba hawajapata waraka. Tunaomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya kwenye majumuisho yake ajaribu kutueleza vizuri au atoe waraka huo au atamke ili Sheria hiyo iweze kuanza kutumika hasa wakati huu mgumu sana wa watu wetu wanaokutana nao. (*Makofi*)

Mheshimwa Spika, tungeomba pia wenzetu wa hospitali na zahanati za binafsi wapunguze au hapa nusu mtu anapofariki, hali kule vijijini ni mbaya sana, *sorry*. Mwenendo wa ugonjwa huu wa corona ni hatari sana tungeomba Serikali kama inaweza kuwasamehe madaktari walioko Magerezani na Wauguzi wa afya ili waje tuungane nao watusaidie wakati huu. Vilevile kama inaweza Serikali madaktari na wauguzi waliostaafu kama inaweza kuwapa mkataba wa muda inaweza ikatusaidia sana maana yake wapiganaji wetu sasa hivi kwenye hii vita ni wauguzi wa afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba vilevile wenzetu wa Idara ya Afya kuna zahanati au hospitali ambazo wamezifungwa tungewaomba sana kama wanaweza muda huu wakarekebisha masharti ili hospitali hizo na zahanati ziendelee kuhudumia watu, itatusaidia sana maana yake hali

ilivyo kama vile kama siyo watu wetu wa afya na Wizara ya Afya kufanya udhibiti ni vizuri watusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimwa Spika, napenda vile kuungana na wewe juzi hapa wakati wa mchango na Mheshimiwa mama Prof. Tibaijuka na Mheshimiwa Ngeleja waliliongea sana suala la dawa za kiejeji. Ni kweli tumekuwqa tukipambambana na mafua kwa muda mrefu sana na wenyiji wanaoutalaam wa mafua sitaki kusema kwamba ni corona, lakini ni vizuri wenzetu wa Wizara ya Afya wakafikiria sana suala la kuongea na wenyiji ili kupata mahala pa kuanzia tutegemea tu kwamba tunategemea kwamba lazima dawa ipatikane Ulaya, au chanjo ni kazi ngumu sana ni vizuri wataalam wetu waungane na wenyiji ambao wamekuwa wakipambana na mafua kwa muda mrefu sana kabla ya dawa za kizungu hazijaja, itatusaidia sana kupambana na hili tatizo najua wote tunakuwa na maeneo yanayoongewa mitaani ni kwamba inawezekana watu weusi wanaweza wakajidhibiti wenyewe au nini.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wataalam wa afya wasiogope, na wasiogope kabisa kutamka kwamba kitu hiki kiko hivi kwa kuogopa kwamba labla watavunja wataalam wao, hapana ni vizuri watamke kabisa kwamba kitu hiki kinaweza kuwa hivi, kitu hiki kinaweza kuwa hivi, itatusaidia sana sasa hivi kuna mkakanganyiko mkubwa sana kila mtu anaamuka na la kwake matokeo yake watu wetu wanakuwa kwenye wakati mgumu sana ni vizuri watu wa Wizara ya Afya wawe na msimamo ambao utatuendesha vizuri kukumbana na hili tatizo.

Mheshimwa Spika, kuna hizi mashine za *oxygen*, tungeomba wataalum wetu wa afya watoe *relief* kidogo kama mtu anaweza kutengeneza hata kama ina *capacity* ndogo waruhusiwe kama za zamani zipo zifanyiwe marekebisho, kusema tu kabisa tunahitaji kupata kitu kipyaa, tunaona wenzetu wa Ulaya ambao wameendelea na ndiyo wanatengeneza wameshindwa kabisa machine hazitoshi, endapo tatizo hili litatokea tunaweza kuwa kwenye wakati mgumu sana. Tunaomba sana wenzetu wa afya Serikali

iruhusu kama watu wanaweza kuagiza iwafikirie haraka ili hili tatizo tuweze kukabiliana nalo. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbobe ameeleza vizuri kwamba suala hili ni bora tukajjandaa nalo hatuna namna yoyote ambayo tunaweza kukabiliana nalo maana yake liko kwa jirani zetu, vilevile linatuathiri kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Afya akaitisha kongamano ambalo litajumuisha wataalam wote wa *pharmacy* watengeneza madawa, vilevile na waganga wa tiba za asili ili waweze kukaa pamoja tuweze kupata nini hasa kilichoko ndani ambacho kinaweza kutusaidia wakati tunasubiri dunia ifanye nini.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, amekuwa akifuatilia hoja zetu Bungeni, tulikuja hapa na hoja ya *spirit* ambayo ni gongo, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amechukua gongo ile ameipelekwa kwenye maabara, na kwenye maabara imeonekana inafaa kuliko *spirit* zilizopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunamuomba Mheshimiwa Waziri wa Afya sasa kwa kuwa wananchi wetu hawawezi kununua hizi sababu tunazotumia ambazo zina *alcohol* asilimia 65, atamke basi wananchi kwa muda huu wa dharura wanaweza kunawia gongo? Ili kuzuia hilo suala ya corona. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii *sanitizer* tunayonawia ina *alcohol* asilimia 65 na gongo ina *alcohol* asilimia 55, basi Mheshimiwa Waziri wa Afya kama anaweza kutoa sasa hivi msamaha huo ili iweze kutusaidia...

SPIKA: Jamani anayechangia ni Profesa naomba msikilize vizuri wengine hata hamjui *alcohol content* ya gongo. (*Kicheko*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, nakwenda *direct* kwenye suala la uwekezaji maana yake najua Ofisi ya Waziri ndiyo inayohusika na uwekezaji, wote

tumeuangalia kwenye eneo viwanda, mahoteli na maweneo mbalimbali. Lakini tunaomba Ofisi ya Uwekezaji iruhusu uwekezaji wa mawazo, mimi nafikiri ni uwekezaji mzuri kuliko uwekezaji wowote, nitatoa mfano ingawaje muda mdogo unakimbia. Nikiwa Zimbabwe ndiyo niligundua uchenjuaji wa dhahabu kwenye mchanga na kwa malundo ambayo yamekuwepo hapa ya dhahabu zaidi ya miaka 50 nilivyokujanayo hiyo teknoloji ilinichukua miezi miwili mitatu nikanyang'anya, lakini kwa kuwa hakuna namna wala kitu unachoweza kudai sikuweza kufanya kitu chochote... (*Makofi*)

SPIKA: Ni kengele ya mwisho, nakupa dakika mbili umalizie.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimwa Spika, ningeomba Wizara ya Uwekezaji kama itatengeneza kitengo mtu akiwa na wazo kokote aliko ambalo akililetta hapa wananchi wanaruhusiwa kuli-copy, lakini ye ye apate *per cent* kutoka kwenye lile wazo, maana yake wanachokamatilia wao ni wazo ambalo limeshikiliwa kwenye computer, lakini wazo ambalo ukililetta uwezi kuwazuia wananchi, lazima walichukue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wenzetu wawekezaji wabadilishe mwelekeo ili tuelekee kwenye eneo lingine eneo la mawazo linaweza kuwa rahisi kuliko leo watu wanasema kwamba huyu kafa na dawa yake, lakini angesema huu mti ni dawa atapanda lini ye ye, lakini wenyewe watasema ukitamka mtii huu ni dawa Mheshimiwa Dkt. Karemani ananitazama, wakisema hii ni dawa Mheshimiwa Dkt. Kalemani anayo dawa ya mifupa, kama anaweza kupewa *ku-share* kwenye kile kinachopatikana ingekuwa bora sana na tusingehangaika na mikutano na kitu chochote, mawazo dunia nzima inayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia bei ya dhahabu imeanguka sana, kwenye masoko yetu, lakini kwenye soko la dunia, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikilize vizuri sana. Dhahabu imeanguka asilimia 50 mpaka 40 kwenye

masoko yetu ya ndani, lakini kwenye soko la dunia haijaanguka, kwanini sasa Benki Kuu isiingie ndani ikanunua hiyo dhahabu kwa wakati huu ili iweze kupata hiso faida maana yake kuna *gap* kubwa sana kwenye siku kumi kabla ugonjwa haujaanza kudorora, lakini bahati nzuri kama wenyewe wanaogopa Benki Mkuu humu tuna Wabunge zaidi ya watano wanaojua dhahabu vizuri sana, hata kama ni kuvunja kanuni basi awachukue hao hawa Wabunge waliomo humu ndani wasimamie zoezi hilo la ununuza wa dhahabu ili Serikali ipate faida, ni vizuri sana wanasema kufa ni kufahana, ni vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba, nilishamtaja Mheshimiwa Sonia Magogo, wanagawana dakika tano tano na Mheshimiwa Khatibu, dakika tano Sonia.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu. Moja kwa moja nitaenda kuanza kwenye suala hili ambalo limekuwa kama ni janga la kitaifa ugonjwa huu wa corona na *cosign* yangu moja kwa moja itakuwa kwa watu vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sasa hivi sisi watu wa mijini tunapata hizi taarifa za ugonjwa wa corona kuititia kwenye mitandao na vyombo vyya habari, lakini ukitathimini kwenye vijiji vyetu sehemu nyingi hawana *access* ya hii mitandao. Kwa hiyo, Napata shaka kidogo kwamba nao wanaweza wakawa na ufahamu ama kupata taarifa sahihi kwa kiwango kile ambacho sisi watu wa mjini tunapata.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo mjini tumeona sasahivi maeneo mengi tunatumia maji na sababu kunawa mikono ili kujikinga na haya maradhi ya corona. Lakini kwa vijiji vyetu maeneo mengi wanauhaba wa maji, unakuta haya maeneo mtu hata yale maji kujikimu yale mahitaji ya muhimu

anashindwa kuyapata. Sasa sidhani kama mtu anatafuta maji kilometa kadhaa anakuja na ndoo moja kwa ajili ya kupata maji walau ya kupikia kama anaweza akayatumia yale maji kwa ajili ya kusafisha mikono kama tunavyofanya huku mijini. (*Makofi*)

Mheshimwa Spika, hivyo ningeliomba Serikali iangalie inawasaidiaje hawa watu wa vijijini, kama inawezelekana kuwapatia hizi *sanitizer* ili waweze kuzitumia ziwe mbadala wa maji kule vijijini, kwa sababu *tuta-control* mjini peke yake na vijijini kukawa bado kuna hiyo *loophole* ya kueneza huu ugonjwa bado kuna watu wanatoka vijijini wanakuja mjini, bado kuna watu wanatoka mjini wanawenda vijijini. Kwa hiyo maambukizi bado yatakuwa na nafasi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeona kwa Mkoa kama Mkoa wa Dar es Salam sasa hivi bodaboda zimekuwa kama ndiyo kama ndiyo nafasi kubwa sana ya usafiri na wameruhusiwa sasa hivi mpaka kuingia katikati ya mji, lakini wasiwasi wangu unakuja kwenye zile elementi ambazo wanavaa abiria, kwa sababu akitua abiria mmoja anakuja kuvalaa abiria mwagine na huwezi kujua kati hao ni nani anaweza akawa na virusi vya corona.

Mheshimwa Spika, kwa hiyo, niombe kama inawezelekana walau huu utumiaji wa elementi uzuwe kwa kipindi ili kuepusha haya maambukizi kuenea kwa kasi. Sambamba na hili nilikuwa napenda kuishauri Serikali, kwa upande wa wauguzi ina maana manesi na Madaktari, ningependa kufahamu Serikali imejipangaje ili kudhibiti haya maambukizi kwa hawa watu ambaa wanakuwa *direct* moja wka moja wanakuwa na *direct contact* na wale watu ambaa wana virusi vya corona. Lakini wakati huo huo tunaona maeneo mengi kuna uhaba wa Madaktari nitolee mfano kwenye Wilaya yangu ya Handeni.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati huo huo tunaona maeneo mengi kuna uhaba wa madaktari. Nitolee mfano kwenye Wilaya yangu ya Handeni. Wilaya ya Handeni katika

Hospitali yetu ya Wilaya ina madaktari watano na tuna uhaba wa madaktari karibia 24. Hospitali ile imekuwa ikisaidia hadi Wilaya za jirani kama Kilindi na Manyara. Kwa hiyo, ukiangalia huo uwiano wa madaktari ambao tunao pale na ukubwa wa eneo ambalo wanatoa huduma na hili janga la *Corona* ambalo lipo inatupa mashaka makubwa. Hivyo niiombe Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza bajeti kwenye Kitengo cha Afya ili kuweza kuendana na hii hali ambayo tunayo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine naomba kuongelea kuhusu miundombinu, miundombinu yetu sasa hivi imekuwa mibaya sana kutokana na hizi mvua ambazo zimenyesha. Ukiangalia hata hapa Dodoma tu maeneo mengine kufikika imekuwa ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Nilishakutaja Mheshimiwa Khatib dakika tano.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama hapa dakika za mwisho mwisho, dakika za majeruhi.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani za dhati na pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Afya, kwa jinsi wanavyochukua juhudui katika kushughulikia janga hili la dunia maana hili siyo janga la Taifa ni janga la Dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme kitu kimoja. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Waziri Mkuu wa Tanzania na juhudui anazozichukua ni kwa ajili ya Taifa zima la Tanzania. La

kusikitisha na jambo ambalo limenifanya leo nimuombe Mheshimiwa Spika kwa bidii zote angalau kunipa hizi dakika tano ili nikupe ujumbe huu ni kwamba kuna mchezo na mzaha mkubwa juu ya maisha ya watu Zanzibar kuhusu ugonjwa huu wa *Corona*. Upo mchezo, mzaha na dharau.

Mheshimiwa Spika, kuna Waziri mmoja alikuwa safari nje ya nchi aliporudi Zanzibar akiwa katika hali ya kuumwa alikataa kukaa kwenye karantini. Waziri huyu Salama Aboud Talib alienda kukaa nyumbani kwake ugonjwa ulipomzidia alirudi hospitali ya umma ya Mnazi Mmoja. Taarifa na uamuzi wa Serikali ni kwamba wagonjwa wote wanaohisiwa kuwa na ugonjwa wakae karantini, alikataa, ndani ya muda wa siku tatu ameng'ang'ana kukaa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Baada ya kuonekana hili jambo limekuwa kubwa na minong'ono na malalamiko kuwa mengi ndiyo alikubali kuwekwa karantini kwa nguvu. Athari yake tayari nyumbani kwake wapo wawili aliowaambukiza na pale hospitali haijulikani ni nini kilichoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alifanya hivi kwa sababu ya kiburi cha madaraka yake. Nachukua fursa hii kumpongeza sana Makamu wa Rais wa Zanzibar alipotoka safari alikwenda kukaa kwenye karantini yeeye mwenyewe bila kulazimishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo utu na uongozi. Leo Waziri huyu aliyekiye amri ya Serikali, amri yako wewe Waziri Mkuu na hata amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nani yeeye na kiburi hiki kakitoa wapi?

Mheshimiwa Spika, jana tumeona kwenye taarifa za habari za Kenya, Naibu Gavana ametoka pale hospitali na pingu anaenda kusulubiwa. Kwa sasa hatuwezi kumchekea mtu kwa sababu ni Waziri au ni nani, lazima Mheshimiwa Waziri Mkuu hili alichukulie hatua haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, isitoshe baada ya kiburi hiki, kuna mpumbavu mwingine anaitwa Hafidh, ni daktari, hadi ninavyoongea ameng'ang'ana hospitali hali ya kuwa

ameathiriwa na ugonjwa huu wa *Corona*. Yuko pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa nini anafanya hivi? Ni kwa sababu ana nasaba au ukoo wa wakubwa. Hii ni hatari inayofanyika Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema wakubwa wa Zanzibar wanawaogopa watu hawa lakini nachosema ni mchezo unaofanywa kwa kuhofia watu na madaraka yao. Leo Uheshimiwa wake ni kwa sababu ana uhai wa Mwenyezi Mungu, anapumua, dakika moja akifumba jicho anageuka anakuwa marehemu, sasa na awe marehemu yeye asiue wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taharuki iliyopo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja baada ya matukio hayo ni kubwa. Hivi ninavyoongea nataka Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilile huyu Daktari anayeitwa Hafidh kama bado yupo pale Mnazi Mmoja au amekubali kwenda karantini? Kwa sababu kauli anazotoa kwenye mitandao ya *Facebook* anasema hakuna yeote anayeweza kumfanya lolote, anazitoa yeye mwenyewe. Pia matusi anayotukana, hayawezi kusemeka kwenye hadhara ya watu wastaarabu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mambo haya yanafanyika Zanzibar. Sasa tufanye nini? Kuna msemo wa Kiswahili unasema: "Zumari ikipigwa Chopocho Pemba anacheza wa Mtwara". Haya maradhi yakianza popote ndani ya nchi ujue ni athari kwa Taifa zima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anaogopewa vipi mtu huyu? Hivi vitu vinasikitisha sana. Tukiangalia juhudzi za Serikali, Taifa na dunia imekaa katika *tension* lakini kuna watu kwa sababu tu eti naitwa Waziri anaamua kuhtatarisha maisha ya watu. Huyu mtu wa namna hii anatakiwa akia mtu na yeye auliwe. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Khatib. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Nape Nnauye atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambapo imeeleza mambo mengi kwa kweli ambayo yamefanyika na mengi ameyachukua yaliyofanyika katika kipindi cha miaka mitano ambayo amepewa dhamana na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, nitoe pole kwa tatizo la *Corona* linalotukabili Watanzania. Naamini Mwenyezi Mungu atatuepusha pamoja na kuchukua tahadhari mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015, Chama cha Mapinduzi tulitengeneza llani ya Uchaguzi. Wakati tunaitengeneza llani tuliweka kazi zitakazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Tulipoikamilisha tukaanza kumtafuta mtu atakayefanya kazi tuliyoiweka kwenye llani. Wakati ule walijitokeza watu wengi walioomba kazi hiyo na Chama cha Mapinduzi mwishoni tukamteua Mheshimiwa John Pombe Magufuli kufanya kazi ya kutekeleza llani. Hakuteuliwa kwa bahati mbaya, tuliona ana uwezo wa kuifanya kazi tunayompa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haikuwa bahati mbaya, chama hiki ni kikubwa sana. Tulitengeneza kazi, tukamtafuta mtu mwenye uwezo, jasiri, mzalendo ambaye atakwenda kutekeleza kazi tulyiompa. Sina mashaka chama hiki kikifanya tathmini leo tulyempa kazi amefanya vizuri na hivyo anastahili kupewa tena miaka mingine mitano ya kukamilisha kazi tulyiompa lakini pia tumpe nafasi nyngine kwa sababu amefanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitapitia maeneo machache. Eneo la kwanza, llani ya Uchaguzi ilimtaka huyu tutakayemba kazi yeye na Serikali yake, wafanye kazi ya kutafsiri ukuaji wowote wa uchumi kwenye maisha ya kawaida ya Watanzania. Kazi hii imefanyika vizuri sana kwa takwimu ambazo zimo ndani ya hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza lilikuwa ni kwenye afya. Kwenye afya tulitaka tusogeze hizi huduma za afya na kuziboresha. Katika kipindi cha miaka mitano Serikali ya Awamu ya Tano imejenga vituo vya afya 352. Kama uchumi usingekuwa una-perfom isingewezekana kufanya kazi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano zimejengwa hospitali 67 za Wilaya. Hata Jimbo langu la Mtama siyo Wilaya lakini tuna Hospitali ya Wilaya. Kazi hii imefanyika vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna mikoa mipyä ambayo ilikuwa haina Hospitali za Rufaa. Mikoa ya Njombe, Songwe, Katavi, Geita na Simiyu zimejengwa Hospitali za Rufaa na kazi inaendelea vizuri. Pia zimejengwa Hospitali tatu za Kanda: Kanda ya Kusini tuna Hospitali Mtwara; Kanda ya Magharibi tuna Hospitali Tabora; na Kanda ya Ziwa inajengwa hospitali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kazi hii, sina mashaka chama changu kitampa fursa tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli awe mpeperusha bendera mwaka huu. Sina mashaka kwamba Watanzania wameona tafsiri ya kukua kwa uchumi kwenye huduma za afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upande wa umeme, nilikuwa naangalia takwimu mpaka asubuhi tayari tumeshakwenda kwenye vijiji zaidi ya 9,000. Vijijini kabisa umeme unawaka. Kama uchumi ungekuwa hauendi sawa kazi hii isingewezekana. Kazi hii imefanyika vizuri tafsiri yake ni kwamba maisha ya watu yanabadilika, inaonesha kwamba kuna kazi nzuri ya uchumi inakua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, elimu, kila mwezi zinatolewa zaidi ya shilingi bilioni 24 kwenda kwenye elimu bure. Tulisema kwenye llani ya Uchaguzi tutatoa elimu bila ada shilingi bilioni 24 kila mwezi zisingewezekana kama siyo kazi nzuri ya kutafsiri ukuaji wa uchumi kwenye maisha ya kawaida ya watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye maji kuna takwimu nyingi nzuri. Kwenye maji kuna ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi mbalimbali ya maji, Arusha, Babati, Dodoma, Kigoma, Iringa, Lindi, Musoma, Morogoro, Moshi, Mtwara, Mwanza, Sumbawanga, Shinyanga na mingine mingi. Kama isingekuwa uchumi umekwenda ndiyo maana fedha zikapatikana kupelekwa huko, kazi hii isingewezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili la kwanza tulimpa Mheshimiwa Dkt. Magufuli alifanye. Mimi kama Mwenezi Mstaafu wa Chama ambaye nilisimamia utengenezaji wa llani ya Uchaguzi nataka niseme kazi imefanyika vizuri na tuna sababu ya kumpa tena fursa Mheshimiwa John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati mzuri wa kufanya tathmini. Kazi ya pili, kwenye llani ya Uchaguzi tulimpa Mheshimiwa Magufuli kazi ya kubadilisha utamaduni wa namna tunavyofanya mambo kwenye nchi yetu. Ndiyo maana tukawa na kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu, wapo watu wengi pengine hawajui. Tuliiweka kwa makusudi kwa sababu ulianza kujengeka utamaduni, mtu unaweza ukawa unafanya kazi unapata kipato kikubwa hakilingani na kazi unayoifanya. Wakati mwengine biashara hewa au kazi hewa, tukasema lazima tubadilishe utamaduni huu ili nchi yetu iende.

Mheshimiwa Spika, kwenye uchumi ndiyo vyuma vinakaza lakini vinakaza kwa sababu wakati mwengine tulizoea dili, dili zikifungwa kwa vyovoyote vile vitakaza. Kwa mujibu wa llani ya Uchaguzi uksikia kelele maana yake kazi hii imefanyika vizuri. Ndiyo maana itabidi tumpe fursa tena

kwa miaka mingine mitano amalizie kazi ambayo alikuwa ameshaianza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye siasa, siasa na yenye we ilishazoea hivyo hivyo, kuna kelele ndio lakini leo ukangalia namna tunavyofanya tumekuwa *more serious*. Nimeona watani zangu CHADEMA wamefanya Uchaguzi, angalia uchaguzi walivyofanya, angalia walivyofanya ACT kwa vyovytile kuna mabadiliko hata kwenye namna ya kuendesha siasa zetu ambayo naamini ni kazi nzuri ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina-recommend kwamba kwa kweli Mheshimiwa Magufuli na Serikali yake wamefanya vizuri. Nimpongeze Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Mawaziri, Watendaji wa Serikali, Vyombo vya Ulinzi na Usalama wameitendea hakiliani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata mtaani hali imebadilika, watu kidogo wako *serious*, hii ndiyo kazi tuliyomtuma Mheshimiwa Magufuli. Mwalimu alituambia ukiwa unasafisha nyumba unaweza ukafagia shilingi, kufagia shilingi hakufanyi nyumba isisafishwe. Mimi naamini upungufu wa hapa na pale katika kutengeneza mambo haya tukakanyagana vidole yatumike vizuri kutusaidia turekebishe mambo siku za usoni ili Tanzania iendeleee kuwa nchi njema ya fursa ya kila mmoja. Kwa hiyo, kwa kweli niipongeze sana Serikali kwa kazi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu nikupongeze Bunge la Kumi na Moja limefanya mabadiliko makubwa sana ya namna ya kuendesha mambo kutoka Bunge la analogia kwenda Bunge la digitali na mengine mengi ambayo umeyafanya. Utakumbuka Bunge hili la Kumi la Moja ulifanya uamuzi wa kijasiri hapa wa kuamua kuanzisha studio ya Bunge ambayo ni uamuzi ulifanywa na Bunge la Kumi, ukaamua sasa twende tutekeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni katika mambo matatu. La kwanza, nimeangalia kwenye randama ya Bunge,

nilidhani ni vizuri tukaitengea fedha studio ya Bunge ili ifanye kazi vizuri zaidi. Kwa sababu huyu ni mtoto wako, umemsimamia wewe ndani ya Bunge hili, tusipomtengea fedha ya kutosha bado mambo hayatakwenda sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tusimuache nyuma kwenye mabadiliko haya ya teknolojia unayoenda nayo na wao tuwape vifaa vya kisasa ili waweze kufanya kazi vizuri. Hii kazi umeisimamia wewe na mimi naamini wananchi wa Kongwa watakuchagua tena urudi uje ukamilishe kazi hii ulioifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la tatu kwenye studio ya Bunge, nimeona tumeanza kupitia Kanuni za Kudumu za Bunge, si vibaya tukazungumzia Kanuni ya kuendesha hii studio ya Bunge nayo ikawa sehemu ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili mambo yakaenda vizuri zaidi. Tupanue wigo ikiwezekana tukafanye *coverage* hata kwenye Kamati za Bunge na kwenye shughuli mbalimbali za Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na naipongeza Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya. Ni matumaini yangu Chama cha Mapinduzi kitasimama tena na Mheshimiwa Magufuli, ni matumaini yangu Watanzania watamchagua tena turudi kufanya kazi ambayo tulimpa mwaka 2015. Ameifanya vizuri kwa miaka mitano, tumuongezee miaka mingine mitano akamilishe kazi tuliyomtuma. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nape Moses Nnauye. Nimeshamtaja Mheshimiwa Peter Serukamba baada ya hapo Mheshimiwa Bulembo.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba nianze na yafuatayo. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya. Mimi nimepata bahati nimekaa Bungeni hapa muda mrefu kidogo, sijamuona Waziri Mkuu ambaye

imekuwa rahisi kwenda kumuona ukiwa na shida na alivyo na uwezo wa kusikiliza. Mungu amjalie sana kwa wema huu na kwa tabia hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana wewe. Kwa miaka hii mitano umetuongoza vyema sana. Wewe ni mnyenyeketu, Job Ndugai niliyemjua mwaka 2005 ndiyo Job Ndugai mpaka leo mwaka 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia na mimi nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano. Rais Magufuli alivyo chaguliwa moja ya mambo kama mnakumbuka alianza mwanzoni ilikuwa ni kubana matumizi, safari za nje, watu kunywa chai na kwenda kwenye semina mahotelini. Kwa kawaida watu wengine hawakuelewa, mimi sasa leo baada ya miaka mitano naona faida za kazi kubwa aliyofanya ya kubana matumizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, amesema Mheshimiwa Nape kuhusu umeme. Tuna vijiji 12,000, tunapofika Juni, 2020 tutakuwa tumeweka umeme katika vijiji 10,000. Maana yake ni nini kwenye uchumi mpana? Maana yake sasa watoto wetu wasoma vizuri mashulen, afya itawezekana lakini pia ndiyo *modernity*ya maisha kwamba tunatoka kwenye kipindi ambacho tulidhani ni mtu tajiri ndiye mwenye umeme, sasa Mheshimiwa Magufuli amefanya umeme ni *essential* kwa maisha ya binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia amefanya kazi kubwa kwenye barabara, alianza zamani. Naweza nikataja barabara nyingi sana lakini mimi itoshe kusema nampongeza sana kwa barabara ya Kigoma kwenda Nyakanazi. Watu wa Kigoma tunalo deni kwa Mheshimiwa Rais Magufuli. Inawezekana wengine hamjui thamani ya barabara ile, barabara ya Kigoma - Nyakanazi inaenda kutuunganisha watu wote wa Kigoma. Kwa hili, tunayo hakika tutatoa shukurani zetu mwezi Oktoba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia kwenye afya, kwa bahati nzuri nimikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo

ya Jamii, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge hakuna kipindi ambacho nchi hii imefanya kwenye afya kuliko miaka hii mitano ya Mheshimiwa Magufuli. Leo hii Hospitali yetu ya Muhimibili imeanza kutoa huduma ambazo huko nyuma zilikuwa lazima uende India, uende South Africa, uende Ulaya; Mheshimiwa Rais Magufuli amefanikiwa huduma hizo sasa zinapatikana hapa kwetu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kwenye maji, tumeanzisha *RUWASA*, Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami ndani ya miaka mitatu ijayo mtaona huduma za maji vijijini zitaongezeka sana kwa sababu ya *RUWASA*. Leo hii ukiangalia vijijini hata kwangu kule kuna miradi midogomidogo inasimamiwa na *RUWASA*, inafanya vizuri sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na Serikali kwa kazi kubwa waliyofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunaangalia uchumi mkubwa, ukiangalia *macro-economic stability* ya nchi nawapongeza sana watu wa Wizara ya Fedha, bado *inflation* imebakia chini kwenye *single digit*, wameweza ku- *control exchange rate*, wameweza ku- *control/uchumi* mkubwa ule na ndio maana leo sasa unaweza ukaona tunajenga barabara, madaraja na tunaweka maji; hii ni kwa sababu uchumi mkubwa umesimamiwa vizuri sana. Kwa hili naomba mnikubalie, ni ya kiupendeleo kidogo, lakini nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi kubwa. Nataka niwasaidie mwelewe na hilo ndio *standard* za Kigoma, kwa hiyo Mheshimiwa Magufuli alivyomchagua Mheshimiwa Mpango mnaweza mkaona *standard* za Kigoma, ndio hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo hii angalia kwa sababu ya uchumi kusimamiwa vizuri tunajenga meli Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika; ni kwa sababu ya kazi kubwa ya kusimamia uchumi mkubwa. Leo tunaanza kufanya kazi ya *infrastructure* ambayo ikiisha ninayo hakika Tanzania ya viwanda sasa itawezekana, leo hii Tanzania inawezekana kwenda *digital*/kwa sababu Tanzania tuna mkongo wa Taifa

kila Wilaya, kwa hiyo tunayo hakika Tanzania kama nchi tutakwenda *digital* muda sio mrefu sana. Kwa hiyo kazi yote hii imefanywa na Serikali ya Awamu ya tano kwa usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri na Serikali nzima, nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, natoka Kigoma kuna wavuvi; sasa nataka nimwombe rafiki yangu Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, kuna nyavu za *TBS* na kuna nyavu za Wizara, wale wavuvi tumewachanganya hawajui hii nyavu ni ya *TBS* ama hii nyavu ni ya Wizara. Niombe sasa waende wakatoe *clarification* ili watu wangu wa Mwamgongo, Kagunga na Ziwani waweze kupata hizo nyavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka niongelee suala la *corona*, ni janga kubwa lakini nimekuja na ushauri nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *Corona* ni jambo kubwa bayu, lakini tutafute *opportunity* na sisi kama nchi zinaezoendelea, nimesikia *African Union* wameanza *movement*, naombeni na sisi kama Tanzania tuwaombe wakubwa wanaotukopesha, *lenders* wote wasimamishe sisi kulipa madeni ili fedha ambazo tunalipa deni la Taifa zitumike kwenye athari za uchumi zinazoletwa na *corona*.

Mheshimiwa Spika, *corona* naiangalia kwa *side mbili*; moja ni suala la afya na utabibu, linasimamiwa vizuri sana; upande mwingine ambaao ni mbaya zaidi ni upande wa uchumi. Leo hii amesema hapa mtu dhahabu tunayo, hatuna pa kuuza kwa sababu wanunuzi hawawezi kuja. Leo hii tunalima, tutaanza kuvuna mazao yetu ya biashara, tutavuna lakini hatutakuwa na pa kuuza kwa sababu wanunuzi hawawezi kuja, hii ni hatari sana kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwaombe leo hii hoteli zinafungwa, migahawa inafungwa, hali ni mbaya ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie aongee na Benki ziwasaidie wafanyabiashara Watanzania hasa wale ambaao wamepata matatizo Benki zisimamishe *loan repayment* kwamba sasa hivi kwa mtu anayeta mizigo toka China, kwa mtu mwenye baa, hoteli, mtu mwenye hoteli,

transporter, watu wa mafuta, watu wa biashara za kwenda mfano mtu anayeuzza maua leo hana pa kuuza maua, lakini ana mkopo benki lazima aendelee kulipa, kwa hiyo ni wakati mgumu, niiombe Serikali iwaombe Benki angalau kwa miezi mitatu yasimamishe *loan repayment*, kwa sababu hapa tutapata tatizo jingine tutapata *corona* ya umaskini , tutapata matatizo makubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la kiafya, lakini tatizo linaloletwa na uchumi linakuwa kubwa sana, kwa hiyo niwaombe watu wa Benki watukubalie kwamba umefika wakati angalau na wao wapate hii *pinch* wasimamishe *loan repayment* kwa miezi mitatu tukiangalia hali inavyokwenda.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema tena, nakupongeze sana wewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu nampongeza sana kwa kazi kubwa ya kusimamia Serikali, tumeona kazi waliyofanya pia watuplekee pongezi zetu kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kizalendo, ya kimapinduzi na mtu anayeona mbali. Mheshimiwa Rais Magufuli anaona mbali na ndio maana ya kiongozi na nina hakika Watanzania watamchagua tena mwaka 2015 ili amalizie kipindi chake cha miaka mitano na nina hakika ataipeleka nchi yetu kwenye uchumi wa kat. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba kwa mchango wako mzuri. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kuendelea kupiga kura kokote kwenye ukumbi ambako mpo, nazidi kuzipata kura zetu, tunaendelea vizuri na wengine wako huku ndani hawajapiga kura bado. Kiongozi wa Upinzani bado hujapiga kura yako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Bulembo wewe ndio mchangiaji wa mwisho mchana wa leo.

MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza nichukue nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuweza kuniona kwenye wateule wake 10 kuja Bungeni kujifunza Bunge linaishije. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Makamu wa Rais nina imani walishirikiana na Mheshimiwa Rais kuweza kufanya uteuzi huu akiwemo na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi leo sina mengi sana nataka kusema machache kidogo. Kwanza ni pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano. Waziri Mkuu ni mfano wa Mawaziri wachache ambao watu walishaonekana. Kwanza ni mvumilivu, pili mstahimilivu, tatu Mheshimiwa Serukamba amesema kumuona ni rahisi lakini hata ukiwa unajadiliana naya huwezi kujua kama ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hajakilewa kile cheo, hakijambeba kama Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hali hiyo, nasema na mimi ni mmojawapo ninayeaga kwamba sitarudi Bungeni, sitegemei kugombea chochote, ni mstaafu kwa sababu nimeshiriki siasa zaidi ya miaka 30, sijawahi kufanya kazi kwenye ofisi yoyote ya Serikali, nimefanya ujasiriamali na siasa miaka 30. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 nilikuwa nagombe Ubunge na mtu alikuwa anaitwa Joseph Rwegasira, Waziri wa Mambo za Nchi za Nje, wengine walikuwa wananyonya, wengine walikuwa darasani hapa, ni wachache waliokuwepo. Kwa hiyo nina imani nimejifunza Bungeni kuna nini, watu wanafanya nini, sasa kipindi cha kung'atuka kimefika.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu nina imani Wanaruangwa watakupitisha bila kupingwa, lakini ikiwa amejitokeza yoyote kwa kukupinga kwa sababu mimi ni mstaafu, gari yangu nitakuwa nayo mpya, mafuta yapo, nitakuja kupiga kambi kwako nihakikishe unashinda na nina imani kwa ushindi wako matunda haya tunayoyaona kwa awamu ya tano si jukumu langu kusema huyo uliyenayo kwa

sababu Mheshimiwa Pombe Magufuli atakuwa Rais na wewe unaweza kuendelea kuwa Waziri Mkuu, nitakuombea dua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nihadie kwako, mimi tulikuwa tunafahamiana kidogo si sana, lakini umenilea sana hapa Bungeni na nimejifunza mambo mengi kwako kwamba hoja sio Uspika, busara ndio kitu muhimu sana. Umejawa na busara, umejawa na huruma, yako mambo makubwa sana yanafanyika Bungeni huku kama hujawahi kukaa Bungeni itakuwa hatari, kwa maana ukiwa Spika leo umekuja jana Bunge hili haliwezi kutawalika, lakini uzoefu wako wa kuwa Mbunge ukaja ukawa Spika na wewe dua yangu naihamishia kwako kwamba nina uhakika Wanakongwa watakupitisha bila kупingwa, lakini wasipokupitisha bila kупingwa ni siku 60 nitakaa 30 kwa Mheshimiwa Majaliwa, nitahamia 30 Kongwa kuhakikisha unashinda. Ahadi zangu mara nydingi hazikai chini, ziko moja kwa moja, lakini nina uhakika na ukiwa Spika basi uendelee kipindi kingine kuwa Spika ndani ya Bunge hili. Uspika ni busara tu, ni hekima, yaani mafanikio ya miaka mitano Mhimili huu umeshiriki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye lile alilosema Mheshimiwa Nape. Nilibahatika kidogo wakati wa kampeni kwenye kusimamia llani nilikuwa natembea na bwana mkubwa aliyekuwa anagombea akakabidhiwa kijiti, yalikuwa yanasesmwa yaliyo kwenye llani, lakini tukipata nafasi ya kukaa sehemu moja namuuliza mzee mbona umetwisha mzigo, haya yatawezekana? Ananiambia hivi nakuahidi tena ndani mwaka mmoja yatawezekana, kweli anasema yatawezekana lakini sasa wenzangu wa Upinzani mnajua wanasesma mwenye macho haambiwi tazama, reli tunajenga, meli tunajenga, maji yapo, barabara zipo, viwanda vinafanya kazi, nidhamu imerudi ndani ya ofisi zetu, nidhamu hii haikuja bure, ukipita kijijini unakuta mama yuko kwenye zahanati na chemli hakuna umeme anakesha pale kwa ajili ya kuhudumia wananchi. Hii hajji yenywewe, ni kwa sababu Mheshimiwa John Pombe amefanya kazi yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa niwaombe, wote tunalia *corona* hapa, mkakati ni nini? Mimi nakuja na mkakati wa *corona*, mkakati wa *corona* niwaombe wenzangu wa Vyama vyta Upinzani wamwache Mheshimiwa Magufuli apite bila kupingwa tusiwe na uchaguzi wa Rais, pamoja na Katiba inasema kwa nini, kwa vyovyyote vile nina uhakika Upinzani hawana Mgombea Urais, sasa kwa nini tutumie gharama kubwa kufanya uchaguzi wakati mshindi tunaye. Utekelezaji unaonekana, aliyoyafanya yako wazi, kipindi kile kidogo tulipata kutoka jasho alikuwa Lowassa ameenda upambe ule, sasa yuko huku? Sioni, kwa hiyo wavumilie, tusitumie hela nyingi ili zibaki tukasaidie *corona*, tugombee Wabunge na Madiwani. Kikubwa wakipata Wabunge wengi au wachache si wanaongeza pato, pato linatokana na Ubunge halitokani na Urais. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hawa ni rafiki zangu lakini katika hili tukubaliane tu kwamba Vyama vyote vyta Upinzani nani atamshinda Mheshimiwa Magufuli, yupo jamani?

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. ALHAJI ABADALLAH M. BULEMBO: Sasa kwa nini tupoteze pesa ambapo wanaenda kushindana na jiwe, haina sababu, tuje humu tuwekeane utaratibu Mheshimiwa Magufuli aapishwe, tufanye uchaguzi wa Wabunge na Madiwani ili tupate pesa za kuwashudumia wananchi wetu katika janga la *corona*. Uchaguzi ni gharama kubwa, Serikali inaumia, unapofanya uchaguzi wa Rais gharama yake inatisha.

Kwa hiyo, nasema haya kwa dhati, lakini kuna wenzangu wa Upinzani watachukia, lakini siku ya mwisho atakuwa ameshinda Mheshimiwa Magufuli kwa asilimia 85 au 90, sasa ni kwa nini tupoteze muda huo? Kwa hiyo nina imani tutaungana nao tu, tunaweza tukaleta hoja tukaungana nao humu ndani, Rais tukamuacha tukaenda Wabunge na Madiwani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na niseme kwamba nashukuru kwa ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge wote, Mawaziri nimepata marafiki, nimepata maadui humu, lakini ndio maisha yanavyokwenda. Naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bulembo kwa mchango wako mzuri. Niwakumbushe ndio maana ya mwamba, jabali, viswahili viko vingi, mtaita majina mpaka mtachoka, ukweli unabaki pale pale. Taarifa zote za CAG ambazo zimesomwa na Waheshimiwa Mawaziri humu ndani ya Bunge zimo tayari kwenye *tablet* yako Mheshimiwa Mbunge popote pale ulipo, kuna sanduku linaloitwa sanduku la nyaraka *e-pigeon*.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye sanduku la nyaraka hizi taarifa zote za CAG tayari ziko huko ndani, kwa hiyo mnaweza kuziangalia wakati wowote. Kama tulivyosema mkakati wetu ni kwamba zitashughulikiwa ndani ya Bunge hili, kwa hiyo Kamati ya PAC na LAAC na kadhalika mijipange na bahati nzuri sasa tunakutana mchana, mtatumia nyakati za asubuhi kukutana na kuhakikisha kwamba taarifa hii ya CAG inafanyiwa kazi ndani ya Mkutano huu na kukamilika.

Utaratibu wenu wa kuita watu lazima ubadilike kila kitu lazima kibadilike, mtandao zaidi, mkimwita mtu basi aje na kuna sababu ya kumwita, ile kuita watu tu ili mradi watokeze mbele yenu, lazima ibadilike. Kwa hiyo kaeni, angalieni utaratibu na mfumo ambao muupendekeze kwa Spika namna gani mnaweza ku-*operate*, kuhakikisha kwamba kazi yetu kama usimamizi kama Bunge inakamilika. Sasa niendelee kuwakumbusha kuendelea kupiga kura, tunaendelea kuzipata.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Makatibu Wakuu na watendaji wote katika Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu

kwa hotuba nzuri iliyosheheni mafanikio katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi niko katika Kamati ya *LAAC*, katika ziara nyingi tulizofanya kukagua utekelezaji wa miradi mikoani, nilijikita sana kuchunguza miradi ya ujenzi wa madarasa, zahanati, vituo vya afya, stendi za mabasi, masoko, miradi ya maji na umwagiliaji na kadhalika. Ninapongeza juhudhi kubwa inayofanywa na Serikali kutekeleza miradi hiyo kwa gharama nafuu na mahali pengine kwa kutumia mtindo wa *force account* na ushirikishaji wa wananchi.

Napenda kushauri mambo yafuatayo; kwanza mara kadhaa tumeshuhudia radi zikiharibu majengo, yakiwemo madarasa na hata kujeruhi na kuua walimu na wanafunzi. Nashauri suala la kuweka mitego ya radi katika *public buildings* zote ziklwemo nyumba za ibada hasa katika maeneo yenye radi liwe la lazima ili kuokoa maisha ya watu na fedha za umma.

Pili, baadhi ya majengo yanalamikiwa kwa kujengwa chini ya kiwango. Naishauri Serikali iajiri wahandisi wachache na mafundi sanifu wengi katika Halmashauri zetu ili wazisaidie Kamati za Ujenzi kudhibiti ubora wa kazi katika majengo ya umma. Hali ilivyo sasa ni uchache mkubwa wa wataalamu hasa katika Halmashauri na *TARURA*. Bado kuna udhaifu mkubwa katika kusimamia ubora wa kazi na usimamizi wa mikataba ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, tatu, mafuriko yanayoendelea sasa kuharibu miundombinu yetu tuyatumie kama changamoto. *Trend and periodicity* ya miaka mingi ya ukame na mafuriko inaonesha kwamba kila baada ya miaka takribani minne huwa nchi yetu inapata ukame na upungufu wa chakula. Tutumie fursa hii sasa kuyavuna maji yanayopotea na kuyahifadhi katika mabwawa ili baadaye tuyatumie kwa kilimo cha umwagiliaji na matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa ni kwamba tunatumia fedha nyingi sana kukarabati miundombinu

iliyoharibiwa na mafuriko huku tukiyachia maji hayo hayo kutiririka hadi baharini bila kutunufaisha.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunakumbuka jambo hili tunapopata ukame, njaa na upungufu wa chakula. Mifano hai ni mafuriko ya *El-nino* yaliyotokea katika miaka ya 1990 na njaa ya mwaka 1974. Rejea pia Azimio la Moshi la Kilimo cha Umwagiliaji, Kilimo cha Kufa na Kupona na maazimio mengine yaliyohusu kupambana na ukame. Naunga mkono hoja.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi kwenye bajeti hii ya mwisho kwa kipindi hiki cha Bunge la Kumi na Moja la Awamu hii ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli. Pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa juhudzi zake katika kuongoza Taifa letu kwa kushirikiana na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba nzuri ya bajeti ya 2020/2021 ambayo imegusa kila eneo na kuelekea mafanikio yalipatika nchi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudzi ambazo inazifanya katika kutoa elimu na kupambana na virusi vya *Corona* ambavyo ni tishio kwa nchi yetu na dunia kwa ujumla. Pamoja na juhudzi hizo je, ni kwa kiwango gani nchi yetu tumeweka mpango wa elimu, vifaa tiba kwa maeneo ya pembezoni na maeneo ambayo yana mkusanyiko wa watu wengi?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekumbwa na mafuriko maeneo mbalimbali ambapo kumepelekea uharibifu wa miundombinu ya barabara, nyumbani na maeneo mbalimbali ya majengo ya huduma kwa jamii, mifugo pamoja na mazao na mashamba. Kwa kuwa jambo hili la mafuriko limekuja kidharura na mvua bado zinaendelea

kunyesha, je, Serikali imejipangaje kurudisha hali ya miundombinu ya barabara kwa haraka ili kuleta urahisi wa mawasiliano kwa jamii?

Mheshimiwa Spika, miradi mingi imekumbwa na kadhia hiyo hivyo kuna uwezekano wa miradi mingi kuchelewa kukamilika kwa wakati mfano mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Nyerere ambao uko Rufiji ambako barabara imeharibika na safari ya kupeleka vifaa kuchelewa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa fedha kwa *TANROADS* na *TARURA* ili kuboresha miundombinu ya barabara?

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mkuu katika suala la mafuriko alilisimamia vyema kwa kufika maeneo mbalimbali yaliyopata kadhia hiyo na kuwafariji na kutoa misaada. Pamoja na hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera kwa usimamizi wa llani na utekelzaji wake kama ulivyoeleza kwenye hotuba yako kwa "mmeahidi na mmetekeleza." Miradi mbalimbali ilioanzishwa imeweza kuongeza kipato cha uendeshaji maisha kwani tumetoa ajira hasa kwa vijana na kuweza kukuza uchumi wetu. Pia kutoa mafunzo mbalimbali kwa vijana ambayo yanawasaidia kuijidesha.

Mheshimiwa Spika, kuna kundi la vijana ambao waliathirika kwa kutumia madawa ya kulevyia na Serikali imefanya juhudini kubwa ya kuhakikisha wanaacha na wengi wanaingia kwenye mfumo wa kutumia dawa ambazo zimewawezesha kurudi kwenye hali yao ya kawaida. Ni vyema Serikali ikawawekea utaratibu wa kuwapa mafunzo ya ujasiriamali. Mfano mzuri wa vijana kama hao ni Kituo cha Kutolea Dawa Kilichopo Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza Bunge Mtandao limeanza kwa wakati muafaka kwani kutokana na tatizo hili la *Corona* sijui Bunge letu lingeendeshwaje. Pongezi kwako na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mkuu na Waziri kwa kazi nzuri ya kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza huduma za afya kwa nchi nzima hii hatua nzuri kwa wananchi kupata huduma kwa urahisi. Ujenzi wa Hospitali kwa Halmashauri 67 katika Halmashauri mpya. Halmashauri ya Mufindi Hospitali imejengwa na itanisaidia sana katika majimbo ya Mufindi Kusini na Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa sekondari ya Mbalamaziwa, Mgololo na Idete, wanafunzi wameanza kusoma katika sekondari ya Idete, nashukuru sana Serikali kwa kukamilisha ujenzi huo.

Kuhusu umeme vijijini kata 15 umeme umeshafika bado kata moja tu ya Idunda, naomba Serikali kupeleka umeme katika kata ya Idunda.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo kubwa sana katika Kata ya Mtwango, Igowole, Nyololo na kata ya Itandula na Mtambula bado hatujapata maji ya bomba. Naomba sana Serikali kukamilisha miradi ya maji katika kata hizo.

Mheshimiwa Spika, barabara ni tatizo kubwa, barabara ya Mafinga hadi Mgololo bado ujenzi wa kiwango cha Lami. Kuna barabara ya Nyololo, Kasanga, Luhunga na Kilolo barabara hizi ni mbovu sana. Naiomba sana Serikali kujenga barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pongezi kwa Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Raisi wetu mpPENDWA Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha Watanzania wanaishi kwa amani na utulivu na

kuendelea kusimamia kutekeleza llani ya CCM kuwaleta wananchi maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayofanya pamoja na hotuba nzuri iliyojaa matumaini ya kufikia malengo yetu ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza kwa kazi nzuri na weledi wa hali ya juu kuhakikisha vikao vya Bunge la Bajeti vinaendelea kwa kuchukua tahadhari zote zinazotakiwa katika kujikinga na ugonjwa wa mapafu ujulikanao "Covid-19". Nakupongeza pia kwa jinsi ulivyoendelea kuimarisha matumizi ya Bunge Mtando ambao umeendelea kurahisisha vikao, lakini pia kupunguza gharama kubwa hasa ya kuchapisha marejeo mbalimbali.

Baada ya pongezi hizo naomba sasa kuchangia kwa kutoa ushauri kuhusu Mfuko wa UKIMWI (*ATF*).

Mheshimiwa Spika, bajeti ya UKIMWI inategemea kwa zaidi ya asilimia 90 fedha kutoka kwa wafadhili wa nje. Lakini tumeshuhudia wafadhili hawa wameanza kutuwekea masharti ambayo hayaendani na utamaduni wetu na kutishia kuondoa ufadhili kwenye suala la UKIMWI. Lakini pia tunashuhudia nchi zote duniani sasa zikiyumba kiuchumi kutokana na shughuli nydingi za kiuchumi kusimama kutokana na ugonjwa huu wa corona. Kwa mantiki hii, tunategemea kuona wafadhili wakijitoa katika kufadhili miradi mingi ya maendeleo ikiwemo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, UKIMWI bado ni tatizo na janga la kitaifa na dunia. Hivyo basi, naungana na wote walioshauri Serikali kuwa ni wakati muafaka sasa kama nchi kuchukua tahadhari mapema kwa kutafuta tozo maalum kwa ajili ya mfuko huu wa UKIMWI. Asilimia 4.7 ya maambukizi kitaifa bado ni kubwa na tishio, hivyo tutoe kipaumbele kwa mfuko huu kuhakikisha tunapata chanzo endelevu cha fedha kwa ajili ya *ATF*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya ya kutuletea maendeleo. Tumeona kwa macho miradi mikubwa inayotekelawa. Lakini pia nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa utendaji wako uliotukuka na kwa hotuba nzuri ya bajeti ya ofisi yako. Baada ya pongezi hizo sasa nianze kuchangia kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la afya. Napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kutuletea fedha kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya Mapera. Wananchi wa Tarafa ya Hagati wamenituma salamu zao za pongezi kwa Serikali ya awamu ya tano.

Hata hivyo tunaomba walau tungepata tena shilingi milioni 500 kwa ajili ya upanuzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Matiri ambayo ina wakazi wengi. Ombi letu lingine ni kuhusu gari ya dharura ya wagonjwa kwa maana ya *ambulance*. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TARURA*, tumeshuhudia mvua nyngi sana katika msimu huu. Mvua hizi zimeharibu miundombinu ya barabara kwa kiwango kikubwa sana. Ushauri wangu ni kuwa Serikali ifanye upembuzi wa kina kila Wilaya ili kubani ukubwa wa tatizo. Baada ya zoezi hilo katika bajeti hii litengwe fungu maalumu kwa ajili ya kurekebisha miundombinu iliyoharibiwa na mvua hizo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa pili katika eneo hili ni kuwa bajeti ya *TARURA* ipande kufikia walau asilimia 70.

Kuhusu Mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemvu, ushauri wangu katika eneo hili ni kwamba Serikali ione

umuhimu wa kuweka ukomo wa kipindi cha kuchangia *inside indefinitely*. Kwani zipo Halmashauri zenyе makusanyo makubwa sana ya ndani. Hivyo kama michango hiyo haitawekewa ukomo wa miaka ya kuchangia basi fedha hizo zitakuwa ni nyingi na pengine kupelekea matumizi mabaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu Jimbo la Nkasi Kusini lina Tarafa moja ya Wampembe yenye kata nne, mawasiliano ya barabara ni magumu yaani hakuna kabisa barabara, kwa hiyo kuna shule za msingi zipatazo kumi shule hizi zina hali mbaya na hazitembelewi na wataalam wa ubora wa elimu hawafiki huko zaidi nafika Mbunge na wakati mwiningine Mheshimiwa *DC*.

Kwa hiyo, shule hazijatembelewa miaka yote mitano ni Mbunge nimekuwa nikiwatembelea, ofisi za walimu ni chini ya mti. Shule hizo ni Lupata, Mkiringa, Mlalambo, Lusembwa, Itanga, Tundu, Lolesha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili; bajeti ya mwaka jana ilionesha kuna mipango ya kununua meli mpya katika Ziwa Tanganyika na kuwa meli ya Liemba itakarabatiwa, lakini katika bajeti hii hajianipa matumaini na tulishawaambia wananchi. Leo hakuna fedha wala mwendelezo wa mipango iliyosemwa katika bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanasumbuliwa sana na zaidi wanachanganywa na wataalam wa Wizara husika wanaambwiwa nunuweni nyavu size fulani wakinunua kwa maelekezo yao wanasema nyavu hazifai na zinachomwa, wananchi wanapata hasara. Tuelezeni kwa nini mnafanya hivyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu lione jimbo hili.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuungana na Wabunge wenzangu waliopata fursa ya kuchangia hoja iliyoko mezani ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa na nzuri iliyo fanyika hadi sasa katika kuliendeleza Taifa letu kijamii na kiuchumi. Kwa hakika chini ya uongozi madhubuti wa Rais wetu mpandwa, Dkt. John Pombe Maguful na Serikali yake yote ikiweko Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara zilizoko chini yake imefanyika kazi iliyotukuka ya kuijenga nchi yetu na kila sekta ni shahidi wa miradi ya kimkakati iliyotekelizwa (afya, ardhi, elimu, habari, kilimo, maji, maliasili, mawasiliano, mifugo, uvuvi, nishati, ustawi wa jamii na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, naomba nichangie hoja moja inayohusu suala la kazi na ajira.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa katika Halmashauri zetu za ukaimishaji wa watendaji wa nafasi mbalimbali za ajira kwa muda mrefu suala ambalo linadhoofisha utekelezaji wa majukumu na upitishaji maamuzi kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido karibu asilimia 50 ya Watendaji wa Vijiji ni watumishi wanaokaimu nafasi hizo tena wengi ni kwa miaka mingi hadi sasa.

Naiomba Serikali kuanzia bajeti hii ihakikishe kuwa nafasi za ajira zinawekewa ukomo wa kukaimu na Serikali itoe pesa za kuajiri na vibali vya kuajiri kwa wakati kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kwenye Hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hotuba ya Waziri Mkuu imeangazia kwenye ukurasa wa nane kuhusu hofu inayoendelea kutanda duniani kufuatia kuenea kwa homa kali ya mapafu inayoletwa na virusi vya Korona (COVID 19).

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali iwaagize viongozi wote wa ngazi zote katika vijiji vyetu, Kata, Tarafa,

Wilaya na Mikoa isambaze habari ya kuwaelekeza na kuziagiza kaya zote zenyet watu wao wanaoishi au kufanya kazi nchi za jirani ambazo nazozimeshaingiliwa na janga hili la virusi vya Korona, watu hao wabakie huko huko hadi janga hili lidhibitiwe na wasijaribu kurudi bila kupitia mipaka rasmi (*border posts*) wapimwe kabla ya kuruhusiwa kwenda makwao.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu kubwa ni kwa wale wanaoweza kuamua kurudi nyumbani kwa kupitia njia zisizokuwa rasmi (njia za panya) na kuvuka mipaka na kwenda hadi manyumbani kwao bila kupimwa na ikitokea akaja mtu ambaye ameathirika; atakuja kuambukiza jamii yetu nzima ambayo kama mjuavyo hatuna miundombinu toshelevu na rasilimali za kupambana na gonjwa hili ambalo bado halina dawa wala chanjo.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali iwekeze katika kuweka vifaa vya kupima na kuzuia maambukizi mapya katika vituo vyetu vyote vya kutolea huduma za afya nchini zikiwemo zahanati, vituo vya afya na hospitali zetu za Wilaya na Mikoa ili kuepuka uwezekano wa kutokea kwa mlipuko wa gonjwa hili kama ilivyotokea kwa wenzetu wa mataifa kama China, Italy, Spain na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kupongeza juhudzi zinazoendelea kufanywa na viongozi wetu wa ngazi za Taifa tukiongozwa na Rais wetu mpandwa Dkt. John Joseph Magufuli, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa na viongozi wetu wa Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata na hata Vijiji katika kuhakikisha kuwa tunafanya kila liwezekanalo kuzuia kuenea kwa homa hii mbaya ya Corona.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudzi hizi nawasihi Watanzania wenzangu tuendelee kumlilia Mwenyenzi Mungu atuondolee janga hili.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nashukuru kwa kupokea mchango wangu wa maandishi na ninaunga mkono hoja.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri lakini nitoe maoni juu ya maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, afya; madaktari bado ni changamoto mfano Wilaya ya Handeni ambayo ina madaktari watano tu ikiwa na upungufu wa madaktari 24 na ukizingatia haihudumii Handeni peke yake bali Wilaya jirani kama Kilindi na Manyara.

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa Wilaya hii kama sikosei unaweza kuwa inalingana na Mkoa wa Kilimanjaro, hivyo utaona ni kiasi gani watu hawa wanataabika. Hivyo niiombe Serikali itusaidie juu ya tatizo hili ambalo limekua ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, elimu; tatizo la uchache wa madarasa linalopelekea mrundikano wa wanafunzi katika madarasa. Serikali imeleta elimu bure na kuhamasisha wazazi wengi kupeleka watoto hivyo ili lile lengo la awali litimie tunaomba nyongeza ya madarasa na shule ili kupunguza umbali wa kufuata elimu unaopelekea watoto wetu wa kike kukatishwa masomo kutokana na mimba za uttoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maji limekua ni mtihani mkubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Handeni. Kuna mradi ambaao umechukua muda mrefu sana wa *HTM*. Tunaomba kujua tatizo ni nini? Athari za ukosefu wa maji Handeni ni kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, viwanda;- tuna uhitaji mkubwa sana wa kiwanda cha matunda. Wale wote wanaopita njia ya Segera - Korogwe na hata kuelekea Tanga Mjini mtaona ni jinsi gani Mkoa wetu umejaaliwa kwa matunda ya kila aina. Lakini cha kusikitisha matunda haya yanatuzidi nguvu, ni mengi kuliko matumizi yanaoza. Hivyo niombe serikali tuangalie juu ya hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa kuweza kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha kwa makini na kwa ufasaha mkubwa hotuba hii iliyojaa matumaini makubwa kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu huduma za jamii; napenda kuchukua fursa hii kuipongeza kwa dhati Serikali yetu ya awamu tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais John Joseph Magufuli kwa kusimamia vizuri pamoja na mambo mengine kuwa na uendelezaji wa huduma za jamii nchini. Kitendo cha kuweka elimu bila ya ada ni kitendo chema na kinapaswa kupongezwa na jamii yote ya Tanzania. Elimu ndio ufunguo wa maisha, mtu kukosa elimu sio jambo sahihi. Tunaipongeza Serikali yetu kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba Serikali ifuatilie na ielimishe wananchi hasa wa kijijini juu ya kuweka fursa hii. Inawezekana fursa hii ikatumika kwa watu wanaoishi mijini tu na kukosekana kuwafaidisha wananchi wa vijijini kutokana na kutokuwa na fursa hii.

Pili ni *TASAF*, miuongoni mwa mipango bora ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na kupunguza umaskini ambazo Serikali yetu imeendelea kufanya ni kupertia mpango huu wa *TASAF*. Mpango huu ni miuongoni mwa mikakati inayopaswa kuendelezwa kwa nguvu zote. Mpango huu umesaidia sana wananchi hasa wale wa kaya maskini, umewainua kiuchumi, kufikra na umewaendeleza katika juhudzi zao za kujitafutia kipato.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa kwa umakini kwa hali ya juu na

Mheshimiwa Rais wetu mpendwa. Ushauri wangu katika jambo hili kwa watendaji kama alivyoagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa waaminifu katika kutekeleza jambo hili. Bado kuna manung'uniko katika upembuzi usiokuwa sahihi wa kaya husika. Bado kuna kaya ambazo hazina sifa ya kupata fursa hii na zinaachwa zile ambazo zinastaahiki kupata fursa hii.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kilimo; kilimo ni uti wa maisha na maendeleo ya nchi. Serikali yetu inaendelea na juhudzi za kusimamia kwa ukamilifu kilimo ili kuona tumefikia katika malengo tuliojijiwekea. Miongoni mwa mambo ambayo Serikali inayasimamia ni pembejeo na zana za kilimo. Bila ya pembejeo na zana za kilimo hakuna uwezekano wa kupata mafanikio ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nashauri sana Serikali kwa kuiwezesha, kuisimamia na kujielekeza Benki ya Kilimo ya *TADB* kuhusu kuwakopesha wakulima wetu wa chini, lakini bado gharama za matrekta ni kubwa sana. Kikundi cha wakulima ambaao nimejjipanga kuendeleza kilimo kuwapa mkopo wa shilingi milioni 78, ni kitendo ambacho kinatakiwa kuangaliwa, si rahisi kuweza kumudu kurejesha mkopo wa aina hii kwa wakati. Ushauri wangu katika hili *TADB* iendelee kutafuta namna nzuri zaidi ya kuweza kuwapunguzia wakulima bei ya trekta ili waweze kumudu kwa wingi kukopa matrekta hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa John Magufuli kwa kazi kubwa sana inayofanya katika kuwaleta wananchi maendeleo na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi mzuri wa Wizara hii pamoja na wasaidizi wake. Naipongeza Serikali kwa ujenzi na kuimarisha

miundombinu, uboreshaji wa huruma za afya na elimu ikiwemo kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itenye fedha za kutosha ili kuwezesha kukabiliana na majanga na maafa yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, mengine nakubaliana na mipango ya Serikali. Nashauri kupunguza kodi kwa vifaa vya kujikinga na maradhi. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii ya kipekee kabisa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha na mimi kuwepo mahali hapa na kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu 2020/2021 iliyopo mbele yetu. Hotuba hii inakwenda kutekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM kama ilivyoainishwa. Napenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na watalaan mbalimbali kwa kuandaa hotuba nzuri itakayokwenda kuleta mapinduzi makubwa katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kwa kuanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu, sisi sote ni mashahidi, tumeona Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa katika maeneo mbalimbali kuhakikisha shughuli mbalimbali za kimaendeleo zinakwenda vizuri bila kusuasua, tumeshuhudia usimamiaji mzuri wa llani ya Uchaguzi ya mwaka 2015/2020 ukifanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni hatua nzuri na ya kujivunia sana tukiwa sisi wanaCCM, kwani tuliahidi kuwaletea maendeleo wananchi wetu bila kubagua.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu, huduma za kiuchumi na kijamii, utawala bora, mapambano dhidi ya

rushwa na ufisadi pamoja na kuhamasisha uwekezaji nchini kwetu, kuvutia wawekezaji mbalimbali kuja kuwekeza na kuzalisha ajira.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa awamu ya tano kwa uongozi wake mzuri na kuhakikisha utekelezaji wa llani ya CCM 2015/2020 unakwenda vizuri. Aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kupambana na janga la virusi vya corona (COVID-19), ikumbukwe janga hili ni la kimataifa kama WHO walivyokwishatangaza hapo awali. Janga hili linaendelea kusumbua na kuathiri watu wetu, idadi ya wagonjwa imekua ikiongezeka na hivi karibuni imethibitishwa kuwa mgonjwa mmoja aliyekuwa na virusi hivi na kulazwa katika *treatment centre* iliyopo karibu na Hospitali ya Mloganzila amefariki dunia. Ni kipindi kigumu sana tunachopititia kulingana na mazingira yetu, lakini ni wajibu wetu kuendelea kushirikiana na kutoa elimu kwa watu wetu juu ya kujikinga na kuchukua tahadhali mbalimbali juu ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, hakika katika kipindi hiki cha janga hili la virusi vya corona (COVID-19) ni vema Serikali ikaangalia ni njia gani ya kukabiliana na janga hili hasa namna ya kuepusha maambukizi mapya kwa wananchi, mazingira yetu yanatofautiana sana na nchi za wenzetu hivyo hatupaswi kuyafanya yale ambayo wenzetu wameyafanya kulingana na mazingira yao, naishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha ili kukabiliana na janga hili, hii itasaidia kuweza kukabiliana na aina yoyote itakayojitekeza katika kipindi hiki hatarishi, kwani Tanzania ni moja ya nchi ambazo zina muingiliano mkubwa wa watu, mikusanyiko masokoni bado inaendelea, katika vyombo vyetu vya usafiri bado kuna mrundikano wa watu na baadhi ya maeneo mengine watu wameendelea kukusanyika, maradhi haya hatuvezi yapuuzia, kuwalinda watu wetu ni wajibu wetu. Hata hivyo naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ilizochukua baada ya janga hili kutokea, kusitisha mbio za mwenge wa uhuru, kusitisha michezo yote nchini, kusitisha shughuli zote za elimu kuanzia elimu ya awali hadi vyuo vikuu,

kusitisha semina, makongamano na mikutano yote ya hadhara, ni maamuzi ya msingi kulingana na aina ya ugonjwa unavyoambukiza.

Naiomba Serikali iendelee kutoa elimu kila wakati katika vyombo vyote vya habari, kuweka matangazo mbalimbali mitaani ili wananchi wapate kujua namna ya kujikinga na janga hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujitahidi kutengeneza fursa mbalimbali za ajira kwa kuendelea kuweka mifumo mizuri ya uwekezaji hasa katika viwanda, ni jambo jema na la kupongezwa, lakini bado tuna changamoto kubwa sana ya ajira kwa vijana wetu, kwa taarifa ya Shirika la Kazi Duniani ya mwelekeo wa ajira kwa vijana ulimwenguni (*Global Employment Trend for Youth*) inaonesha kuwa tatizo la ajira kwa vijana Tanzania wenye elimu kuanzia sekondari na kuendelea ni kubwa kuliko wale wenye elimu ya kiwango cha chini. Aidha, Watanzania wenye elimu za chini wamepata ajira lakini ajira zao ni duni ama kipato cha chini na za mazingira hatarishi kama sehemu mojawapo ya kuwatumikisha kwa kuwa uelewa wao juu ya masuala ya sheria na taratibu za kazi ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubali kuwa kilichotufikisha hapa ni aina ya elimu tunayoipata kutoka mashulenii. Hatua ya kwanza ya kulitatua tatizo hili ni kugusa mitaala yetu kwanza, bado ipo kikoloni ndio maana kila kijana anawaza kuajiriwa zaidi kuliko kujajiri na hili sio kosa lao, yaani hakuna kitu tunachokiogopa kama mitaala yetu ya elimu kubadilisha ili iendane na mazingira yetu ya sasa ili itusaidie kukabiliana na hili tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunajifunza mambo mengi shuleni ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na mazingira yetu. Niliwahi kusema kuwa kwa nini mfano tusikubali kuingiza masomo ya ufundi kwenye shule zetu zote za sekondari kutegemeana na mazingira shule ilipo? Cha kushangaza hata zile shule zinazotoa fani za ufundi kwa sasa zipo taabani, hata tukienda kwenye shule hizo tukafulize

wangapi wanasomea masomo hayo ya ufundi tutakuta hakuna. Tabaka hili la ukosefu wa ajira kwa vijana ni kubwa sana na kila mwaka idadi inazidi kuongezeka, hii ni nguvu kazi kubwa ambayo ni wajibu wa Serikali kuiwekea mipango mizuri ya ajira ili iweze kuzalisha, vijana kukosa ajira kuna athari zake kubwa.

Naiomba Serikali ije na mpango mzuri zaidi wa kuwasaidia vijana wetu katika kujiajiri na kuajiriwa, Serikali iweze kuajiri vijana wenyewe uwezo na kuwatengenezea fursa vijana wengine katika ajira binafsi hasa katika kilimo, nchi yetu ina ardhii kubwa sana hivyo tukiwekeza hasa kwenye kilimo kwa vijana wetu tutapata faida kubwa, kwanza ajira yenye kwa vijana, kuingiza kipato na Serikali kupata kodi ya mazao, uzalishaji wa chakula utaongezeka na kupelekeea Taifa kuwa na chakula cha kutosha. Lakini tukiendelea kusema vijana wajiajiri na hatujawahi kujiliza wanajiajirije? Hiyo mikopo wanaipataje? Sote tunajua masharti magumu ya benki zetu hapa nchini, benki hawatoi fedha bila kuwa na *asset* ya kuweka kama *bond*, hawa vijana wana *asset* gani? Ni kijana yupi mwenye hati ya nyumba au kiwanja au chochote anachowenza kukiweka kama *bond* ili apate mkopo?

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zote nilizotangulia kuzisema na kushauri, lakini naipongeza tena Serikali kwa kuweza kutambua umuhimu wa kundi hili la vijana, kama fursa muhimu na kwa maendeleo ya Taifa, naipongeza Serikali kwa kuendelea na uboreshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Katika mwaka 2019/2020 Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.2 ambapo vikundi 586 vyenye jumla ya vijana 4,222 kutoka katika Halmashauri 155 walipata mikopo hiyo. Hata hivyo naishauri Serikali kuwaendeleza wabunifu mbalimbali katika vifaa mbalimbali walivyobuni ili viweze kulisaidia Taifa letu, na sisi tuwe na vifaa vilivyobuniwa hapa kwetu, hili pia litasaidia kuongeza chachu kwa vijana wetu kuwa wabunifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto pia inayowakibili wenzetu wenye matatizo ya ulemavu, hawa wanapaswa kuendelezwa kulingana na matatizo waliyokuwa nayo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha watu wenye ulemavu wanaendelezwa katika fani mbalimbali ili waweze kujiajiri na si kuwaona baadhi wakiwatumia huko mitaani kuomba omba misaada, hii haileti taswira nzuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua uwekezaji ni njia pekee inayoleta maendeleo na kuzalisha ajira, tukiwa na wawekezaji wengi hasa katika sekta ya viwanda wataleta tija kubwa na faida kwa wananchi, ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi. Hata hivyo naipongeza Serikali kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za kuhamasisha na kufanikisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuvutia mitaji, teknolojia na ujuzi ambaao ni chachu ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

Aidha, tumeambiwa Serikali yetu imeendelea kufanya tafiti za kisekta (*investment sectoral profiles*) ili kubaini hali halisi ya ukuaji, mnyororo wa thamani, fursa zilizopo na changamoto za kisekta kwa lengo la kutoa mapendekezo ya maboresho katika sekta husika, hii itasaidia sana katika kurekebisha baadhi ya maeneo yenye changamoto. Katika hatua za awali tumeona tafiti hizo zimefanyika katika maeneo ya mbolea na kemikali, mifugo na mazao yake, pamba, uchakataji wa mazao ya kilimo kama vile korosho, michikichi na parachichi, nafaka na mbegu za mafuta. Halikadhalika matokeo ya tafiti hizo yameendelea kutumika katika kunadi fursa mbalimbali za uwekezaji ndani na nje ya nchi na kuishauri Serikali kuhusu mikakati na maboresho yanayohitajika katika kuvutia uwekezaji kwenye sekta husika, mwenendo huu ni mzuri na wenye kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuandaa mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia sera na miongozo ikiwa ni pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021. Mpango huu ni

wa mwisho katika mfululizo wa mipango ya kila mwaka wa kutekeleza Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) wenye dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochaea mageuzi ya uchumi na maendeleo ya watu wetu. Ni hatua nzuri na ya kuungwa mkono.

Aidha, naipongeza Serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, Serikali imetuambia Mahakama imeendelea kuimarisha huduma kwa kuweka mifumo na taratibu mbalimbali za kuwafikia wananchi katika maeneo yote nchini ili kupunguza mrundikano wa mashauri na kuhakikisha mashauri hayo yanamalizika kwa wakati. Mojawapo ya utaratibu unaotumika ambao ni mzuri na umeleta tija ni kuwatumia Mahakimu wenye mamlaka ya ziada (*extended jurisdiction*) kusikiliza mashauri ya Mahakama Kuu, ni utaratibu mzuri wenye kufanya sasa Mahakama zetu kutokuwa na mrundikano wa mashauri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali za kujenga uchumi wa viwanda, napenda kuipongeza Serikali kwa kuwezesha jumla ya viwanda vipyta zaidi ya 4,000 vimejengwa katika mikoa mbalimbali. Viwanda vilivyojengwa vinazalisha bidhaa za ujenzi, pamoja na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ikiwemo nafaka, matunda, mafuta ya kupikia na bidhaa za ngozi. Ujenzi huu wa viwanda vipyta nchini, umechangia kupatikana kwa ajira mpya 482,601 nchi nzima, ni vyema sasa tukaongeza juhudii zaidi ili viwanda viongezeke, wananchi wetu wapate ajira kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri Mkuu ni hotuba kiongozi kwa Wizara zote Serikalini, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefafanua kwa upana juu ya vipaumbele vya Serikali ya awamu ya tano ikiwemo masuala ya elimu, afya, miundombinu ya mawasiliano na uchukuzi, kilimo, ujenzi, bandari, reli ya kisasa, ununuzi wa ndege mpya, ujenzi wa viwanja vya ndege, kilimo na mifugo,

maji, ujenzi wa bomba la mafuta kutoka nchini Uganda kwenda Tanga, ununuzi wa meli mpya na vivuko, ujenzi wa madaraja makubwa nchini, umeme na ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme wa maji wa *Mwalimu Nyerere Hydropower Station* pamoja na uzalishaji wa umeme kutoka katika vyanzo vingine kama vile gesi, makaa ya mawe, umeme juu na joto ardhi. Miradi hii itasaidia kuliwezesha Shirika la Umeme nchini *TANESCO* na Wakala wa Umeme Vijiji (REA) kusambaza umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya tano imeleta mapinduzi makubwa katika kupeleka Tanzania kuwa nchi ya viwanda, huu ni mwanzo mzuri katika kulijenga Taifa letu.

Kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa ya *Standard Gauge (SGR)* huu ni ukombozi katika kuhakikisha kwamba barabara zetu za lami na changarawe ziweze kudumu kwa muda mrefu na kuokoa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ya awamu ya tano imefanya kazi kubwa sana katika kuleta mageuzi makubwa ya uchumi nchini ambapo tumeshuhudia mapambano dhidi ya madawa ya kulevyo, masuala la mapambano dhidi ya rushwa yameimarishwa ambapo fedha nydingi zimeokolewa. Pia Serikali yetu imeimarisha ukusanyaji wa mapato ya kodi, tunaipongeza sana Serikali yetu ya awamu tano kwa kuimarishe makusanyo ya mapato, niombe Serikali iendelee kuimarishe na kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kufunguliwa kwa shirika letu la ndege la *ATCL* ni jambo kubwa na la kujivunia, ndege mpya zimenunuliwa na hivyo kuinua sekta ya utalii nchini na kuleta fedha za kigeni nchini na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vyatengenezo na usalama vinachangia pakubwa katika kuhakikisha utulivu na usalama wa nchi, hivyo nashauri Serikali ivipatie vitendea kazi vyatengenezo ili kufanya vyombo vyatengenezo viende na wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia Tanzania ya viwanda nashauri fedha zinazotengwa katika bajeti zipelekwe kwa wakati ili kuharakisha miradi iliyopangwa itekelezwe ipasavyo.

Nashauri kwa wamiliki wa viwanda vinavyotumia sukari ya viwandani walipwe kwa wakati fedha zao ambazo wanadai sasa takriban miaka minne hawajalipwa asilimia 15 *withholding tax* ambayo inapelekea wamiliki wa viwanda kupunguza uzalishaji pamoja na kupunguza wafanyakazi sababu mitaji yao imeshikiliwa na Serikali. nashauri walipwe illi uzalishaji uongezeka na kupata pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, nashauri askari wa usalama barabarani wasiwabambikizie makosa madereva, watumie weledi wao kubaini makosa mbalimbali, maana utakuta trafiki anatumia kifaa cha kumulikia *speed* maarufu tochi, badala ya kupiga picha namba ya gari wanapiga picha bodi ya gari na kutumia picha hiyo kukamata magari yote ya kampuni husika maana jina na rangi za magari zinafanana. Hivyo nashauri askari wapatiwe mafunzo ya kutosha kuondoa kero.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii na mimi kutoa mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo:-

Kwanza nianze na maradhi ya Corona. Ili kudhibiti ugonjwa huu mambo yafuatayo yazingatiwe:-

Mosi, kama Serikali imeamua shughuli za kijamii waendelee kama masoko, maeneo ya usafiri wa umma na kadhalika, wakati umefika sasa nikuzuia watu kutoka nje ya nchi, pia maeneo yaliyopatikana maambukizi yazuiliwe watu kutoka na pia kuingia.

Jambo la pili ni muhimu kuangalia upatikanaji wa vifaa vya uchunguzi pamoja na vifaa kwa ajili ya wauguzi na madaktari kuweza kujinga na maambukizi wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa.

Tatu, katika Ofisi ya Waziri Mkuu iko haja ya kutenga bajeti ya dharura ili kukabiliana na janga hili kwani dharura inaweza kutokea wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, nnem mwaka 2017 tulipitisha sheria ya mgawanyo wa wafanyakazi katika taasisi za Muungano asilimia 72 kwa 28 likiwemo Bunge la Jamhuri ya Muungano hadi sasa marekebisho ya wafanyakazi bado, naomba lifanyiwe kazi ili uwiano upatikane.

Tano, kutokana na janga la Corona Serikali iangalie ni namna gani kuangalia kuondoa kodi kwa biashara zote zilizoathirika kutokana na janga hili walau kwa miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa ushauri wangu utafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwa maandishi na nitachangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika maeneo mawili ya afya na maji.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza na maeneo hayo mawili, naomba kuipongeza Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na wasaidizi wake wakuu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kwa makubwa wanayowatendea Watanzania hususan wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo wadogo pamoja na wafanyakabiashara-wamachinga nchini. Ahsanteni sana kwa kuwatetea na kuwasitiri utu wao kwa namna iliyotukuka, ni Mwenyezi Mungu pekee ndiye atakayewalipa.

Mheshimiwa Spika, Job Yustino Ndugai pamoja na msaidizi wako Mkuu Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika hongereni sana kwa kulismamia na kuliendesha Bunge hili la Kumi na Moja kwa ustadi wa hali ya juu. Mmetupitisha salama katika majaribu mengi na sasa mmeendelea kutudhihirishia uwezo wenu mkubwa katika kipindi hiki kigumu cha janga la dunia la maambukizi ya Covid-19. Kwa kweli mlisahili nafasi hizo na mnastahili kuendelea kuliongoza Bunge la Kumi na Mbili ili nchi hii ya Tanzania iendelee kuwa tulivu na yenye amani.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri anayehusika na afya kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kusimamia kudhibiti maambukizi ya virusi vipyta vya Corona nchini kwa ustadi mkubwa. Kwa kweli ni muhimu kufuata miongozo ya *WHO* katika vita hii ya dunia nzima. Nilitaka kuiomba Serikali ijiandae na kukabiliana na milipuko utakapoingia kwenye Jamii mapema ikiwa tutafikia hatua hiyo itakayolazimu kuwa na wahudumu wa afya wengi na vifaa tiba na vitendanishi kwa wingi sana. Ni bora kuijandaa hata kama Mwenyezi Mungu atatuepusha na janga hilo na kwa kweli tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atuepusha na janga hili.

Aidha, naomba tusilisahau tatizo la UKIMWI, na naomba Serikali izingatie mapendekezo ya Kamati ya UKIMWI hususan kuutunisha Mfuko pamoja na kutenga fedha zetu za ndani za kutosha kuwezesha kazi za kudhibiti maambukizi mapya na kuwashumia wanaoishi na VVU zifanyike kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee eneo moja la sekta ya maji ambalo ni matumizi ya *force account* katika kutekeleza na kusimamia miradi ya maji nchini. Uamuza huu uliofanywa na Serikali ya awamu ya tano na kusimamiwa na Mheshimiwa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Maji pamoja na timu yake yote ya Wizara ya Maji ni uamuza wa kihistoria unaotuondolea dhulma walijokuwa wanaipata wananchi hasa wa vijiji ya kutopata huduma stahiki ya maji na kwa wakati. Nikitolea mfano miradi ya maji ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, tulikuwa na wakandarasi wanne,

(Ockra, Elegance, Vibe na Kipera) pamoja na mhandisi mshauri, Norplan. Baada ya Waziri wa Maji kuachana nao kwa sababu za mikataba, miradi hiyo sasa inatekelezwa kwa *force account* na gharama za miradi yote kwa ujumla imeshuka kwa zaidi ya asilimia 45! Hiyo ni faida kubwa sana, imeokoa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, wasiwasи wangu ambao ningependa Serikali iniondolee ni rasilimali watu kwa upande mmoja wa *TARURA* na kupotea kwa kazi na ajira kwa upande wa wakandarasi. Ushauri wangu ni kuwa wakandarasi wajirekebishe kwa kushirikiana na wahandisi wa Wizara wanaoanda *BOQs*, waache kuifilisi Serikali na kuwadhalumu wananchi wanaokosa huduma ya maji wanayostahili na kwa wakati na *TARURA* waongezewe uwezo wa kuwasimamia wakandarasi kwa miradi mikubwa na uwezo wa kutekeleza miradi wao wenye kwa miradi midogo na ya kati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo; kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wake pamoja na Waziri Mkuu pamoja na Naibu wote wawili kwa utekelezaji mzuri wa llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji huo mzuri naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo; kwanza ni usambaji wa umeme vijiji. Nipongeze dhamira ya dhati ya Serikali ya kusambaza umeme na kufikia zaidi ya vijiji 9000, ombi langu kwenye usambazaji umeme kuangalia yale maeneo ambayo bado usambazaji wa umeme kama ilivyo kwenye Jimbo la Tunduru Kusini ambapo kati ya vijiji 65 ni vijiji vitano ndio vina umeme tena kwa mitaa michache sana kama kijiji cha Mchuruka, Azimio, Umoja, Chiwana na Airport pamoja na kijiji cha Mbesa. Hivyo ninaomba Serikali kuititia

mradi wa REA /// sehemu ya pili kutoa kipaumbele maeneo ambayo yapo nyuma kama ilivyo Jimbo la Tunduru Kusini.

Pili ni usambazaji wa maji vijijini; ninaishukuru Serikali kutupatia miradi ya maji mitano katika vijiji vya Amani, Mtina, Mbesa, Lukumbule na miradi midogo midogo ya Namasakata, Nalasi, Chiwana, Semeni.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kuongeza kiwango cha fedha kwenye maji vijijini kwani vijiji vingi havina maji kutokana na tabianchi, mito mingi imekauka hivyo kuna mahitaji ya visima vifupi na visima virefu. Kutokana na uwezo mdogo wa wananchi wetu kulipia maji huko vijijini ni vyema miradi hiyo iwekewe umeme wa jua kupunguza gharama za uendeshaji, hasa kwenye mradi wa Nalasi, Lukumbule na Mtina. Serikali imetumia fedha nyingi sana lakini haifanyi kazi kama ilivyotarajiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu barabara za vijijini na mijini. Kutokana na hali ya mvua nyingi zilizonyesha mwaka 2019/2020 ninaomba Serikali kuangalia uwezekaji wa kuongeza fedha TARURA ili iweze kukarabati barabara na madaraja zilizoharibika na mvua. Kuna haja ya kuongezea TARURA fedha kutoka Mfuko wa Barabara kutoka 30% mpaka 40% ili kutengeneza barabara nyingi zaidi kwani mazao mengi ya chakula na biashara yanatoka huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, nne ni suala la elimu ya msingi na sekondari. Ninaomba Serikali kutenga fedha nyingi za kujenga madarasa ya shule ya msingi na sekondari kukabiliana na wingi wa wanafunzi ili kuondokana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaosoma katika darasa moja.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Tunduru Kusini wananchi walifyatua tofali zaidi ya laki moja kwa ajili ya kujenga miundombinu za shule za msingi na sekondari lakini Halmashauri imekosa fedha za kujenga miundombinu hiyo. Hivyo ninaiomba Serikali kutoa fedha kuunga mkono juhudhi hizo za wananchi ili kupunguza adha ya madarasa na vyoo pamoa na nyumba za walimu.

Vilevile shule nyingi za kata hazina maabara ya sayansi pamoja na upungufu wa walimu wa sayansi. Ni vyema Serikali ikaitupia jicho.

Katika Jimbo la Tunduru Kusini hakuna sekondari ya *high school*, hivyo ninaiomba Serikali kuweka *high school* katika kila tarafa ili kuongeza usihofu wa watoto kwenda *high school*.

Mheshimiwa Spika, tano, ujenzi wa vituo vya afya na zahanati. Nipongeze Serikali kwa kutupa vituo vitatu katika Halmashauri ya Tunduru, pamoja na pongezi ninaomba Serikali iongeze kukarabati Kituo cha Afya Mtina ambacho hazikupata majengo ya ziada ya kuboresha kama ilivyo Nkasale na Mchoteka. Vilevile ninaiomba Serikali kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Kituo cha Afya Nalasi, Mbeya ambapo kuna vijiji sita na kata mbili na wakazi zaidi 30,000.

Vilevile ninaomba ongezeko la kasi ya ujenzi ya zahanati kwani bado idadi ya zahanati na vituo vya afya ni ndogo ukilinganisha na idadi ya watu.

MHE. MWANTUM DAU HAJI: Mheshimiwa Spika, kuna suala la watu wenye ulemavu na wanawake na vijana ambaao bado hawajitambui kuhusu vikundi na asilimia kumi na mikopo ya *VICOBA*. Mikopo yao hawawezi kurejesha marejesho katika Halmashauri zao, wanajisahau na kupelekea madeni makubwa kwenye mabenki na Halmashauri kukaa na madeni hayo kwa kweli hili lioneokane na Serikali, lakini pia naishauri Serikali ifanye juu chini iwafanyie semina au mafunzo kwenye Halmashauri zao ili wajue nini maana ya mikopo na wajue kuwa kuna wenzao wanasubiri pesa ile ya marejesho.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la walemavu huwa hawataki kukaa vikundi kutokana na matatizo yao ya kuwa wako mbali mbali kukutana inakuwa vigumu, kwa hiyo asilimia mbili hii inakuwa haina kazi kubwa katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, vilevile watu wenye ulemavu hawana ushauri kuhusu Corona, bado hawafahamu kitu wapowapo tu. Kwa kweli hili Serikali ilitambue na kuwapatia ufahamu walemvu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la vijana na kuhusu ajira; vijana wengi hawajui kuhusu ajira, wanakwenda wapi vijana, wanazurura zurura vibaya huko nchini. Serikali ilione hili na ajira zikitoka zinakuwa kidogo, wasaidiwe vijana hao.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la madawa ya kulevyia pamoja na jitihada zake bado hili janga la madawa lipo, vijana wanateketea Serikali ichukue jitihada kubwa ili liondoke kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa nimpongeze Rais wangu Mheshimiwa John Joseph Pombe Magufuli kwa Jitihada zake anazoendelea kuzifanya nchini pamoja na watendaji wake wote wana chapa kazi kweli.

Pia nikushukuru wewe Spika kwa jitihada zako unavyolisimamia Bunge tukufu, kwa kweli wewe ni mfano wa kuigwa. Nimshukuru Waziri Mkuu kwa umahiri wake wa kazi zake anazozifanya kwa kweli yeye ni mfano wa kuigwa pamoja na Mawaziri wenzake wote wanachapa kazi kweli.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuleta maoni yangu niloyaona, ahsante na naomba kuwasilisha.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, naomba kuanza mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai.

Pili naomba nikushukuru wewe kwa namna unavyoliongoza Bunge hili la awamu ya tano kwa umahiri mkubwa na weledi wa kiwango cha juu. Pia nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John J. P. Magufuli kwa namna Mwenyezi Mungu alivyomjalia vipawa mbalimbali vinavyomwezesha

kuliongoza Taifa letu kwa weledi mkubwa. Na mwisho lakini si kwa umuhimu nitoe pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na unyenyekevu mkubwa aliouonyesha katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa hili. Pia nimpongeze yeye pamoja na wasaidizi wake katika ofisi yake kwa namna wanavyojituma kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba nianze mchango wangu kwa kuanza na sekta ya uwekezaji. Pamoja na mazingira mazuri ya uwekezaji nchini lakini bado kuna watendaji hawaendi na kasi ya Rais wetu. Tatizo lingine ni upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji hasa kwa wawekezaji wa mashamba makubwa, kodi nazo kwa wawekezaji sio tu zimekuwa kubwa pia zimekuwa nyingi zinazofanana. Hapa ninamaana mamlaka za usimamizi ni nyingi mno zinazofanana kimantiki japo zina majina tofauti.

Mheshimiwa Spika, sekta nyingine ninayopenda kuchangia ni sekta ya ardhi, Taifa letu sasa linakumbwa na tatizo kubwa la uuzwaji holela wa ardhi. Huku vijiji watu wanauza sana bila ya utaratibu. Serikali za Vijiji zimepewa mamlaka ya kuuza si zaidi ya heka 50, lakini wajanja huenda huko vijiji na majina ya ukoo mzima ili wapate ardhi kubwa zaidi. Mfano Mkoa wa Lindi lindi hili la uuzwaji wa ardhi ni mkubwa sana kwa ajili ya mashamba ya korosho na ufuta. Hili linaenda sambamba na uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababishwa na ukataji hovyo wa miti kwa kigezo cha kufungua mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, lingine katika hili ni suala la mipango miji, idara hii ina uhaba mkubwa wa wataalam wa mipango miji jambo linalosabisha miji yetu isipangike na badala yake tunakuja na sera ya urasimishaji. Katika Halmashauri zetu urasimishaji huu unatuongezea matatizo badala ya kutatua tatizo. Naomba kuishauri Serikali kuongeza wataalam wa upimaji na upangaji miji katika Halmashauri zetu nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaloomba kuchangia ni juu ya taasisi au idara za Serikali zile zilizotengewa fedha zake kwa mujibu wa sheria, kama vile REA, maji UCSAF na kadhalika. Fedha hizi ni bora zikaenda kwa wakati mara zinapokusanya kutoka Serikali Kuu kwani iko miradi inayokwama au kuchelewa katika taasisi hizo kwa kigezo cha ukosefu wa fedha na kwa kuwa fedha zilitengwa mahususi kwa kazi hizo basi Serikali ione umuhimu wa kupeleka fedha hizo haraka.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu wastaaifu; kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa kwa wastaaifu kupata mafao yao, kwa sasa muda mfupi zaidi kwa mstaaifu kupata mafao yake ni miezi sita. Naiomba Serikali kupunguza muda huu kwani wastaaifu hawa huwa ni kama adhabu kustaifu kwao, wakati wengine kama si wote wamelitumikia Taifa hili kwa weledi utumishi uliotukuka. Hivyo basi Serikali ione umuhimu wa watu hawa kupewa stahiki zao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali ifanye utafiti wa kina kuona kama ni Mkoa gani, una umri gani, Wilaya gani ina umri gani au ni Halmashauri gani ina umri, hili litaisaidia Serikali inapojenga majengo yake ya kitaasisi yawe uwiano wa kitaifa zaidi. Mfano ziko Wilaya au Halmashauri za muda mrefu hazina majengo ya Kiserikali, wakati ziko Wilaya mpya au Halmashauri mpya zimekamilika kwa majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, Liwale ni mionganini mwa Wilaya za Mkoa wa Lindi, Wilaya hii ni ya tangu mwaka 1975 lakini hadi leo hii Wilaya hii haina jengo hata moja lenye hadhi ya Wilaya. Wilaya ya Liwale, haina ofisi ya Mkuu wa Wilaya, haina jengo la Mahakama ya Wilaya, haina jengo la Polisi la Wilaya, haina jengo la Hospitali ya Wilaya, haina jengo la Halmashauri ya Wilaya. Hii ni mifano michache niliyoamua kuitoa kusisitiza hoja yangu.

Naiomba Serikali kuzingatia ushauri wangu ili kuimarisha umoja wa Taifa letu katika kugawana keki yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naomba nirudie tena kuishukuru tena Serikali ya awamu ya tano kwa niaba ya Wanaliwale kwa kuendelea kutupatia umeme vijijiini, kutujengea vituo viwili nya afya, kutupatia miradi ya maji katika kata nne, Wanaliwale wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa yote tuliyotendewa na Serikali yake ya CCM.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana viongozi wetu wote, Mheshimiwa John Pombe Magufuli - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu - Makamu wa Rais, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu pamoja na wewe Mheshimiwa Spika wetu na waandamizi wengine wote kwa nafasi zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Watanzania tuungane kwa pamoja kumwomba sana Mwenyezi Mungu aiepushe Tanzania na dunia nzima kwa janga hili la dunia, kwa kweli hakuna mbadala katika janga hili.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ije na mkakati wa kuboresha kukabiliana na majanga kwa kutazama, kutathimini na athari za tabianchi kwa kutenga fedha, wataalam na vifaa ambavyo kwa matukio ya sasa hali hii ya maafa na majanga haiepukiki.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kuitia Halmashauri iteue shule moja ya msingi na sekondari zenye mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu ili kupata fursa elimu kwa kuwa kwa sasa kundi hili halina mfumo rasmi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawaambia wapinzani kuwa kila Mtanzania ameelewa Serikali ya CCM imefanya nini, kwa hiyo *propaganda* haina nafasi tena katika Serikali ya awamu ya tano, tukutane Oktoba kitaelewaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja asilimia 100.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa yote anayotutendea sisi viumbe wake hapa duniani. Hata tunayopitia hivi sasa ya COVID-19 ni matakwa yake yeye Mola wetu, tunamuomba atuepushe na janga hilo la kimataifa na kutupatia hali ya furaha, amani na upendo, Amen.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kiongozi wetu wa nchi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuongoza vema wananchi wake na kuletea maendeleo makubwa katika kipindi cha miaka minne iliyopita ya uongozi wake. Miradi mikubwa mikubwa ya maendeleo imeandaliwa na kuanza kutekelezwa. mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (*standard gauge railway*), ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere, ununuzi wa ndege nane na ya tisa inakuja kwa ajili ya shirika letu la ndege (*Air Tanzania*), ujenzi wa Hospitali za Wilaya kwa nchi nzima, ujenzi wa Vituo vya Afya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Morogoro Kusini tumenufaika kwa kupata Hospitali ya Wilaya inayojengwa Mvhuha, vituo vitatu vya afya kwenye Kata za Duthumi, Kisemu na Kisaki. Ujenzi wa majengo yote matano kwa kila kituo katika vituo viwili vya afya vya Duthumi na Kisemu, vimekamilika. Tunasubiri vifaa na mashine zipelekwe pamoja na madaktari na wauguzi na wafanyakazi wengine ili vituo hivyo vianze kufanya kazi ya kuwashudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kisaki fedha zake za ujenzi zimekwishatolewa na Serikali, kwa kweli kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais mwenyewe alipotembelea Kisaki na maandalizi ya ujenzi umeshaanza. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa moyo wake wa huruma, upendo na kututhamini. Tunasema asante.

Napenda pia kumshukuru Mama yetu mpendwa Mheshimiwa Janeth Magufuli, kwa upendo mkubwa alionao moyoni mwake kwa kutupatia baiskeli kumi kwa ajili ya watoto walemaruvu katika jimbo langu la Morogoro Kusini. Namshukuru sana mama yetu Mwenyezi Mungu amzidishie, Amen.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2020/2021. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwa ufasaha na ustadi mkubwa mafanikio yaliyopatikana katika Awamu ya Tano chini ya kiongozi wetu mkuu, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kazi kubwa na nzuri umefanyaika, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi na wasaidizi wako kwa kutuletea Bungeni maendeleo ya kidijitali. Mheshimiwa Spika umekuwa mstari wa mbele kwenye mabadiliko haya ya kisayansi ndani ya Bunge la Tanzania lakini pia umekuwa mfano wa kuigwa wa kuimarisha mahusiano mazuri kati ya Bunge na mihilli mingine miwili hapa nchini; Serikali na Mahakama. Kuwepo kwa mahusiano haya mazuri kati ya mihimili yetu mitatu hapa nchini kunatuletea uhakika wa kuwepo maendeleo, amani na ufanisi mzuri katika jamii yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeelezea mambo mengi yanayomgusa kila mwananchi. Mvua zinazonyesha kwa nguvu nchini kote jumboni kwangu imeleta madhara makubwa kwenye miundombinu ya barabara, mashamba na nyumba za wananchi. Kwa bahati mbaya mafuriko haya kwenye maeneo kama Kata ya Selembala huwaibua mamba wanaotoka Mto wa Mvuha na kuwadhuru wananchi. Mwanafunzi wa miaka kumi na moja anayeitwa Rahma Ramadhani Nemelagani wa darasa la nne wa shule ya Msingi

Kiganila aliuawa kwa kuliwa na mamba. Mwenyezi Mungu amuweke mahala pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Spika, barabara yetu ya Bigwa - Mvuha - Kisaki kujengwa kwa kiwango cha lami, Serikali inasubiri nini? Naomba tuanze kujenga. Barabara za ndani la Jimbo la Morogoro Kusini ambazo ndizo zinakwenda kwa wananchi vijijini kwenye mashamba zimeharibiwa na mvua. Tunaomba Serikali itusaidie fedha za kutengeneza barabara hizi kwa kiwango cha kustahimili mvua hizi. Pengine wakati umefika sasa Serikali ifanye tathmini kama gharama za kila mwaka za kuweka vifusi vya udongo katika baadhi ya barabara zetu za vijijini kuna tija ikilinganishwa na gharama ya mara moja ya kuweka lami.

Mheshimiwa Spika, janga la COVID-19 Wabunge wenzangu wameeleza na Serikali imetoa maelezo muhimu ya jinsi ya kujikinga. Mungu azidi kutusimamia. Ni ugonjwa hatari. Niombe tu jamii yetu kutopuuza maelekezo yanayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kuheshimu na kutii masharti ya *quarantine*. Wanaoambukizwa ugonjwa huu sio kwa makusudi hivyo tusiwaone kama ni watu wahalifu bali wapelekwe hospitali na kwa kweli tunahitaji kuwaonesha upendo na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu wapate nafuu na kurudi kwenye afya zao za kawaida.

Mwisho, Jimbo la Morogoro Kusini linakumbushia ombi la kutupatia chuo cha ufundi - VETA na kinaweza kujengwa katika mojawapo ya Kata za Lundi, Duthumi au Kisaki. Vijana wengi wanamaliza masomo yao ya msingi na sekondari na wakipatiwa mafunzo hayo ya ufundi wataingia katika mfumo wa uchumi wa viwanda na kutoa mchango wao mkubwa. Naunga mkono hoja.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri yenyewe mafanikio kwenye sekta zote.

Mheshimiwa Spika, awamu hii imeweka historia ya nchi hii kwa ujenzi wa reli ya kisasa *SGR*, ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Mwalimu Nyerere, ununuzi wa ndege na kufufua shirika la ndege, uboreshaji wa huduma ya afya ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za Wilaya, ujenzi wa maboma ya shule za msingi na sekondari na msingi, mafanikio ya usambazaji umeme vijijini na pia miradi mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri ya bajeti, napendekeza Serikali iendelee kuimarisha Kamati ya kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa virusi vya corona (covid-19) ikiwa ni pamoja na kuwezesha kuwepo kwa *coronavirus contingency plan* kwa sekta zote. Hii itasaidia kuimarisha utambuzi wa changamoto za kiafya na za kiuchumi lakini kutambua pia fursa zilizopo na ambazo zinaweza kupunguza athari za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuchukua hatua za kuchochaea ubunifu katika kukabiliana na changamoto zinazotukabili ikiwemo hata watalaam wetu kushiriki uvumbuzi wa chanjo ya covid-19'.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iangalie fursa kwenye sekta ya kilimo na madini na kuongeza uwekezaji na hata kuvutia wawekezaji kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, napendekeza mpango wa haraka kuvutia wawekezaji katika madini ya chuma, bati na Niobium. Pia Serikali iongeze mtaji wa Benki ya Kilimo (*TADB*) na Benki ya Rasilimali (*TIB*).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunaposhuhudia mtikisiko wa uchumi kidunia, napendekeza Serikali kuangalia

jinsi ya kusaidia mabenki na hata uwekezaji kwenye kilimo kuwezesha kuwepo kwa *stimulus package*. Kuna fursa kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula na hata mazao ya mifugo. Katika kipindi hiki Serikali iendelee kusisitiza kuimarisha matumizi ya teknolojia kwenye masoko ya mazao (*TMX*) na mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwa kifupi hoja iliyoko mezani.

Naomba nitangulie kwanza kuwa kumpongeza sana Waziri Mkuu na Waziri na Naibu Waziri walioko chini yake pamoa na watendaji wote kwa wasilisho zuri na kazi nzuri inayofanyika Wizarani.

Mheshimiwa Spika, kipekee niruhusu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanyia Watanzania tangu walivyomchagua mwaka 2015. Lakini pia nichukue nafasi hii kukupongeza kwa dhati kabisa kwa jinsi ambavyo umeliongoza Bunge letu tukufu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye maliasili na utalii na afya kwenye mchango wangu huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Waziri Mkuu atusaidie mgogoro wa mpaka kati ya wananchi wa Kitongoji cha Momela na Hifadhi ya ANAPA utatuliwe kwa hekima kama ilivyo dhamira ya Mheshimiwa Rais kwa kuunda jopo la mawaziri nane. Historia inaonesha wananchi wa eneo hilo wamekuwa *victim* wa kuchomewa nyumba na kutaka kuhamishwa tangu mwaka 1951.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Momela kiko katika hatari ya kufungwa kwa sababu ya tatizo dogo sana la *ownership*. Tulikwenda pale na Naibu Waziri wa Afya akatoa maelekezo isainiwe *MOU*ya *PPP*ili *status quo* ya kituo iwe *maintained* pamoa na kupandisha hadhi kituo kiwe

charitable hospital. Hayo hayajafanyika mpaka sasa na matunda yake wananchi wa eneo hilo ambalo liko mbali na Hospitali ya Wilaya wanakosa huduma muhimu ya afya bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa 100%.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uzima kujumuika hapa leo kwa pamoja kuchangia hoja hii muhimu ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu lakini pia nikushukuru wewe binafsi kwa umahiri katika uongozi wako katika kipindi chote tukiwa hapa na hasa kwa ubunifu na mabadiliko ya matumizi ya Bunge Mtandao ambao umeturahisishia Wabunge utendaji wetu wa kazi ya kuwawakilisha wananchi wetu tunaowawakilisha.

Vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Makatibu Wakuu kwa hotuba na kazi nzuri wanayofanya kuwaleta Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani na pongezi hizo naomba kutoa mchango wangu wa ushauri kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maboresho madogo kwa kuwa hotuba imebeba mambo mengi mazuri kwa Watanzania.

Kwanza ni uwekezaji wa shamba la Mkulazi I kwa zao la alizeti. Shamba la Mkulazi I liliopo Kata ya Mkulazi, Tarafa ya Ngerengere, Mkoani Morogoro lina ukubwa wa hekta zaidi ya 61,000. Kutokana na tafiti mbalimbali za udongo, maji, hali ya hewa na kadhalika, eneo linalokubali kilimo cha miwa ni hekta 28,000 ambazo zitazalishwa sukari kupitia kampuni tanzu ya *NSSF* ya *Mkulazi Holding Company Limited*. Na

eneo lillobaki zaidi ya hekta 33,000 zinatafaa mazao mengi kama vile mahindi, mtama, mihogo na alizeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo kuu la Kampuni ya Mkulazi kwa sasa ni kuendeleza eneo linalolimwa miwa na kwa kuwa tuna tatizo kubwa la upungufu wa mbegu za alizeti kwa malighafi ya viwanda vya ndani na upungufu mkubwa wa mafuta ya kula. Naomba kuishauri Serikali kuitia Wizara kuliazima eneo hili kwa vijana, kina mama na wakulima kwa ujumla kwa utaratibu wa kilimo cha kitalu katika vikundi vya wakulima au wakulima wakubwa wenye uwezo wa kulima maeneo makubwa kilimo cha alizeti ili kutosheleza mahitaji ya viwanda vyetu ya tani zaidi ya milioni mbili kwa mwaka tofauti na sasa wanapata tani laki sita tu na kulazimika kufanya kazi chini ya kiwango na kulazimu kutumia fedha za kigeni kuagiza mafuta nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ukifanyiwa kazi kuanzia kilimo cha mwaka huu cha vuli utakuwa na faida kubwa kwa taarifa za kiuchumi na kijamii pia. Tutaongeza ajira kwa vijana, tutaongeza kipato na uchumi wa watu wetu, utainua uchumi wa tarafa, utaokoa fedha za kigeni tunazotumia sasa kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi, tutaimarisha shughuli za kiuchumi na kuimarisha huduma za jamii katika eneo la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, pili vibali vya kazi kwa wawekezaji wakubwa toka nje; pamoja na nia nzuri ya Serikali kulinda ajira za Watanzania kwa kudhibiti ajira za wageni nchini kwa utoaji wa vibali, lakini kuna nafasi za ajira lazima zishikiliwe na wenyewe au watu wa karibu wao wanaowaamini. Kwa mfano nafasi za kuu kama *CEO* na Ukarugenzi Mkuu na Fedha hii nafasi wawekezaji wanapenda kuwa watu wao kwa vigezo zaidi hasa cha uadilifu, historia, mahusiano na maono ya mtumishi binafsi na ya kampuni badala ya kuangalia utaifa pekee.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo naomba kuishauri Serikali kuangalia namna ya kuwapa na kuwaongezea muda wa vibali wenye makampuni hayo watu wao wa karibu

wanawaamini kuendelea kubaki nchini kuendeleza makampuni yao, kinyume cha hapo inaweza kumlazimu mwekezaji kusitisha uwekezaji wake nchini na kuhamishia nchi nyingine kwa kutokuwa na mtu sahihi anayemuamini kumkabidhi kusimamia rasilimali zake alizowekeza hapa nchini.

Ushauri wangu waongezewe muda wa vibali kwa muda na haraka ili kuvutia uwekezaji nchini badala ya mtizamo hasi kuwa hatutaki uwekezaji wa watu kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa vijana na ujasiriamali na biashara kwa mazao ya kilimo; vijana ni nguvu kazi kubwa sana katika Taifa letu na kwa takwimu zilizopo nguvu kazi ya Taifa zaidi ya 67% ni vijana na zaidi ya vijana, lakini kila mwaka wanaingia katika soko la ajira na uwezo wa Serikali na sekta binafsi kuajiri ni vijana laki moja na hamsini na tano tu kwa mwaka. Kwa muktadha huu sekta yenye uwezo wa kutoa ajira kwa wingi bila kubagua wala kuchagua ni sekta ya kilimo kwenye mnyororo mzima wa thamani kuanzia uzalishaji mashambani, biashara ya mazao ya kilimo, kutoa huduma ya pembejeo za kilimo, usafiri, vifungashio, zana za kilimo, fedha za mitaji, usafirishaji na kadhalika, lakini kutokana ni mifumo ya masoko ya mazao hasa kwa mazao ya kimkakati inawaondoa vijana katika kujihusisha na biashara ya mazao ya kilimo kwa wakulima kuwa kwenye soko la nje moja kwa moja au kuwa kwenye minada yenye wanunuzi wa nje ambao kimsingi ndio walikuwa wanunuzi wa wajasiriamali vijana katika kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu ukiendelea tutaweza kutengeneza matajiri na wafanyabiashara wakubwa wa kesho wa Taifa hili kwa kuwa mazao ya kilimo ndiyo msingi wa kuwatengeneza kwa uzoefu na mitaji yao mikubwa na kubambia sekta nyingine baada ya mafamikio na kujenga uchumi imara kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii naomba kushauri mfumo wa wanunuzi wa mazao ya wakulima wa stakabadhi ghalani na minada kufanyiwa

mabadiliko na kuwa na masoko ya ngazi mbili. Ngazi ya kwanza ni soko la wakulima kuwa mazao yao kupitia vyama vya msingi ili kudhibiti ubora na bei kwa wakulima. Soko hili litawahusisha wakulima kwa maana ya wauzaji na wanunuzi wa ndani, wajasiriamali, wakulima wakubwa, vyama vikuu, wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara pamoja wenyewe viwanda vya ndani vya kuchakata mazao ili kivipatia malighafi kwa bei himilivu ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuweza kushindana katika solo la kimataifa na mataifa mengine. Hawa wote ndio wanunuzi katika soko la awali na kuwa katika solo la upili kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, soko la upili ni stakabadhi ghalani au *TMX* linalowakutanisha wafanyabiashara wa ndani, wakulima wakubwa na wanunuzi wa nje kwa mazao yanayosafirishwa nje ya nchi na yanayotumika kwa viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utasaidia kutatua changamoto zilizopo katika mfumo wa ushirika na masoko ya mazao kwa sasa. Wakulima watapata malipo taslimu na kwa wakati, utaondoa rushwa kwenye ushirika, ukosefu wa malighafi kwa viwanda vya ndani mfano viwanda vya korosho na kahawa, kutoa ajira kwa vijana kwa kujiajiri katika biashara ya mazao ya kilimo na kuongeza mapato ya Serikali kwa wajasiriamali na wafanyabiashara ya kununua katika soko la awali na kuuza katika soko la upili.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi wake mahiri na miongozo yake kwangu katika kuwatumikia Watanzania kuwaletea maendeleo. Vilevile nimshukuru tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Serikali na jinsi anavyotusimamia na kutuelekeza mara kwa mara katika kutimiza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, aidha nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja muhimu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuridhia barabara kutoka Bigwa - Kisaki kujengwa kwa kiwango cha lami kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 kufuatia maombi ya watu wa Morogoro Kusini Mashariki kupitia mimi Mbunge wao hapa Bungeni na Bunge lake kupitisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya bajeti hiyo kupita kwa barabara hiyo ya Bigwa - Kisaki kujengwa kwa lami na kuendelea kuomba Serikali na kushauri kuhimiza ujenzi kuanza haraka kutokana na umuhimu wa barabara hii kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yangu kutoa kibali cha ujenzi wa barabara hii ili mchakato wa kutafuta mkandarasi ukaanza ili kuanza ujenzi mwaka huu. Pia nashauri kwa kuwa nafamu Serikali ina majukumu mengi na tatizo la kukabiliana na Corona kwa sasa basi naiomba Serikali barabara yote ya kilometra 78 basi inaweza kutoa kwa awamu, kwa mwaka huu Serikali ikatoa kwa awamu hata kwa kilometra 40 na mwaka mwingine kutoa sehemu iliyobaki kilometra 38 ili ujenzi wa barabara mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara hii kwa sasa umeongezeka sana pamoja na Makao Mkuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, kupita katika tarafa tano kati ya sita za Halmashauri ya Morogoro lakini barabara hii inakwenda kwenye mbuga nyeti ya Hifadhi ya Nyerere, Mbuga ya Hifadhi ya Wanyama ya Selous kwenda kwenye Bwawa la Kisasa la Nyerere pamoja na kuunganisha mikoa ya Morogoro na Pwani.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii utarahishia ujenzi wa Bwawa la Nyerere, kuimarisha shughuli za utalii kwa kuboresha barabara pamoja na kukuza uchumi wa watu wetu kwa kurahisisha mawasiliano yao na kupunguza gharama za usafirishaji wa mazao na kuongeza kipato na uchumi wa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, barabara hii kila mwaka Serikali inatumia zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa mwaka kwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe lakini bado inaharibika hasa kutokana na madhara ya mbuga.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine Serikali kutoa kibali cha ujenzi mapema ili kuanza ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kwa kuniunga mkono na ushirikiano wanaonipa na kuwatumikia kuwalettea maendeleo yanayoonekana jimboni kwa macho.

Mheshimiwa Spika, nakushuru wewe tena kwa kunipa nafasi na ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, kwanzu kabisa nimpongeze Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia nimpongeze Waziri Mkuu pamoja na timu yake kwa kuwasilisha hutuba yake nzuri iliyogusa kila mahitaji ya Watanzania.

Mheshima Spika, naomba nianze kuchangia suala zima la afya na niendelee kuipongeza Serikali yangu tukufu kwa kujenga vituo vya afya zaidi ya 350 na zaidi pamoja na Hospitali za Wilaya, pamoja na hayo kuna maeneo mengine wananchi wamejitlea kujenga vituo vya afya kwa nguvu zao pamoja na zahanati na wamefikia hatua nguvu zimewaishia, hivyo wanahitaji Serikali yao tukufu iwaunge mkono kama maeneo mengine walivyopewa fedha kwa ajili ya kujenga majengo ya kisasa.

Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu iwapatie wananchi wa Jimbo la Lushoto fedha kwa ajili ya kumalizia vituo viwili vya afya ambavyo kimoja kipo Kata ya Gare na cha pili kipo Kata ya Ngwelo, kwani vituo hivi vikimalizika, vitapunguza

usumbufu wanaoendelea kuupata kwa kutembea zaidi ya kilometra 50 mpaka 60 kufuata huduma za afya Wilayani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna zahanati nyingi zimejengwa kwa nguvu za wananchi na zimeisha lakini hazina vifaa tiba pamoja na watumishi, kwa hiyo niiombe Serikali yangu itenge fedha za kutosha katika bajeti hii ili zahanati zile ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi zianze kutoa huduma kwa wananchi wetu pamoja na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, nichangie suala la elimu, niipongeze Serikali kwa kujenga madarasa mengi ya sekondari na msingi, kwakweli madarasa yale yameleta tija na ufanisi mkubwa hasa kwa wananchi, kwa jitihada hizi naomba niishauri Serikali yangu tukufu kwa nini isitumie mfumo huu huu kumalizila maabara zillizojengwa kwa nguvu za wananchi, pamoja na kujenga hosteli katika mashule yetu ya sekondali ili wanafunzi wetu wa kike kuepuka kupata mimba za utotonu na zisizokuwa za lazima na watoto hawa kutimiza ndoto zao.

Kwa kuwa Jimbo la Lushoto lina shule za sekondari zaidi ya 30 na zenye hosteli ni sekondari tatu tu na hosteli hizo hazina ubora. Kwa hiyo niiombe Serikali yangu iweze kunipatia fedha ili tuweze kujenga hosteli angalau katika sekondari zifuatazo Malimbwi Sekondari, Mariam Mshangama Sekondari, Kwai Sekondari, Ubiri Sekondari, Claus Sekondari na Ngwelo Sekondari.

Mheshimiwa Spika, tutakapojenga hosteli katika shule hizi tutakuwa tumewaokoa watoto hasa wa kike katika janga hili la kupata mimba na pia ufaulu utaongezeka katika mashule yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara zetu hasa za *TARURA* kwa kweli chombo hiki kinafanya vizuri ila kina changamoto ya rasilimali fedha na ukizingatia chombo hiki kina barabara nyingi za vijijini ambazo ndizo zinazotoa mazao kutoka kwa wakulima, hivyo basi niishauri Serikali yangu

iongeze asilimia kumi ili jumla wapewe asilimia 40 angalau wataweza kukabiliana na changamoto hizi za barabara kuliko ilivyo kuwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme, niendelee kuipongeza Serikali yangu tukufu kwa kusambaza zaidi ya vijiji 9000 mpaka sasa, kwa kweli ni kazi kubwa sana imefanyika, ushauri wangu niiombe Serikali yangu itenge bajeti ya kumalizia vijiji vilivyobaki ili kuondoa manung'uniko kwa wale ambaao bado hawajapata umeme, hasa katika Jimbo la Lushoto lenye vijiji 62 lakini vilivyopata umeme ni vijiji 30 tu.

Kwa hiyo bado vijiji 32 na hii imeleta malalamiko ya kila siku na sisi Wabunge kuulizwa maswali ya kila siku na kukosa majibu yake, pamoja na haya Waziri wa Nishati alitoa waraka wa gharama za umeme zisizidi shilingi 27,000 lakini maagizo hayo hayafuatwi, wananchi bado wanalamika, kwani wanapofika *TANESCO* wanaambiwa hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu naomba Waziri atoe tamko tena na ufuatiliaji ufanyike pamoja na kutoa onyo kali kwa Mameneja wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, wakati tunaelekeea katika ukomo wa Bunge hili, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza na kuwapongeza Wabunge wenzangu wote kwa kazi tuliyofanya hapa kwa muda wa miaka hii mitano.

Mheshimiwa Spika, tumepata changamoto kadhaa lakini sote tumshukuru Mungu na changamoto hizo zitumike katika kuboresha Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu kuna mambo mengi yaliyozungumzwa. Hata hivyo ningependa kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu elimu kuna ongezeko kubwa la watoto wanaoingia katika shule za msingi na sekondari hasa baada ya Serikali kuondoa ada. Hata hivyo ongezeko hilo haliendani na hali halisi iliyopo katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhaba wa walimu, ili kuhakikisha dhamira ya Serikali kukuza elimu inafanikiwa, Serikali inao wajibu wa kuongeza ajira za walimu pamoja na uboreshaji stahiki zao yaani makazi yao, mishahara, posho na stahiki nyingine.

Mheshimiwa Spika, pili ni vyumba nya madarasa, kila mwanzo wa mwaka wa masomo katika kidato cha kwanza na cha sita kunakuwa na upungufu wa vyumba nya madarasa. Hali hii inaleta usumbufu mkubwa kwa wanafunzi kwa kuwa wengine hucheleva kuanza masomo. Kwa kuwa idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na wale wanaomaliza kidato cha nne wanajulikana, wataalam wetu wanao wajibu wa kulishughulikia tatizo hili mapema ili kuondoa usumbufu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo bado tuna upungufu mkubwa wa vyumba nya maabara na vifaa nya maabara, ni vema Serikali kuangalia katika bajeti hii uwezekano wa kukamilisha vyumba nya maabara ambavyo vilianzishwa.

Mheshimiwa Spika, shule nyngi za zamani za msingi zinaelekea kubomoka. Jimboni kwangu kuna shule nyngi zinabomoka na hazikaliki au zinapaswa kufungwa. Kama Serikali ilivyofanya jitihada ya kuboresha shule za sekondari za zamani ione uwezekano wa kuboresha shule za misingi pia.

Mheshimiwa Spika, tatu ni shule za ufundi; ni muhimu tuharakishe ujenzi wa shule za ufundi katika kila Wilaya hasa kipindi hiki ambacho tunahimiza uchumi wa viwanda na kuimarisha *private sector* ili vijana wetu baada ya kumaliza elimu yao katika ngazi mbalimbali waweze kujilajiri.

Mheshimiwa Spika, mageuzi yaliyofanyika kuanzishwa kwa *TARURA* yameleta mafanikio makubwa sana katika Halmashauri zetu. Hata hivyo, *TARURA* inakumbwa na tatizo kubwa la kibajeti.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa fedha za Mfuko wa Barabara kugawanywa kwa kiwango sawa kati ya *TANROADS* na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji ni kubwa sana nchi nzima. Katika jimbo langu limekuwa kubwa zaidi kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha chemichemi nyingi kukauka, ongezeko la binadamu na wanyama na kadhalika. Pamoja na hayo yote chanzo cha maji kimekuwa kile kile tangu enzi za ukoloni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa dhamira yake ya kuanzisha chanzo kipycha ya Ziwa Chala. Naiomba Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi huu ili kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tunapoteza maji mengi sana kutokana na maji ya mvua. Wilaya ya Rombo tuna mito mingi sana ya msimu na inayopitisha maji mengi sana wakati wa mvua na ina makorongo ambayo yanaweza kuzuiwa ili kuhifadhi maji hayo sambamba na kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuperomoka kwa vyama nya ushirika Waziri Mkuu amefanya jitihada kubwa za kuufufua na kupambana na ufisadi ndani ya ushirika. Chama cha Ushirika cha *KNCU* ambacho nacho killilingiliwa na ufisadi kilikuwa msaada mkubwa kwa wakulima wa kahawa katika Wilaya ya Rombo na Mkoa wa Kilimanjaro kwa jumla. Hivi sasa wakulima wengi wameamua kuachana na kilimo cha kahawa na kupanda mbogamboga na migomba. Licha ya ushirika, pembejeo ni ghali sana, bei ni ndogo na hivyo kuwakatisha tamaa wakulima. Ni vema Serikali iingilie kati ili zao hilo lisije likatoweka maana lilikuwa chanzo kikubwa cha fedha za kigeni na uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, umezuka ukatili wa kuwadhalilisha watoto katika jamii. Watoto wanaingiliwa kinyume na maumbile, wanaingiliana wenyewe kwa wenyewe na mimba za utotoni mashulenii. Wengi hawaongelei jambo hili kwa kuchelea aibu lakini kama Taifa tusipokuwa makini Taifa letu linaweza kuja kugeuka kuwa la mashoga. Serikali iondoe uoga, ichunguze na kushughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati, kazi inayofanyika kupeleka umeme vijijiini na *REA* ni nzuri na ya kupongeza. Naiomba Serikali kuendelea kumaliza maeneo yaliyobaki na hasa katika jimbo langu yapo maeneo yaliyobaki na yenye malalamiko yafanyiwe kazi ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, katika awamu hii hospitali na vituo vingi vya afya vimejengwa nchi nzima. Katika Jimbo la Rombo ipo Hospitali ya Wilaya inajengwa na kituo cha afya. Hata hivyo Rombo tuna uhaba mkubwa wa watumishi wa idara ya afya. Ninaishauri sana Serikali kwamba sambamba na ujenzi wa hospitali na vituo hivi vya afya Serikali iajiri watumishi wa afya nchini kote.

Mheshimiwa Spika, mwisho mengi yamefanyika katika awamu hii. Katika miundombinu, sekta zote yaani barabara ingawa mvua zinazoendelea kunyesha imeleta athari kubwa lakini kazi inaendelea, usafiri wa anga na reli kazi zinaendelea, hali kadhalika meli na vivuko katika maziwa yetu yameboresha usafiri na sekta ya uvuvi. Kwa hali hiyo kama Watanzania tunao wajibu wa kupongeza jitihada hizi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipongeze Serikali kwa kazi kubwa na nzuri sana inayofanyika ya kutuletea maendeleo Watanzania. Nimpongeze Rais wetu mpandwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uongozi wa kizalendo usio mfano wa kuiongoza nchi yetu. Nimpongeze pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru na kumpongeza sana rafiki na kiongozi wangu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ya kusimamia shughuli za Serikali. Kazi inaonekana, huduma zinaonekana, maendeleo yanaonekana na hilo hakuna ubishi.

Mheshimiwa Spika, Niipongeze sana Serikali kwa maendeleo makubwa ambayo yamepatikana katika jimbo langu la Buchosa. Mambo ni mengi haina sababu ya kuyataja katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ningependa kutoa ushauri kwa Serikali ni kuhusu urahisishaji wa namna ya kufanya biashara hapa nchini. Katika eneo hilo bado yako mambo ambayo yanasuryua wafanyabiashara. *Blue print* inabidi ifanyiwe kazi kwa nguvu zaidi. Kuna taasisi za udhibiti bado zinasuryua wafanyabiashara badala ya kuwawezesha na kuwasimamia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ninampongeza Waziri Mkuu kwa namna ambavyo anachapa kazi yeye na wasaidizi wake wote katika kutekeleza mipango mbalimbali ya kibajeti ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mvua zilizonyesha zimeathiri kwa kiasi kikubwa na uharibifu mkubwa wa barabara nyingi, mashamba na mifugo.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kuona namna ya kusaidia kwa haraka sana kuhakikisha wananchi wanapata chakula. Kupimiwa viwanja bure, kuwafanya wananchi kuwa na makazi na kujenga maeneo salama.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze fedha upande wa ujenzi, barabara zimeathiriwa sana, sasa shughuli za usafiri na usafirishaji zimekuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tunahamia upande wa Waheshimiwa Mawaziri, tunaanza na Mheshimiwa Josephat Kandege, dakika tano; utafuatiwa na Mheshimiwa Kwandikwa dakika tano pia. Mhesimiwa Kandege!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wamepongeza hotuba nzuri sana ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa dakika tano na hoja ambazo zimeibuka kuhusiana na Wizara ya TAMISEMI sina uhakika nitagusa ngapi lakini kwa sababu tarehe 8/4/2020 Mheshimiwa Waziri wa Nchi atakuwa na fursa ya kuwasilisha hotuba yake, ufanuzi tutautoa na tutakuwa na muda wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa niruhusu nипитie machache katika kutoa ufanuzi. Kuna hoja ambayo ilikuwa imelbiliwa na Mheshimiwa *Engineer Chrisotpher Chiza* ambayo ilikuwa inahusu ushauri katika majengo ya Serikali na hasa katika maeneo ambayo kuna matukio mengi ya radi, akashauri Serikali ianze kuweka vitega radi. Naamini katika maeneo ambayo yanapata tatizo kubwa ni pamoja na Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanatoka maeneo ambayo kuna usumbufu mkubwa wa radi, wazo hili sisi kama Serikali tumelichukua na tulishaanza kulifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, katika majengo yote ya Taasisi za Umma ambayo yataendelea kujengwa tutahakikisha

kwamba tunaweka vitega radi, kwa sababu pale ambapo radi inatokea athari zake zinakuwa kubwa. Ni vizuri pia hata wananchi sisi Waheshimiwa Wabunge tutumie fursa kuelimisha wananchi kwa sababu gharama yake wala sio kubwa sana katika kuweka vitega radi.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambayo ilikuwa imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kidogo akiwepo Mheshimiwa Vulu, Mheshimiwa Bobali Hassan, Mheshimiwa Christina Ishengoma, Mheshimiwa Livingstone Lusinde ikiwa inaongelea suala zima la *TARURA* pamoja na kazi nzuri ambayo inafanyika, lakini wameomba kwamba ikiwezekana bajeti ya *TARURA* itazamwe.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba maeneo mengi *TARURA* imekuwa ikifanya kazi vizuri ukiachilia mbali huo ufinyu wa bajeti, lakini pia ni vizuri pia tukakumbushana kwamba pamoja na kwamba *TARURA* inahudumia takribani kilometra 108,942, pia *TANROAD* nayo ambayo ina mzigoto mkubwa kwa sababu barabara zake nyingi ambazo zinajengwa ni zile za kiwango cha lami ambayo gharama yake ni kubwa, lakini ni ukweli usiopingika na baada ya hili Serikali kulitambua tumeanza kupitia *formula* ambayo itasaidia.

Mheshimiwa Spika, pia ni ukweli usiopingika kwamba tukitegemea bajeti hii ambayo tunatenga kila mwaka kwa ajili ya kujenga Taasisi kubwa kama *TARURA*, fedha hii haitoshi. Ndiyo maana Serikali inatumia vyanzo vingine kuhakikisha kwamba tunaijengea uwezo *TARURA* kama ambavyo hata mwanzo *TANROADS* ilijengewa uwezo ikasisimama vizuri ili iweze kufanya kazi kama ambavyo inatarajiwa na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015 bajeti imekuwa ikiongezeka kwa kadri inavyopatikana. Tunaendelea kujengea uwezo *TARURA* ili ifanye kazi nzuri kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wamesifia kazi nzuri ambayo inafanywa na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ambayo iliibuliwa na Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji ambayo inahusu Jimbo lake ambako kumepatikana mafuriko makubwa sana, lakini kipekee akawa anaomba kwamba Kituo cha Afya kile ambacho hakiwezi kutumika hata baada ya kwamba mafuriko yameondoka, basi ni vizuri Serikali ikatazama uwezekano wa kujenga Kituo cha Afya kipyaa.

Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge, avute subira kama ambavyo nimesema kwamba kuanzia tarehe 8, bajeti yetu itawasilishwa, atapata ufanuzi ulio mzuri kuhusiana na nini ambacho tumepanga kufanya.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja pia ambayo imeibuka ambayo ni vizuri nikatumia fursa hii kutoa ufanuzi; kuna Kampuni ambayo inajenga *Stiegler's Gorge* kule ambapo kumekuwa na ubishano, *service levy ilipwe wapi?* Je, inatakiwa ilipwe sehemu ambayo Ofisi iko kwa maana ya Kinondoni au ilipwe sehemu ambayo mradi unatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa maelekezo mahususi; Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeelekeza *service levy* inatakiwa ilipwe kule ambako mradi unatekelezwa na wanufaika ni Rufiji pamoja na Morogoro vijijini. Kwa hiyo, hoja ya kwamba Ofisi iko Kinondoni ndiyo eti *service levy* ikalipiwe Kinondoni, siyo sahihi hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Elias Kwandikwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili name niweze kuchangia katika hotuba hii muhimu na ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninaomba uniruhusu pia nimfikishie salamu za Watanzania walio wengi, kila mahali tulipotembelea miradi, tumekuwa tukipokea pongezi na salamu za wananchi wakisema kufikishe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, pongezi kwa Mheshimiwa Rais. Nami nitumie nafasi hii niziwasilishe salamu na pongezi kutoka kwa wananchi, kwa sababu wanatambua kwamba Serikali yao ya Awamu ya Tano kwa kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ndiyo kiunganishi muhimu cha sekta za uchumi katika nchi hii na kwamba ni kichocheo katika kukua kwa uchumi na maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nizungumze tu kama ufanuzi kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza nianze kwa kuwapongeza kwa michango mizuri na utashuhudia kwamba uchangiaji wa bajeti una mabadiliko makubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa sababu kwa sehemu kubwa tumepokea ushauri na sehemu kubwa tumepokea maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza majukumu yetu, wanafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, nami nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla na yale yote ambayo wameyatoa kama ushauri, nasi kama Serikali na kama Wizara pia tutaendelea kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nifafanue tu mambo mawili ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi walizungumza hasa hoja ya kuimarisha miundombinu iliyoharibiwa na mvua katika kipindi hiki ambacho tumepokea mvua nyingi. Niseme tu kwamba Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu hasa ya barabara na madaraja yaliyoharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha nchini kuanzia kipindi cha Oktoba, 2019 mpaka mwezi Machi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba tumejipanga kwa maana ya kuendelea kurejeshea miundombinu. Ukiangalia kwa ujumla wake, ukubwa wake kwa kipindi hiki kulikuwa kuna makadirio kama ya shilingi bilioni 34.3 ambapo upande wa *TARURA* ilikuwa kama shilingi bilioni 40 na upande

wa *TANROAD* shilingi bilioni 34. Kwa hiyo, utaona athari hizi zimetuchota mafungu makubwa sana kuendelea kuimarisha.

Mheshimiwa Spika, kubwa niseme tu kwamba tumejipanga vizuri kuhakikisha Serikali inaendelea kurejesha miundombinu ili ile sera ya kuhakikisha wananchi wanapita na kwenda kwenye shughuli zao za maendeleo, ziendelee bila kupata kikwazo chochote.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara hii muhimu ambayo Mheshimiwa Lubeleje alikuwa ameizungumzia. Hii barabara utakubaliana nami kwamba ni barabara muhimu. Ni barabara inayotuunganisha kutoka Mbande kwenda Kongwa - Mpwapwa mpaka kule Kibakwe. Hii barabara tulishaifanyia usanifu kwa ajili ya kufanya matengenezo. Kwa sasa shughuli za ujenzi zinaendelea, Mkandarasi aliyeko kwenye *site* amekamilisha kilometra tano na zile kilometra nyiningine 11.7 kukamilisha kilometra 16.5 kwenda mpaka Kongwa ikifika mwezi wa Tano natumaini kwamba tutakamilisha barabara hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile uko ujenzi wa kilometra mbili ukitoka Mpwapwa kuja Kongwa unaendelea vizuri na tumeshasaini mkataba na Mkandarasi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubeleje na wananchi wa maeneo hayo tuliyoyataja wasiwe na wasiwasi, tumejipanga vizuri kuona kwamba tunaendelea kupeleka huduma hii muhimu ya barabara kuelekea Mpwapwa na siyo Mpwapwa peke yake, kwenda mpaka maeneo mengine ambayo tunajua yanayo uzalishaji mkubwa na huduma hii ni muhimu sana kwa Wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lubeleje pia alizungumza juu ya madaraja muhimu sana haya; kule Godegode, Mpwapwa, Nyasungwi na Mbande. Niseme tu, katika mwaka wa fedha huu ambao tunaokwenda nao tulitenga fedha na kazi ya usanifu wa madaraja hayo ulishakamilika. Tunaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba tunarejesha madaraja haya muhimu ambayo Mheshimiwa Lubeleje ameyataja, nasi tunayaangalia kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa ujumla wake, Dodoma ni kati ya Mikoa ambayo imeshambuliwa sana na hizi mvua nydingi tulizopata. Kwa hiyo, utaona Dodoma ni kubwa, maeneo mengi yalikuwa yamepata athari za mvua. Niwahakikishie tu wakazi wa Dodoma na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kwamba tumejipanga kuhakikisha tunaenda kufanya maboresho makubwa kwenye maeneo haya ambayo yameharibiwa; siyo hapa Dodoma tu, lakini na maeneo mengine ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka nichangie hayo kwa sababu ya muda, lakini niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba tutakwenda kufanya maboresho ya miundombinu hii. Yumkini katika bajeti inayokuja pia tutaonyesha namna tulivyojipanga ili maeneo yote haya yaliyopata athari za mvua tutakavyoyafanya urejeshaji kupitia bajeti.

Mheshimiwa Spika, naamini Bunge lako litatupitishia fedha ili tuende kufanya kazi kubwa kuhakikisha wananchi wanarudishiwa huduma muhimu za miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ni hotuba nzuri na bajeti nzuri ili tuende tukafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Elias John Kwandikwa. Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa sababu hotuba hii imeeleza

kwa ufasaha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano na imainisha kazi ambayo inakwenda kufanyika katika mwaka 2020/2021. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya katika Serikali hii.

Pia napenda kuwapongeza Mawaziri katika Ofisi yake, Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Angella Kairuki, hakika wanaonyesha mfano namna ambavyo wanawake wanafanya kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika Sekta ya Elimu na niseme kwamba michango yote tumeipokea. Kwa sababu ya muda na kwa kuzingatia kwamba ndiyo mara yangu ya kwanza kuongea Bungeni tangu Benki ya Dunia ilipopitisha mkopo wa shilingi milioni 500, nitumile nafasi hili kutoa shukurani za dhati kwa Benki ya Dunia kwa kuidhinisha mkopo huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, unafahamu namna ambavyo mkopo huu uliletä sintofahamu na hata kuna kipindi ambapo katika Bunge lako kulikuwa na mjadala kuhusu suala hili. Tunashukuru kwamba baada ya majadiliano wameweza kuzipitisha. Niseme kwamba fedha hizi zinakwenda kuimarisha elimu ya sekondari, zinakwenda kuondoa vikwazo na hasa kwa watoto wa kike kuhakikisha kwamba wanapata elimu iliyo bora. Mradi huu utakwenda kunufaisha watoto wasiopungua 6,500,000 na utatoa kwa elimu kwa watoto wote wa kike na wa kiume bila ubaguzi wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi huu utasimamiwa na Wizara ya Elimu ambayo ndiyo ina dhamana ya kusimamia elimu hapa nchini na tutahakikisha kwamba tunasimamia mradi huu kwa kushirikiana na wadau wote muhimu.

Kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania kwamba Serikali iliomba huu mkopo kwa sababu ina dhamira ya dhati ya kuboresha elimu. Kwa sababu sasa mkopo umeidhinishwa, Serikali inakwenda kuutekeleza kama ambavyo tumekubaliana na Benki ya Dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu na wakati mwingine huwa unakemea hizi tabia; yapo mambo ambayo yameshaanza kuleta majadiliano kuhusiana na huu mkopo na ndiyo maana nimeona mimi mchango wangu niutumie katika kuleta ufanuzi. Mradi huu unatekelezwa katika mfumo wa "Lipa Kulingana na Matokeo" kama ambavyo Wabunge wote mnafahamu mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo tulionao. Tunao uzoefu, tunayo dhamira, tunao uwezo wa kuhakikisha kwamba tutatekeleza mradi huu kulingana na mipango ambayo tumeiweka ili tuweze kufikia malengo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania, nia yetu iko pale pale, uwezo wetu uko pale pale, tunakwenda kuimarisha elimu yetu na tutahakikisha kwamba tunawashirikisha wadau wote katika hatua zote ili kuhakikisha tunafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia mradi huu ambaao utakuwa na mazingira ambayo ni jumuishi na rafiki kwa watoto wetu wote, nizungumzie na mimi janga ambalo liko kwenye nchi yetu na dunia kwa ujumla, suala la virusi vya *Corona*.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu shule zetu zimefungwa, wanafunzi wako nyumbani. Hivyo basi, imekuwa kwa kweli ni jambo ambalo kidogo linaathiri hali yetu ya elimu kama ambavyo linaathiri sekta nyingine. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuendelea kusisitiza na katika mchango wa Wabunge, kuna suala ambalo lilijitokeza kwamba kuna baadhi ya wazazi ambaao watoto wao wanaendelea kwenda *tuition*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekataza mikusanyiko isiyokuwa ya lazima na Serikali ilifunga shule kwa sababu ya kuwaweka watoto katika mazingira salama ili wasiwe na mikusanyiko. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kusema kwamba *tuition* zote zinazofanyika sasa hivi ni batili. Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wahakikishe kwamba wanasimamia

maelekezo ya Serikali. Mtu ye yeyote anayeendesha *tuition*, ni batili, achukuliwe hatua inayotakiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kutambua kwamba Wanafunzi wako nyumbani na wanahitaji kuendelea kuwa wanapata elimu hata wakiwa nyumbani, tunayo huduma ya maktaba ambayo inatolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo kiutaratibu ili uweze kupata vitabu katika huduma hiyo ilikuwa unapaswa kulipa. Sasa kwa kutambua kwamba wanafunzi wamefunga shule, Serikali inatoa huduma ya upatikanaji wa vitabu vyote kuanzia Elimu ya Awali, vya Shule ya Msingi, Shule ya Sekondari kuanzia *O-level* na *A-level* bila malipo yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwasih i sana wanafunzi wote, huko waliko majumbani kwao watumie muda wao kusoma vitabu ambavyo Serikali inawapa *access* bila gharama yoyote badala ya kwenda kuzurura mitaani na kuiweka katika hatari ya kuweza kupata maambukizi ya virusi vya *corona*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, narudia kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Prof. Ndalichako. Baadaye ukiwapatia Wabunge hiyo *link* ya huo mtandao wa Maktaba ya Taifa inaitwaje, itasaidia sana kuwapatia wapiga kura. Ahsante sana.

Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani, Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli inatekelezeka kwa asilimia 100. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri wengine waliochangia kupongeza kwa kweli taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu maeneo ambayo nitapita kwa kifupi sana ni matatu. Jambo la kwanza ililioneckana ni kuhusiana na suala la *LNG* na suala la pili ni mradi wa mafuta wa *ECOP*wa Uganda na Tanzania na eneo la umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze na la mwisho. Katika eneo hili la kupeleka umeme vijijini, napenda niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaonisikiliza kwamba jambo hili limetupa sifa sana kidunia, tumefanya kazi nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, labda niwapitishe Waheshimiwa Wabunge kidogo tu. Mwaka 2008 tulipoanza kutekeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini tulikuwa kwenye nafasi ya 50 Afrika na tulifikisha asilimia 16.5 lakini Mwaka 2015 tulipofikisha sasa asilimia 39.5 tulikuwa na nafasi ya 25 Afrika. Mwaka 2017 tukiwa tunasogea sasa, wakati tunapelekea umeme vijijini tulifikia asilimia 47 tukiwa kwenye nafasi ya 18. Mwaka 2018 tulifikia nafasi ya nne Afrika tukiwa na asilimia takribani 58. Mwaka 2019 mwezi Desemba tulikuwa nafasi ya tatu, wakitupita Afrika Kusini na Nigeria. Mwaka huu mwezi wa Pili tukashika namba moja. (*Makof*/ *Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu, mwaka 2019 Afrika Kusini walikuwa na silimia 64 umeme vijijini; Nigeria walikuwa na asilimia 72 kwa umeme vijijini; leo sisi tunapoongea tuna asilimia 75.2 umeme vijijini. Kwa nini nimelazimika kuyasema haya?

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa kipindi chote hiki kuwapelekea umeme Watanzania. Takribani shilingi trilioni 2.8 zimetumika kuwapelekea umeme wananchi kwenye maeneo haya. Hongera sana Mheshimiwa Spika, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nampongeza sana Mheshimiwa Rais katika jukumu hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, huwezi ukazungumza uchumi wa viwanda kama umeme vijijini haupo. Viwanda vinajengwa na *raw materials* kutoka vijijini, kwa hiyo msitari wa kwanza kupeleka viwanda ni kuanzia vijijini. Serikali yetu imejipambanua vizuri; huwezi leo ukazungumza kujenga kiwanda Dar es Salaam, eneo liko wapi? Huwezi kuzungumza kujenga kiwanda kizuri Dodoma Mjini, eneo liko wapi? Maeneo ya viwanda yako vijijini, ndio maana umeme tumepeleka huko. Kwa hiyo, jambo hili tumelitekeleza vizuri sana, naipongeza sana Serikali. Katika hili, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. Wametupa ushirikiano mzuri sana katika kufanya kazi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeona niseme machache katika eneo hili kwa sababu ya muda. Najua tutawasilisha taarifa yetu mwezi ujao tarehe 26, nitaeleza kwa upana zaidi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi, tunapoongea hapa, zipo Wilaya 35 ambazo Kata zake zote zimefikiwa na umeme, vijiji vyake vyote vimefikiwa na umeme. Kwa hiyo, mradi unaokuja hatutapeleka umeme kwenye vijiji, bali kwenye Vitongoji tu. Ni jambo kubwa sana limefanyika kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, katika eneo hilo, ni-reserve muda tu kwa ajili ya taarifa nyingine ambazo nimetakiwa nizieleze mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la mradi wa *LNG* kumekuwa na *concern* kubwa sana kwamba inawezekana mradi huu hautekelezeki. Naomba nitoe taarifa mbele ya Bunge lako tukufu; mradi wa *LNG* uko pale pale. Utatekelezwa na kazi za kufanya zinafanyika na Serikali imetenga fedha na harakati za kutekeleza zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe taarifa kidogo. Ni kweli takriban miaka miwili iliyopita *speed* imekuwa siyo nzuri na zipo sababu za msingi. Sababu ya kwanza, kwanza nilipongeze Bunge lako, mwaka 2018 uliunda Tume Maalum ya Wabunge Kupitia Mikataba ya Kugawana Mapato. Katika mapendekezo ya Tume ya Wabunge, ilipendekeza mikataba

yote 11 (*PSA*'s) zifanyiwe mapitio na taratibu nyingine ziendelee baada ya mapitio hayo kukamilika. Sasa hili ni letu sisi kama Serikali. Tulifanya hivyo kwa nia njema ili kuhakikisha kwamba tunapokwenda huko mbele ya safari hatuangukii shimonii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baada ya mapendekezo ya Tume ya Bunge, Serikali imefanyia kazi mapendekezo hayo. Pamoja na kazi iliyofanyika ni kufanya mapitio. Mwanasheria Mkuu wa Serikali amefanya kazi hiyo, nampongeza sana na kazi imekamilika. Hivi karibuni taarifa imewasilishwa Serikalini. Kinachofanyika sasa, Serikali inatafakari taarifa hiyo ili mapendekezo yatakayotokana na mapitio hayo sasa tuendelee na hatua ya utekelezaji wa mradi wa *LNG*.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua tu tuliyofikia, jambo la kwanza tumetenga gesi asilia tani milioni 10 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali iko pale pale. Jambo la pili, tumetenga fedha kuwalipa wafidiwa 693 ambao watafidiwa takribani ekari 2,071; na hivyo pesa zipo. Najua Waziri wa Fedha amejiandaa kuwalipa taratibu zikikamilika, nadhani ni mwisho wa kipindi cha fedha cha mwaka huu. Kwa hiyo, ambao wamepitija na mradi huu wawe na imani na Serikali, watalipwa fidia zao ilimradi uhakiki utafanyika. Nimeona nitoe taarifa kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni mradi wa mafuta wa Hoima na Tanzania. Kwanza naipongeza Serikali mradi huu unatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nieleze tu kidogo yapo mambo mawili ambayo tumeyafikia kwa sasa. Jambo la kwanza ni wenzetu Waganda walianza majadiliano na wazalishaji wa mafuta kwenye mkondo wa juu, imetuchukuwa muda mrefu lakini napenda kutoa taarifa kwamba wametuletea taarifa majadiliano wamekamilisha kwa hiyo sasa kuanzia hapo tunaweza kuendelea na mradi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili tumekamilisha kwa upande wetu tadhimini ya watakao fidiwa ambao wanafika watu takribani watu elfu tisa kwa upande wa korido, lakini takribani watu elfu 3,420 kwenye maeneo yatakapo jengwa *camp* fedha zipo takribani bilioni 50 zimetengwa na Serikali yetu tukufu na Bunge lilipitisha tunashukuru sana kwa kazi hii. Kwa hiyo, niseme tu kwamba miradi itatekelezeka bila wasiwasi wote isipokuwa haya mambo mawili tunayakamilisha.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwenye mradi huu ni suala la corona tunachofanya kwa sasa kwa sababu wataalam wetu hawawezi kwenda Uganda na waganda kuja Tanzania tunafanya mikutano kwa video *conference* ili kuonyesha kwamba Serikali tumekusudia kutekeleza mradi huu, kwa sababu ya muda nimeona nichangie haya machache sasa naunga hoja asilimia mia moja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani sasa atakuja Mheshimiwa Waziri Fedha na Mipango Dkt Philip Mpango dakika saba.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nianze kwa kuunga mkono hoja iliyosomwa hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa umahiri mkubwa kabisa lakini niwapongeze pia mawaziri wote na watendaji katika ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye hoja tu moja kubwa ambayo ilisemwa karibu na wachangiaji wote na ni hoja ya corona.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme ni kweli mlipuko wa virusi vya corona licha ya adhari kubwa za kiafya umekuwa ni tishio kubwa kwa mafanikio ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika bara la Afrika lakini pia na dunia nzima. *United Nations economic commission for Africa* wamekadiria kwamba ukuwaji wa uchumi wa bara letu la Afrika unaweza kuanguka kwa kati ya asilimia 2 mpaka 3 katika mwaka huu 2020.

Mheshimiwa Spika, lakini Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) tayari wameshatangaza kwamba uchumi wa dunia unaingia kwenye m dororo katika mwaka 2020, *economic research*. Sasa sisi kama nchi kama zilivyo nchi nyingine tumeanza kupata madhara katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia wamezisema sehemu mbalimbali hususani upande wa utalii kuna shida kubwa na mnyororo mzima wa sekta ya utalii, lakini mapato yanayotokana na biashara mbalimbali ndani na nje ya nchi tunaona tatizo, lakini pia usafiri wa anga biashara za maua tunaona shida uzalishaji viwandani nk.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa kutokana na hali hiyo Serikali imeunda kikosi kazi cha wataalam ambacho kinaendelea kufanya uchambuzi wa kina wa athari hizi zinazojitokeza na niseme tu kwamba hii kazi ni muhimu ikafanyika kwa umakini na ndiyo iweze kuwa msingi wa kuandaa programme ya kiuchumi ya kukabiliana na janga hili vinginevyo tunaweza kuishia *alarmist* lakini bila *fact* kutoka kwenye sekta mbalimbali ili tuweze kuhakikisha tunaanda mikakati ambayo kweli ni hakika na timu hii inajumuisha wenzenetu kutoka Zanzibar wako kwenye kamati ya kitaalam lakini pia kwenye kamati ya kitaifa ambayo inaongozwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, katika Wizara yangu tumeelekeza pia na Wizara zote za kisekta ikiwemo benki kuu kukutana na wadau mbalimbali kwa majadiliano ili tupokee mapendekezo yao na baadhi tumeshapokea *Tanzania Association of two operators*, tumepokea kutoka Umoja wa Mabenki Tanzania *Hurting operators*, Shirikisho la Vyama vya Utalii, *Tanzania Private sector foundation*, kuna ma casino kadhaa lakini *Tanzania horticulture Association* na wadau wengine na tunawashukuru sana kwa michango yao milango iko wazi tunaomba na wengine watuletee mapendekezo yao katika Sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nitakacho fanya sasa, naombwa nitoe tu vidokezo vya mikakati ambavyo inaandaliwa hivi sasa na viko katika sehemu tu kuu tatu. Sehemu ya kwanza

ni ugharamiaji wa mahitaji ya msingi ya vifaa ya kujikinga na corona lakini pia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutokea huduma za afya ili ni jambo la msingi sana ili tuweze kuokoa maisha ya watu wetu kwa hiyo maana yake ni kwamba ni pamoja na vituo mahususi vya kutolea huduma, tiba za dharura lakini pia lengo kubwa likiwa ni kuzuia maambukizi ya corona kwa hiyo, lazima tufikirie gharama za vifaa kinga *person protective equipment* masuala ya barakoa, *ventilators, gaunt* za wahudumu wa afya na madaktari na n.k.

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni pamoja pia na gharama za kutafuta namna ya kuongeza madaktari na watumishi wengine wa afya kwa hiyo, hii ni *block* ya kwanza na vyanzo vya kugharamia eneo hili ambavyo tunafikiria ni pamoja na bajeti kuu ya Serikali hususani kasima ile ya dharura, mapato ya halmashauri mchango ya hiari ya wananchi, makampuni binafsi na umma, misaada ya fedha na vifaa na mikopo nafuu kutoka kwa taasisi za fedha za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pia nchi rafiki na ninapenda nitumie nafasi hii kama mfano tu kutambua mchango wa *Twiga Minerals Cooperation Limited* ambayo tayari wameahidi kutoa mchango wa dolla za kimarekani 1.8 milioni ambazo zitatumika kusaidia *Isolatin Untis* Mlonganzila na vituo vingine vya karantini, mabibo hostel. Lakini pia kusaidia *Isolation centre* Musoma, Shinyanga na Geita, pia ziko fedha kwa ajili ya kusaidia shughuli za kupambana na janga hili katika ngazi za *local Government* na tunawashukuru sana kwa dhati na tunaomba na wengine waige mfano huu mzuri makampuni mengine, mabenki, taasisi na wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea kushauriana na IMF na benki ya dunia kuhusu namna nchi yetu inaweza kunufaika na programme za dharura za Taasisi hizo ili kukabiliana na hili janga. Kwa upande wa *World Bank* na *IFS* wana programme inaitwa *Fast track COVID – 19 facility* na *IMF* wana *rapid crediting facility for low income country's* tunaendelea na majadiliano tuone namna ambavyo Tanzania inaweza ikanufaika na sehemu hizi.

Mheshimiwa Spika, nguzo ya pili, ni kupunguza makali ya mdodoro wa uchumi hasa katika sekta ambazo zimeadhirika na nimeshayaeleza, sekta ambazo tayari kuna dalili za kuumia kwa hiyo, hatua ambazo tunafikiria ni pamoja na kuhakikisha hifadhi ya chakula ya kutosha nchini, kuchukua hatua za kibajeti ikiwa ni pamoja ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi katika baadhi ya maeneo na kuzielekeza kuongeza nguvu kukabiliana na corona, lakini kukarabati miundombinu ya usafirishaji ili tuweze kuwafikia wananchi wetu hasa walioko vijijini lakini tutaongeza kasi ya kulipa madeni na malimbikizo ya madai mbalimba lakini pia kuchukuwa hatua za kikodi na za kiutawala zinazolenga kutoa huweni kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nguzo ya tatu ya mpango ambaao unaandalisha, ni hatua ya kuilinda sekta ya fedha na lengo ni kuhakikisha mabenki yetu yanaendelea kuwa na ukwasi wa kutosha tuna akiba ya fedha ya fedha ya kigeni ya kutosha lakini sarafu pia iendelee kuwa imara na itakuwa ni muhimu tudhibiti ongezeko kubwa la mikopo chechefu lakini hususani kwa kuwapa nafuu mabenki...

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Malizia.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mhehsimiwa Spika, tutatoa unafuu kwa mabenki ili yaweze kufanya *loan rescheduling* kwa maelezo hayo machache, nilitaka tu niliakikishie tu Bunge lako tukufu kwamba Serikali ipo kazini kuandaa mpango wa kupambana na madhara ya corona ya kiuchumi na muwe na uhakika tutakapo kamilisha tutawasilisha kwa maamuzi ndani ya Serikali na Bunge litapata taarifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa fedha na Mipango sasa tunaingia ndani ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaanza na Naibu Waziri Stella Ikupa dakika saba. Ikilia tu kengele maana dakika saba zimeisha.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana nafasi awali ya yote ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya ulinzi wake katika kipindi chote cha miaka ambayo nimekuwa ndani ya Bunge lako tukufu toka 2015.

Mheshimiwa Spika, Iakini pia nitumie kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kumsaidia kwenye eneo hili la watu wenyе ulemavu. (*Makofи*)

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo Serikali yake imeweza kumdhampuni mtu mwenye ulemavu na kuhakikisha kwamba mambo mbalimbali ya watu wenyе ulemavu yanashughullika na hatimaye ustawi wa mtu mwenye ulemavu kuweza kuonekana iliwa ni pamoja na kumjumuisha kwenye maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Rais hatuna kitu cha kukulipa sisi kama watu wenyе ulemavu zaidi ya kuendelea kukuombea afya njema lakini pia ulinzi, pia baada ya hapa maisha ya hapa dunia ninaamini kuna maisha mengine basi usima wa milele. (*Makofи*)

Mheshimiwa Spika, nitumie kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu ninakushukuru sana kwa miongozo ambayo umeendelea kunipatia na hatimaye nimeweza kutekeleza majukumu yangu vizuri na kuendelea kukusaidia kwenye eneo hili la watu wenyе ulemavu, Mheshimiwa Waziri Mkuu ninakushukuru sana nimeweza kufurahia vizuri maisha ndani ya ofisi yako. (*Makofи*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Jenista dada yangu kwa jinsi ambavyo ameendelea kuniongoza kwa jinsi ambavyo ameendelea kunelekeza sita koma kumshukuru kwa kweli amekuwa ni dada yangu mzuri sana na kuniongoza katika utendaji wangu wa kazi Mheshimiwa Jenista nakushukuru. (*Makofи*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia sambamba na hilo nikushukuru Mheshimiwa Angella Kairuki, dada yangu kwa jinsi ambavyo umeendelea kuniongoza na kunipa maelekezo mbalimbali niweze kukushukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu Mheshimiwa Antony Peter Mavunde kwa ushirikiano mkubwa ambao umenipatia katika kutekeleza majikumu yangu ndani ya ofisi ya Waziri mkuu nikushukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika wewe mwenyewe pamoja na Naibu Spika kwa jinsi ambavyo mmeweza kuliongoza Bunge letu, pia kwa jinsi ambavyo umeyashughulia masuala ya watu wenye ulemavu tunaona umehakikisha kwamba maeneo mbalimbali ndani ya viwanja hivi vya bunge yanakuwa ni rafiki kwa watu wenye ulemavu ninakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana makatibu wakuu ndani ya ofisi ya Waziri Mkuu, makatibu wakuu wako watatu, kipekee kabisa nikushukuru Andrew Masawe umenipatia sana ushirikiano mkubwa sana katika kutekeleza majikumu yangu. Ninaomba nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi za kuweza kutenga nafasi mbili za watu wenye ulemavu ambazo zimeniwezesha kuingia mimi na Mheshimiwa Amina Mollel pacha wangu Mbunge machachari hakika amekuwa akifuatilia vizuri utekelezwaji wa masuala ya watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wakinamama UWT Mkoa wa Dar es Salaam lakini pia UWT ngazi ya mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na visiwani. Ninaenda haraka haraka kwa sababu ya muda naomba nijikite sasa kwenye hoja zilizotolewa na waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ambayo inaitaka Serikali kuweza kuimarisha kitengo cha watu wenye Ulemavu pia Baraza la Ushauri kwa watu wenye ulemavu, kushughulikia migogoro ya vyama vya watu wenye ulemavu. Serikali ya Awamu ya Tano tunaposema kwamba imetekeliza imetekeliza masuala ya watu wenye ulemavu

imeteketeza kweli kweli na inaendelea kuyatekelez kwa kishindo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kitengo cha watu wenye ulemavu tumeendelea kuhakikisha kwamba fedha zinatengwa rasilimali fedha zinatengwa kwa ajili ya kitengo hiki kupitia kifungu cha 2034, lakini pia tumeendelea kukipatia vitendea kazi vyta kisasa kitengo hiki. Sambamba na hilo tumeongeza watumishi katika kitengo hiki ikiwa ni pamoa na kuteuwa kaimu mkurugenzi wa kitengo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa baraza Serikali imeweza kulizindua Baraza la Ushauri kwa watu wenye ulemavu kwa kuwa lilikuwa limemaza muda wake. Mheshimiwa Rais aliteua Mwenyekiti na hatimaye Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aliweza kuteua wajumbe wa baraza hilli na baraza hilli liliweza kuzinduliwa mwezi Juni, 2019 na linaendelea kutelekeza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na pia tumeendelea kulitengea fedha.

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande wa migogoro ya watu wenye ulemavu tumeendelea kuvifuatilia vyama hivi na kuvishauri kuhakikisha kwamba vinatekeleza katiba ambazo vimeweza kujivekea vyenyewe. Katika hilo katika eneo la kutatua migogoro basi mfano mmoja wapo mzuri ni Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Viungo (CHAWATA) ambacho kilikuwa kimeshindwa kufanya uchaguzi kwa takribani miaka kumi. Serikali iliweza kuingilia kati na kufuatilia mgogoro huu pia tulienda mbali zaidi kwa kuwapatia rasilimali fedha na hatimaye uchaguzi wao uliweza kufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja pia ya kwamba Serikali iweze kutekeleza Mkataba wa Marakesh. Ikkumbukwe kwamba 2019 Septemba, 11 Bunge lako liliweza kuridhia Mkataba huu wa Marakesh na hatimaye kusainiwa na Mheshimiwa Rais. Baada ya hapo ulipelekwa nchini Geniva ambapo kwenye Shirika la Hati miliki (*World Intellectual Property Organization*) ambako sasa

umepelekwa kwa ajili ya uhakiki na hatimaye uweze kutelezwa kama ambavyo inatakiwa.

Mheshimiwa Spika, tunaposema kwamba Serikali yetu imetekeleza mambo mengi imetekeleza kweli kweli. Pamoja na hilo Serikali imeweza kuvifufua vyuo vitatu nya ufundi kwa watu wenyе ulemavu. Vyuo hivi kimoja kipo Mkoani Tabora ambacho Ruwanzari, lakini pia Mkoani Tanga (Masiwani) na Mirongo Mkoani Mwanza na kupelekea kwamba idadi ya vyuo hivi kuwa vyuo vitano na pale mwanzoni vilikuwa viwili.

Mheshimiwa Spika, hili lilikuwa ni tamanio kubwa la watu wenyе ulemavu kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinafunguliwa na vinasaidia watu wenyе ulemavu ambao wanashindwa kuendelea na masomo ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Serikali imeweza kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa kwa watu wenyе ulemavu kwa kuufungulia akaunti katika Benki Kuu ya Tanzania. Sambamba na hilo Serikali imeweza kupendekeza Mfuko huu uweze kutengewa shilingi milioni mia mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya machache ninaomba nitumie Bunge lako Tukufu hili kuwatachia Waheshimiwa Wabunge wote kila la kheri na upendeleo wa Mwenyezi Mungu na kibali kiendelelee kuwa pamoja na sisi ili tuweze kurejea katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante nawasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge makofi hayo hayatoshi. (*Makofi*)

Ahsante sana Mheshimiwa Stella Ikupa dada yetu tunakupongeza sana na tunafarijika sana kuwa nawe. Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu tafadhali dakika saba pia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA

NA AJIRA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliye niwezesha kusimama siku ya leo.

Mheshimiwa pia, nachukua fursa hii kipekee kabisa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani na heshima kubwa aliyonipa ya kuendelea kuhudumu katika eneo hili kama Naibu Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo yao ambayo imetusaidia sana katika utendaji kazi katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nisingependa sana kurejea maneno ya Waheshimiwa Wabunge waliotangulia lakini niseme tu kwa kipekee kabisa tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa upendo wake, uvumilivu na namna ambavyo ametuongoza katika ofisi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru kipekee sana Mama yangu mpendwa, Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama pamoja na Dada yangu Mheshimiwa Angela Kairuki kwa namna ambavyo mmendelea kutulea katika Ofisi ya Waziri Mkuu na kutupa ushauri lakini na upendo wenu wa dhati amba o umefanya kazi hii iwe nyepesi sana kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Makatibu Wakuu wote chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Watendani wote kwa ushirikiano mkubwa sana walionipatia lakini bila kumsahau Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu dada yangu lkupa Stella Alex kwa namna tulivyoshirikiana kwa pamoja kutekeleza majukumu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nichukue fursa hii kukupongeza sana wewe mwenyewe kwa namna ambavyo umeleta mapinduzi makubwa ya kiteknolojia ndani ya Bunge letu. Hii ni kuonesha kwamba kuna uhusiano mkubwa sana kati ya maendeleo na teknolojia na watu wenye asili ya Mkoa wa Dodoma. Hongera sana kwa kazi kubwa ambayo umeifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa heshima kubwa walijonipa. Niwaambie tu kwamba mwili wangu bado una nguvu na akili yangu ina nguvu ya kufanya kazi ikiwapendeza niko tayari kuendelea kuwatumikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa naomba nijielekeze katika hoja za msingi ambazo zimewasilishwa. Hoja ya kwanza ilikuwa ni ushauri ambao ultolewa kwa *WCF* (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi), namna bora ya kuendelea kutoa elimu kwa waajiri ili waendelee kujandikisha na kutimiza wajibu wao kisheria. Tumepokea ushauri huu na *WCF* wanaendelea kutoa elimu kwa waajiri, wafanyakazi na wadau wote kuhakikisha kwamba takwa hili la kisheria linafanyiwa kazi kwa sababu ni jambo ambalo linawasaidia sana wafanyakazi wanaopata madhara wakiwa kazini kupata fidia.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo lilizungumzwa ni Serikali kuendelea kuwapa mafunzo ya ujuzi waraibu wa madawa ya kulevyo ambao wameachana na madawa ya kulevyo na hivyo kukosa shughuli ya kufanya. Ofisi ya Waziri Mkuu kuititia Fungu 65 tumeendelea kutekeleza ushauri huu kwa kuwahusisha waraibu wa madawa ya kulevyo katika shughuli mbalimbali za ukuzaji ujuzi. Hivi sasa tunavyozungumza katika Programu ya Kukuza Ujuzi ambayo inaendeshwa chini Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu, tumewaingiza pia watu ambao walikuwa wanatumia madawa ya kulevyo kama sehemu ya kuwajengea ujuzi na kuwafanya wapate shughuli ya kufanya na waache kuendelea kutumia madawa ya kulevyo.

Mheshimiwa Spika, nchi nzima tuna takribani watu 5,875 ambao wameshaingia katika Program ya Kukuza Ujuzi katika eneo la ufundi stadi. Kati yao watu 1,020 ni warailbu wa madawa ya kulevya. Hii ni kuonyesha kwamba ni kwa namna gani kama Serikali tuliona kwamba lazima tuwashirikishe pia na wenyewe ili waweze kupata ujuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilizungumzwa ni kuhusiana na vikundi vyta vijana kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo ilitolewa rai na Waheshimiwa Wabunge kwamba idadi ya vijana kukusanyika kuunda kikundi ni kubwa sana na wakashauri pia twenda katika hatua hata ya kumfanya kijana mmoja aweze kukopeshwa. Kama Serikali kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana tulionia hilo na kuitia Mwongozo wa mwaka 2013 ambao tumeufanyia marekebisho, hivi sasa tunakamilisha taratibu za kumfanya hata kama ni kijana mmoja ambaye anaweza kuleta tija na kuajiri vijana wengine pia anaweza kukopesheka pasipokuwa kwenye kikundi ili kuweza kuwasaidia vijana waweze kupata fursa hiyo ya kiuchumi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, pia ilijitokeza hoja ya kuboresha Programu ya Kukuza Ujuzi. Ofisi ya Waziri Mkuu inaendesha Programu ya Kukuza Ujuzi yenye lengo la kumjengea ujuzi kijana wa Kitanzania ili kuitia ujuzi huo aweze kujiajiri na kuajiri vijana wengine. Kazi hiyo tumeifanya mwaka huu lakini pia katika mwaka ujao wa fedha tutaifanya kazi hii kwa ukamilifu. Tutaendelea na Programu ya Kitalu Nyumba ambayo itafikia vijana wengi zaidi mikoa yote 14 ambayo imebaki katika awamu ya pili. Tutaendelea pia na Programu ya Kurasimisha Ujuzi kwa Vijana wenye ujuzi ambao hawajapitia mafunzo rasmi ya ufundi. Programu hii tunafanya na VETA na vijana wengi wamenufaika.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea na Programu ya Mafunzo ya Vitendo Kazini (*Internship*) ambapo hivi sasa kwa kushirikiana na sekta binafsi tunawachukua vijana wahitimu wa vyuo vikuu tunawapeleka katika taasisi mbalimbali za kibashara, iwe ni viwanda au makampuni wanakaa kwa

miezi 6 - 12 wakipata uzoefu kwa fani waliyoisoma na baadaye wanapewa Hati ya Utambulisho kwa maana ya *Certificate of Recognition*. Ikitokea siku anakwenda kuomba kazi akiulizwa uzoefu basi anaweza akatoa ile Hati kuonyesha kwamba amewahi kufanya kazi kwa vitendo kwa muda wa miezi 6 - 12 ili tuwe tumeondoa changamoto hiyo ya uzoefu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa katika eneo langu ilikuwa ni hoja ambayo ilisemwa na Waheshimiwa Wabunge ya ushiriki wa vijana katika kilimo. Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tunatekeleza mpango mkakati wa pamoja wa kuwahusisha vijana kwenye kilimo ambapo tunaanza na hatua ya kwanza ya kuwapa elimu na kuwaondolea fikra hasi kwamba kilimo ni shughuli ya mwisho ya kufanya mtu akikosa shughuli zote. Kwa hiyo, tumeanza na awamu hii ya kwanza ya kutoa elimu, tumezunguka karibuni kanda zote za nchi nzima kuwaellimsha vijana. Hatua ya pili tumeendelea kuwaweka vijana hawa katika makundi ilhali tukiendelea kusisitiza maelekezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyatoa ya kila mkoa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za kilimo na uzalishaji mali. Baada ya hapo hatua ya tatu ni kwenda kuwaunganisha na Benki ya Kilimo ili waweze kupata fursa ya mikopo na mitaji ili waendeshe shughuli hizo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naunga mkono hoja nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Antony Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi). Sasa nakuja kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Mheshimiwa Angella Kairuki, ana dakika kumi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI): Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nami niendelee pale ambapo wameishia wenzangu, kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Raís wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake shupavu unaotufikisha katika hatua hii kwa kishindo na kwa mafanikio makubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kipekee, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo mara kadhaa alikutana na wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi na amekuwa akitoa maelekezo kwetu wasaidizi wake na watendaji kuhakikisha kwamba changamoto za wawekezaji zinatatuliwa ili kuharakisha maendeleo ya nchi yetu. Nampongeza pia kwa uamuzi wake mzuri na makini wa kuliweka jukumu la kusimamia uwekezaji chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo ambalo limewezesha kupata mafanikio makubwa katika kusimamia uwekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza kipekee Makamu wa Rais pamoja na Rais wa Zanzibar kwa maelekezo mbalimbali ambayo wamekuwa wakitupatia kwa namna ambavyo tunatekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu kwa hotuba yake mahiri ambayo imeweeka msingi na mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa hakika hotuba hii pamoja na mambo mengine tumeshuhudia namna ambavyo imegusa masuala ya uwekezaji ambayo ninayasimamia chini ya uongozi wake madhubuti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana dada yangu, pacha wangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista kwa namna ambavyo tumeshirikiana kwa pamoja katika ofisi hii katika masuala mazima ambapo ametusaidia katika uratibu wa shughuli za kiserikali lakini masuala ya uwekezaji. Pia namshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde pamoja na Mheshimiwa Ikupa kwa namna ambavyo tumefanya kazi kwa karibu. Nimshukuru sana Katibu Mkuu Mama Mwaluko, Katibu Mkuu Nzunda na Bwana Masawe pamoja na watumishi wote Wakuu wa Taasisi na Wakurugenzi kwa namna ambavyo wameweza kutoa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu tulionyayo katika Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki nisipochukua nafasi hii kukushuru sana wewe binafsi kwa

namna ambavyo umetulea na kutuongoza. Vilevile namshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna ambavyo mmekuwa na usimamizi mzuri na uvezeshaji wa shughuli za Bunge lakini kwa kuanzisha huduma za Serikali mtandao. Kwa hakika na Serikali naamini haitatuchukua muda mrefu kwani itatusaidia pia na sisi katika kutoa huduma kwa wawekezaji kupunguza urasimu na gharama kwa wawekezaji wetu. Tunaamini pia kuwa mfano ambao umeuonyesha itakuwa ni chachu kubwa kwa matumizi ya Serikali mtandao pia kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nishukuru sana Kamati yetu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuititia kwa Mheshimiwa Mchengerwa (Mwenyekiti), Mheshimiwa Najma Giga (Makamu Mwenyekiti) na wajumbe wote kwa namna ambavyo wametupa ushirikiano mkubwa lakini kwa ushauri wao mzuri ambao kwa hakika umetuwezesha sana kuongeza ufanisi katika uhamasishaji, usimamizi na kufanikisha uwekezaji nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana *TNBC TIC, TPSF, TCCIA, CTI*, Jumuiya wa Wafanyabiashara Tanzania na *CEO Roundtable*. Pia sitasahau Balozi zetu za Tanzania nje ya nchi ambazo kwa hakika wamekuwa na mchango mkubwa wa kufanikisha uwekezaji na biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani zangu kwa sekta binafsi, napenda kutoa salamu za pole kwa msiba wa aliyekuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Ndugu Shamte uliotokea hivi karibuni. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua pia uwekezaji unafanya katika wilaya na mikoa, sina budi kutambua na kuwashukuru Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote, Wakuu wa Wilaya na Wenyeviti wetu wa Halmashauri, Madiwani na viongozi mbalimbali kwa namna ambavyo wamefanya kazi yangu ya kuhamasisha uwekezaji kuwa nyepesi na rahisi na kwa namna ambavyo tumeshirikiana nao. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tutaendelea

kukutana na wawekezaji na wafanyabiashara ili kuweza kusikiliza kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili na kuzitatua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee kabisa nimshukuru sana sana mume wangu kipenzi, Mheshimiwa Balozi Mbelwa Kairuki pamoja na watoto wangu Kemilembe, Kokubelwa pamoja na Mwesigwa kwa mapenzi yao na kwa uvumilivu wao kwangu wakati wote na kwa kunipa egemeo muhimu linaloniwezesha kuhimili majukumu yangu niliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru UWT, Mkoa wa Dar es Salaam, UWT - Baraza Kuu Taifa pamoja na *TUCTA* kwa ushirikiano mzuri walijonipatia napotekeleza majukumu yangu. Kwa hakika sina cha kuwalipa zaidi ya kuwashakikisha kwamba sitowaangusha. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Same.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):
Mheshimiwa Spika, naambiya nishukuru na Same hapa, Same nakuja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kipekee nielezee machache kuhusiana na wepesi wa kufanya biashara Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wote ambao wamechukua wajibu wao katika kuhakikisha kwamba tunapanda nafasi tatu katika Tathmini ya Wepesi wa Kufanya Biashara. Nishukuru Wizara zote zinazosimamia yale maeneo 11 ambayo tunapimwa kwa mchango wao mzuri ambao kwa hakika ndiyo umepelekea kupata mafanikio haya.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwashakikisha kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara mbalimbali 11 zinazosimamia maboresho, tutaweza kufanya vizuri zaidi mwaka huu mwezi wa 10 lakini na katika miaka mingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa melengo yetu kwa mwaka 2025 ni kuhakikisha kwamba tunafikia nafasi ya digit 2. Mwaka huu tulikuwa na nafasi ya 141 na tunaamini kwamba ndani ya miaka hiyo mitano ijayo tutaweza kufikia malengo hayo.

Mheshimiwa Spika, nitaje maeneo matatu ambayo tayari tumeshawenza kufikia nafasi ya tarakimu 2 ikiwemo suala la upatikanaji wa mikopo. Namshukuru sana Waziri wa Fedha na BoT tumefikia nafasi ya 67 kati ya 190. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mahiga pamoja na Jaji Mkuu kwa upande wa usuluhishi wa migogoro ya kibiasara na kulinda mikataba.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni suala la upatikanaji wa umeme kupitia kwa Mheshimiwa Kalemani ambapo tumefikia nafasi ya 85 kati ya 190. Naamini kupitia Mawaziri hawa, tunayo nafasi ya kufanya vizuri zaidi na nitoe rai kwa Mawaziri wengine na kwa Makatibu Wakuu kwenye maeneo yale mengine nane yaliyobakia kuona namna gani tutafanya maboresho ili kuwa nafasi nzuri zaidi kimataifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nishukuru sana sekta binafsi kwa uamuza wao wa kuwekeza nchini na kwa namna ambavyo wanaendelea kuwekeza mitaji. Nawaomba waendelee kuwa na imani wakitambua kwamba nafasi ya Tanzania katika biashara na uwekezaji itaendelea kuimarika zaidi, waendelee kutuamini wakitambua kwamba tutatekeleza majukumu yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kutekeleza mpango wetu wa *blueprint*, kuhuisha mpango wa kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuanzisha utaratibu wa kuwapa Ubalozi wa Heshima katika masuala ya uwekezaji; kuimarisha Kituo chetu cha Uwekezaji Tanzania na kuimarisha mfumo wa kupokea na kutatua changamoto za wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile tutaboresha sera na sheria ya uwekezaji, kuimarisha miundombinu ya kiuchumi kama vile nishati ya umeme, maji, mawasiliano na miundombinu, kuimarisha huduma za kifedha ili kuwezesha upatikanaji wa

mitaji kwa wawekezaji wa ndani na kuimarisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji kwa kuendelea kuzihimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo ya uwekezaji. Pia tutalinda wawekezaji wa ndani dhidi ya ushindani usio na haki unaotokana na uingizaji wa bidhaa za magendo.

Mheshimiwa Spika, sitaweza kujibu hoja zote lakini nishukuru sana kwa michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Tunatambua nia yenu ni kuweza kuona kwamba nchi yetu inakuwa na mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji. Ni imani yangu watumishi mbalimbali katika Wizara zetu na taasisi za Serikali wataendelea kubadilika kwenda na wakati kulea wawekezaji na kufanikisha uwekezaji ili kuhakikisha kwamba uwekezaji Tanzania unaendelea kukua, kuimarika na kuchangia zaidi katika pato la taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na niwahakikishie kwamba majibu yao watayapata kwa maandishi na tutaendelea kutekeleza yale yote waliyoshauri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji. Tunakushukuru sana kwa hotuba yako.

Sasa niombe nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (*Chief Whip*), Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, una dakika 20.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, kwa kudra za Mwenyezi Mungu, naomba kwanza nichukue nafasi hii na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha kwenye mkutano huu wa Kumi na Tisa. Huu ni mkutano wetu wa mwisho katika kipindi cha miaka mitano. *Inshallah* Mwenyezi

Mungu ametupa uhai tumeweza kufika siku hii ya leo. Kwa vile tunakwenda kwenye uchaguzi, naomba nianze kwa kukutakia wewe binafsi kila la kheri katika uchaguzi mkuu ujao. Tunaamini utapita kwa kishindo na dua za kupita bila kupingwa zikaanguke juu yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Iakini naomba nimtakie Mheshimiwa Waziri Mkuu kila la kheri. Bosi wetu, kiongozi wetu mkuu na yeye akapite bila kupingwa ili kuonyesha ni namna gani tunaweza kufanya kazi nzuri. Siwezi kuacha kusema nakitakia kila la kheri Chama changu cha Mapinduzi kikashinde kwa kishindo. Hizo lugha za kushindwa zinazotoka upande mwingine zishindwe na zilegee na tutakwenda kushinda kwa kishindo kabisa. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Sambamba na kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa dhati ya moyo wangu nakupongeza sana, wewe umeunganisha sifa za Maspika wote. Kama ni *standard* wewe umekuwa na *standard* iliyopitiliza, kama ni kutumia utaratibu na mifumo wewe umepitiliza, kwa kweli unastahili sifa zote na pongezi. Vilevile nipongeze timu ambayo imekusaidia sana Naibu Spika, tumemwona hapa amefanya kazi nzuri, Wenyevit wa Bunge na viongozi wote wakiongozwa na Katibu wa Bunge kama Mtendaji Mkuu ndani ya Bunge. Kwa kweli tunawashukuru mmefanya kazi vizuri, mmetusaidia sana Serikali kuweza kutekeleza majukumu yetu na hasa yale yanayohusiana na shughuli za kibunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niungane na Mawaziri wenzangu na Wabunge wote ambao wamempongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Wamempongeza sana inajieleza wazi hotuba ya Waziri Mkuu kwa nini Rais huyu anastahili hizo pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upande wangu naomba niongeze mambo machache kwa nini tunampongeza Rais huyu. Rais

huyu ni Rais mwenye msimamo thabiti pale yanapokuja maslahi ya Taifa la Tanzania. Rais wetu huyu ana sifa nyingine ya kutokuyumba wala kuyumbishwa kwenye maamuzi ambayo yanakwenda kuleta maendeleo kwa Watanzania na nchi yetu. Tumeshuhudia Rais wetu ni shujaa na jasiri kweli kweli na mmeona katika mambo magumu ambayo Taifa hili lilitakiwa lipite Rais wetu amesimama kuwa jasiri na shujaa hakutetereka anastahili pongezi sana. Rais huyu anasifa ya kuwa mwenye kujali, mmeona katika ziara zake anavyojali maisha ya Watanzania na anavyoumizwa na maendeleo ya nchi hii nani Rais kama Magufuli? (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Hakuna. (*Makofi/Vigelegele*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, Rais wetu ni namba moja na anastahili sifa zote kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema Rais huyu amejipambanua kuwa ni Rais mnyenyekevu lakini ni msikivu na mstahimivu. Haya yote unayaona, hasemi mwenyewe matendo yake ndiyo yanajidhihirisha. Ukimkuta Kanisani anadhihirisha hayo matendo yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ni kwa nini amekuwa msikivu na mnyenyekevu, amebezwala na watu ambao yeye ndiyo anawaletea maendeleo. Rais wetu Mwenyezi Mungu akubariki na akuongezee miaka mingi. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nadiriki kwa kumaliza eneo hili la Rais wetu kwa kusema, tumejapata Rais bora mwenye maono ya dhati kabisa, msimamo thabiti, mkweli, anayewajali wananchi wake na aliyekubali kuwa tayari kufia Taifa letu la Tanzania, Mwenyezi Mungu ambariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa fursa na nafasi ya kuweza kutumikia katika Serikali yake na leo tunaingia kwenye bajeti ya tano tukiwa tunamaliza miaka mitano. Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani uliyonipa

mpaka kufika hatua hii ya siku ya leo. Pia nimshukuru sana Makamu wa Rais, mama yetu Mama Samia, kwa kazi nzuri, na hasa kumsaidia Rais wetu. Tumemuona amekuwa msaada mkubwa kwa Rais wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati niungane na Waheshimiwa Wabunge kumshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Kwangu Mheshimiwa Waziri Mkuu alitumia taaluma yake ya ualimu kunifundisha mwalimu mdogo Jenista, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli amejidhihirisha katika kutusaidia kutenda kazi zetu ndani ya Serikali kwa sababu amefanya kazi kwa weledi mkubwa sana.

Naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu; tunakushukuru, tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu kila la heri katika maisha yako yote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, siwezi kuacha kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Angellah, pacha wangu, mdogo wangu, Waziri mwenzangu, lakini nawashukuru sana wadogo zangu, vijana shupavu; Mheshimiwa Antony Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa. Hawa kwa kweli kama ni uteuzi ulipata mahali pake, ni vijana wachapakazi kwelikweli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana washirika wangu katika kazi ya utatu, Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri na tasisi zote zinazosimamia masuala ya kazi. Mambo haya yasingewezekana kama sio Makatibu Wakuu watatu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambao walikuwa ni mhimili mkubwa sana wakiwaongoza watendaji wote, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Taasisi zote ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tumefanya kazi nzuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwaambie Wanaperamiho, nawapenda na nawashukuru sana. Wameendelea kuniamini, naomba waendelee kuniamini, wembe ni uleule na mwaka huu wa 2020 kitaeleweka tu. Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Peramiho. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za dhati katika kipindi hiki cha miaka mitano zimuendee Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, kaka yangu, Mheshimiwa Omari Mchengerwa na Makamu Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa Najma Giga, Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria wamesoma hotuba yao hapa, wameipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya kazi vizuri sana, ni kwa sababu wao walitushauri vizuri, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Dkt. Tisekwa na Kamati nzima ya UKIMWI, tumefanya kazi kubwa sana kwa pamoja, nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Kamati ya Bajeti ikiongozwa na kaka yangu, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki na hasa kwenye Mfuko wa Bunge. Kamati hii iliisaidia kuiambia Serikali mahitaji ya Bunge ili Bunge liweze kutekeleza kazi zake za Kibunge; nawashukuru sana Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, siwezi kumaliza shukrani zangu bila kumtaja Mheshimiwa Mtemi Chenge na ndugu yangu, Mheshimiwa Ngeleja, Kamati ya Sheria Ndogo na Wajumbe wa Kamati hiyo tumefanya nao kazi sana sisi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninawashukuru sana Wajumbe hao wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pia shukrani za dhati kwa Wabunge wote. Kazi hii ya kuwa *Chief Whip* hapa mbele isingewezekana kama Wabunge wote upande wa Upinzani na Chama Tawala wasingenipa ushirikiano. Nawashukuru sana na Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kutoa msisitizo kwamba pongezi zetu na shukrani hizi tunazozitoa zinatoa fursa kwetu sisi kama Serikali kuweza kujifunza mambo mengi, lakini katika kipindi hiki pia tumepata taarifa za misiba, majanga ya mafuriko na vitu mbalimbali ambavyo vimepoteza baadhi ya wenzetu. Nitoe pole kwa Chama cha

CUFkwa kupotelewa na kiongozi wa chama; nitoe pole kwa TBCkwa kumpoteza mtangazaji mahiri aliyesaidia kuihamishia Serikali hapa Dodoma, tunawapa pole sana. Vile vile tunawapa pole na wengine waliokumbwa na majanga ya namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize eneo hilo la kwanza kwa kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tunaingia kwenye Uchaguzi Mkuu, tunapoingia kwenye Uchaguzi Mkuu watu wamekuwa wakitafakari na kuomba uchaguzi huu uwe huru na uwe uchaguzi wa haki. Naomba kuwaomba sana Vyama vyaa Siasa vyote nchini, wadau wa demokrasia na wadau wengine wote, ili uchaguzi huu uishe salama, naomba sana tufuate sheria bila kushurutishwa, tutii kanuni na taratibu na miongozo itakayotolewa na Tume ya Uchaguzi. Kwa kufanya hivyo ndio tutakuwa na uchaguzi huru na uchaguzi wa haki na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 99(2) nitaendelea kujibu hoja kadhaa na zile ambazo sitapata nafasi ya kuzijibu naomba tutazileta kwa maandishi na zitaingia kwenye *Hansard* ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza kutoka Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, kama nilivyosema pale mwanzo walitupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na hasa katika kukusanya maduhuli. Idara moja tu ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa muda mfupi sana waliweza kuvuka lengo la maduhuli ambayo walikuwa wamepangiwa na tukaweza kufikia zaidi ya asilimia 80 kabla mwaka haujaisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge Ofisi ya Waziri Mkuu ni Ofisi Kiongozi, ndio inayotakiwa kuonesha njia. Tutajitahidi kuhakikisha hii *standard* ambayo tuko nayo tunailinda ili tusimwangushe Waziri Mkuu na tusiiangushe Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilizungumzwa sana na Wabunge wa Upinzani, alizungumza sana Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mwakajoka, Mheshimiwa Susan, Mheshimiwa Bungara, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na hii ilikuwa inahusu Tume Huru ya Uchaguzi; hoja hii imezungumzwa sana. Tumekuwa tukijibu hoja hii mara kadhaa hapa Bungeni na tumekuwa tukiendelea kueleza ipasavyo kwamba Tume hii ya Uchaguzi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukienda Ibara ya 74(7) imetamkwa kabisa kwamba taasisi hii ya Tume ya Uchaguzi ni taasisi huru; imetamkwa kabisa. Pia ukienda Ibara ya 11 inaonesha kabisa Tume ya Uchaguzi haitaingiliwa na mtu ye yote, hata vyama vya siasa, katika kufanya maamuzi yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kujua nijambo moja; ninao hapa mfano wa tume hizo ambazo zina jina la tume huru ambazo ziko katika nchi mbalimbali kwenye *regions* ambazo na sisi ni wanachama, lakini tume hizo zote zinazoitwa ni tume huru ni lazima tuijilize misingi yake kwanza ya tume yoyote ya uchaguzi ni ipi ambayo inatakiwa kuangaliwa ili kuweza kuipima tume hiyo?

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa la kwanza ni kuangalia muundo wa tume hiyo. Tume hizo zote zimebekwa kwa mujibu wa Katiba ya kila nchi, hata tume yetu sisi imewekwa kwa mujibu wa Katiba ya Nchi yetu ya Tanzania. Lakini tume hizo zinapimwa kwa utendaji wake katika misingi ya kufuata sheria na kanuni; Tume yetu hii pia imewekwa kwa mujibu wa sheria na inafuata sheria na kuweka utaratibu wa kikanuni wa kuendesha mambo yake; huo ni msingi mwingine.

Mheshimiwa Spika, Tume yetu imeendelea kupimwa kwa mwenendo wake unaokisi weledi wake katika kufanya na kusimamia chaguzi. Hili linapimwa namna gani; tunaipima tume ndani ya nchi lakini viko vyombo vya kimataifa vinaipima Tume yetu ya Uchaguzi kama inafuata weledi na inazingatia sheria. Hao wote wamefanya hiyo kazi na hakuna hata mara moja waangalizi wa kimataifa wamesema Tume

hii sio tume bora na haifai kuendelea kusimamia uchaguzi katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nilisema pale mwanzo; tume hii imeundwa kwa mujibu wa Katiba na tume hizo nyingine zilizopewa majina ya huru zinakuja kujifunza kwenye tume yetu. Sasa nimesema kama imewekwa kwa mujibu wa Katiba ina maana hii ni tume inayowawakilisha Watanzania na imewekwa na Watanzania wenyewe kwa sababu Katiba ni *document* ya Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nimeendelea kujiuliza; ninayo hapa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge la Jamhuri ya Muungano linawekwa na Sura ya Tatu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia, naomba nisome kifungu cha 63(2) kwamba; *63.-(2) Sehemu ya Pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.*

Kwa hiyo sisi hapa Wabunge tuna madaraka kwa niaba ya wananchi, lakini tunatekelezaji majukumu yetu kwa madhumuni ya madaraka hayo tuliyopewa? Kifungu cha 63(3)(a) kinasema tunaweza kutekeleza majukumu yetu kwa niaba ya wananchi kwa kuuliza maswali kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo yako katika wajibu wetu wa kila siku.

Mheshimiwa Spika, mimi ni *Chief Whip* katika Bunge lako hili, nimefanya utafiti mdogo; mpaka hapa tulipofika tumeuliza maswali ya msingi 3,545; tumeuliza maswali ya nyongeza 9,317. Maswali hayo na naomba niendelee kusema nimefanya utafiti mdogo ambao wewe ndio unaweza ukasema vizuri zaidi kwa sababu ni utafiti wa Bunge; Mbunge wa Upinzani ambaye ameongoza kwa kuwa na maswali mengi ya msingi na ya nyongeza ana maswali 52; na Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ambaye ameongoza kwa kuwa

na maswali mengi, huu ni utafiti wangu mdogo, unaweza kufanya zaidi – ana maswali 103.

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia, kati ya maswali hayo yote 9,317 yaliyoulizwa kwa mujibu wa Katiba iliyotupa madaraka ni maswali mangapi yameulizwa kuhusu Tume huru ya Uchaguzi, maswali hayo hayafiki hata asilimia moja ya maswali yote yaliyoulizwa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya hapo nimejiuliza ajenda ya Tume Huru ya Uchaguzi ni agenda ya Watanzania ama ni ajenda ya watu wachache? Kwa hiyo hayo mambo ni lazima tuyaangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeendelea kufuatilia, hotuba zinazosomwa wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu kutoka upande wa Upinzani, nimeendelea kufanya huo utafiti; mwaka 2014 hotuba wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu ndani ya Bunge hili ilibeba hoja ya Katiba Mpya; 2015 hotuba ya Kiongozi wa Upinzani wakati wa Hotuba ya Waziri Mkuu ilibeba ajenda ya Katiba Mpya; mwaka 2016 hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ilibeba hati idhini ya Mawaziri kufanya kazi kutoka kwa Rais; hotuba ya mwaka 2017 ilibeba dhana ya kesi za Wabunge wa Upinzani. Sasa najiuliza hivi kipaumbele cha wale ambao wanasema sasa ni lazima tupambane kwa ajili ya Tume huru ya Uchaguzi badala ya yale ambayo ni matakwa ya wananchi; wananchi wanataka maji, barabara, kilimo, elimu, afya, na hayo tumeyafanya vizuri sana katika kipindi chetu chote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa tuhakikishe kwamba uchaguzi wa mwezi Oktoba, 2020 usibague vyama vya siasa, wote twende tukiwa na haki sawa. Tunapokea ushauri wao lakini tunataka tukumbushe kidogo; vyama vingi vya siasa vilianza toka mwaka 1992 katika Nchi yetu ya Tanzania. Tume ya Uchaguzi hii ambayo ni tume huru kwa mujibu wa Katiba imeanza toka mwaka 1993 ikaanza kusimamia uchaguzi wa mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 wagombea urais katika Uchaguzi Mkuu walikuwa wanne, Vyama vya Upinzani

na Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo tume haikujali nani anagombea ilitekeleza wajibu wake. Wabunge 186 walishinda wa Chama cha Mapinduzi na Wabunge 46 wa Upinzani. Mwaka 2000 wagombea urais walikuwa wanne, mchanganyiko wa vyama, Wabunge walioshinda 202 CCM, 29 Upinzani.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 wagombea urais walikuwa 10, wapinzani tisa CCM mmoja, wote waligombea na Tume hiyo ya Uchaguzi haikujali misingi ya vyama. Wabunge walioshinda walikuwa 206 CCM, 26 walikuwa kutoka Upinzani. 2015 wagombea urais pia walikuwepo, Wabunge walioshinda 195 walikuwa wa Chama cha Mapinduzi, 65 walikuwa wa Upinzani. Hao ni Wabunge kwenye Majimbo.

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo, naomba kuwahakikisha Watanzania uchaguzi huu utasimamiwa vizuri, vyama vyote vitapata haki sawa, vitashiriki ipasavyo, lengo letu liwe moja; kulinda amani na utulivu wa nchi yetu ili uchaguzi uweze kuisha vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu UKIMWI. Kwenye suala la mapambano dhidi ya UKIMWI ilikuwa ni Mfuko wa *ATF*. Tulikuwa tumeulizwa kuhusu fedha za wafadhili, tulilizwa kuhusu masuala ya ukusanyaji wa *data* na uwezo wetu wa ndani katika kukabiliana na tatizo hili la UKIMWI. Tunamshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI, Makamu wake na Wajumbe, walitushauri vizuri sana na sisi tumeanza kutekeleza

Mheshimiwa Spika, kwanza, ili kuifanya *ATF*jitegemee bodi imekamilisha mpango mkakati wa kuhakikisha tunakusanya rasilimali za kutosha za ndani lakini Bodi ya Mfuko huo pia imeshafanya kazi ya kumwajiri *Resource Mobilization Manager* ili aweze kukusanya uwezo wa kuhakikisha Mfuko huu unakuwa na kazi. Tumepata Mshauri Elekezi wa kutusaidia kuhakikisha fedha za mfuko huu zinakusanya. Hata hivyo, tunaishukuru Kamati na tunaendelea na majadiliano kati ya

Kamati na Serikali kuwa na vyanzo vya uhakika vya Mfuko wa UKIMWI Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunawashukuru wafadhili, wameendelea kutoa *commitment* yao. PEPFAR kwa mwaka 2020/2021 wameongeza bajeti ya UKIMWI katika nchi yetu kwa asilimia nane, kwa hiyo tunawashukuru sana. Kwa hiyo tutaendelea kufanya hizo kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumeanza mradi Serikali, TAC AIDS na shirika ambalo linatusaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI nchini la Umoja wa Mataifa UNAIDS, tumeamua kutengeneza mradi wa pamoja wa ku-*train* utaratibu na mfumo mzuri wa ku-*collect data* kutoka katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na UKIMWI. Kwa hiyo tunayafanya kazi hayo yote.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevyaa Nchini. Hoja ya kwanza ilikuwa ni kwa nini hakuna mradi wa maendeleo; tumepokea ushauri huo, lakini kwa kuanzia tumeamua kutumia Fungu 65 kwenye Mradi wa Skills Development kuanza kuwafundisha wale wote wanaoacha kutumia dawa kuwapa mafunzo ya ufundi ili waweze kujajiri. Nadhani jambo hili litawasaidia sana vijana wetu na wataondokana na matumizi ya dawa za kulevyaa.

Mheshimiwa Spika, tuliagizwa tukamilishe maabara ya kitaifa ya kuhakikisha tunakuwa na maabara ya kupima sampuli za dawa za kulevyaa, hasa kesi zinavyotokea na ukamataji. Hiyo maabara tumeanza kuifanyia kazi, vifaa vyote tumekwishanunua, tunachosubiri sasa hivi ni kupata miongozo ya TBA ili jengo letu liweze kutengenezwa vizuri na hayo yote yaweze kufanya.

Mheshimiwa Spika, wametusaidia kutushauri Kituo chetu cha Itega kiwe ni kituo cha kitaifa kitakachokuwa na *combination* ya kazi kuhusu waraibu. Kwa hiyo pale itakuwa ni *medication center*, itakuwa ni *vocation center* lakini itakuwa ni *counseling center*. Tunataka kukigeuza Itega iwe ni *model* ya vituo vyote vitakavyoanza kujengwa katika Nchi

ya Tanzania. Kwa hiyo tunazingatia jambo hilo na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kudhibiti matumizi ya dawa za kulevyta nchini kwa asilimia 90 na sasa hivi bei ya dawa ya kulevyta Tanzania kwa kilo moja imefika Dola za Kimarekani 12,000, lakini kwa nchi nyingine ambazo udhibiti bado haujawa mkubwa bado kilo moja inauzwa kwa 4,000 tu. Kwa hiyo hiyo ni kazi nzuri iliyofanywa na nadhani tuwapigie makofi sana na tuwapongeze wenzetu kwa kazi nzuri waliyofanya.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na hoja za Bunge. Bunge limepewa pongezi sana kwa kazi nzuri uliyoifanya wewe mwenyewe na hasa kuanzisha Bunge Mtandao. Sisi Serikalini tunakushukuru, umeokoa fedha za Kitanzania zisizopungua shillingi billioni mbili kwa makaratasii yaliyokuwa yanazunguka hapa Bungeni. Tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Ofisi za Wabunge, unafahamu kwamba mjadala huu tunao ndani ya Tume ya Huduma za Bunge, kwa hiyo, *inshallah* Mwenyezi Mungu akituridisha, basi jambo hili litazungumzwa ili lipatiwe muafaka ndani ya Tume. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya michezo ya Wabunge kwa mwaka huu wa 2020. Bado tunashawishika kuendelea kutii utaratibu na sheria. Nchi ambayo inakuwa na uchaguzi, haishiriki mashindano hayo. Kwa hiyo, tunaomba mtukubalie tuendelee kuzingatia hiyo sheria na tusishiriki mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na maswali kuhusu *OSHA*, tutaendelea kufanya ukaguzi wa afya na usalama mahali pa kazi. Tumeshatengeneza mfumo wa *work place inspection management*, kaguzi za kisekta na kupunguza tozo ili kuwavutia waajiri wengi wajisajili. Hiyo yote tunafanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maige aliuliza kuhusu *Workers Compensation Fund*kuona ni namna gani tunaweza

kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ya kupunguza tozo kwenye *private sector*. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Maige kwamba tumefanya *actuarial* mwaka 2018, mfuko unaendelea vizuri. Wataalam wametushauri tufanye *actuarial* nyiningine mwaka 2021, matokeo yake sasa ndijo yatupeleke kwenye kubadilisha viwango vya tozo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ushauri mwingine kwamba mifuko ya hifadhi ya jamii iwekeze kwenye miradi ya kimkakati. Tumeshaanza kufanya hivyo. PSSSF muda siyo mrefu watafungua kiwanda kikubwa sana cha bidhaa za ngozi pale Karanga Moshi. Kwa hiyo, ni kazi ambayo tumeamua kujikita nayo. Mfuko wa NSSF umebadilisha matumizi ya nyumba zake kuwa ni *hostel* za vijana wetu wa Vyuo Vikuu na wanafunzi wapatao karibu elfu nane na kitu wamepata nafasi na fursa ya kupata makazi bora katika nyumba za NSSF na tumegeuza mradi huo umekuwa ni mradi wa kimkakati.

Mheshimiwa Spika, tulisikia malalamiko ya Mheshimiwa Goodluck:-

Mheshimiwa Spika, nitaomba tukutane naye ili tujue kule PSSF tunaweza tukafanya nini kuondoa hilo tatizo. Kama Mkurugenzi ananisikia hapa, basi aanze kujipanga ili tuendelee kufanya kazi kwa weledi, tuwasaidie wastaifu wetu wasipate matatizo katika masuala yote ya *pension*.

Mheshimiwa Spika, maswali ni mengi, lakini ninaona kwa muda ambao umenipatia, haya yanaweza kutosha kujibiwa kwa siku hii ya leo, lakini tutaendelea kuyajibu yote kwa maandishi na tutayaleta katika ofisi yako. Ninawahakikishia Wabunge, Serikali imejipanga, Tume ya Uchaguzi itasimamia uchaguzi vizuri na tutakuwa na uchaguzi wenye matokeo ambayo ni halali kwa mshindi na ni halali kwa yule ambaye atakuwa ameshindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote,

ninamshukuru kila mtu kwa kunisikiliza na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi (*Chief Whip*), tunakushukuru sana kwa hotuba nzuri ambayo imepitia maeneo mengi. Tunajua uwanja wako ni mpana zaidi, ila muda hautoshi, lakini tunashukuru kwa kupitia yale maeneo ambayo ni muhimu. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mmekuwa mkichangia leo *almost* ni siku ya nne na uchangiaji wetu umekamilika. Hatua inayofuata ni kumwita mtoa hoja ili sasa aweze kuhitimisha hoja yake kwa kujibu masuala mbalimbali yaliyojitekeza wakati wa mijadala.

Niseme tu kwamba, *microphone* hizi mbili hapo mbele tumekuwa hatuzitumii, lakini nadhani tukiziweka ziwe huru kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ya upande huu na Kiongozi wa Upinzani ya upande huu na mkazitumia ninyi tu, nadhani pia hazina shida. Kwa hiyo, nimwite sasa mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mkuu na nikuombe basi usogee utumie hii *mic* yako hii ili Watanzania wote waweze kukuona vizuri na waweze kufuatilia unachokiongea. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana uhitimishe hoja yako. Ahsante sana. Pia, niwakumbushe kabla Mheshimiwa Waziri Mkuu hajaanza kwamba upigaji kura uendelee. Leo upigaji kura ndiyo mahudhurio ya siku ya leo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. (*Makof*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kusema kwamba sote tunajua wajibu wetu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha pia kukutana hapa kwenye kikao hiki muhimu, Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuhitimisha mjadala wa hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka huu wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninakushukuru sana na Mheshimiwa Naibu Spika kwa pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge, Katibu wa Bunge na timu yako kwa umahiri mkubwa uliouonyesha katika kusimamia mwenendo mzima wa majadiliano yetu ya hoja hii ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Kamati ya Kudumu ya Bunge na Bajeti na Masuala ya UKIMWI kwa michango yao mizuri sana kwenye hoja hii ambayo imetolewa hapa kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu mlionchangia hoja, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala wa Taasisi zote za Serikali pamoja watumishi wote kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kipindi chote cha mjadala wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ingawa niliwahi kuwashukuru Mawaziri ambao nafanya nao kazi, lakini nalazimika pia kurudia tena kuwashukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Nchi ambaye anashughulikia Uwekezaji. Pia ninaye Naibu Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini pamoja na Mheshimiwa Stella Ikupa, Mbunge na Naibu Waziri anayeshughulikia Walemauvu.

Mheshimiwa Spika, bila kuwasahau Makatibu Wakuu ambao wanasmamia na kuratibu shughuli zote za Ofisi ya Waziri Mkuu, Bwana Tixon Nzunda, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu; yuko pia Mama Mwaluko, naye pia ni Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Bwana Massawe ambaye pia tunashirkiana naye vizuri sana akishughulikia eneo la Kazi; bila kuwasahau Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambao pia tunafanya nao kazi kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenu yenye hoja za kuboresha mipango na kazi zilizokusudiwa kutekelezwa na Serikali, hasa katika mwaka wa fedha ujao wa 2020/2021. Mjadala huu umeendelea kuthibitisha uimara na umakini wa Bunge letu katika kutekeleza wajibu wake wa kikatiba, lakini pia kuishauri Serikali na kusimamia vizuri Serikali yetu ili iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia nataka niendelee kutumia nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia na kuipongeza Serikali, pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais; na pia sisi wasaidizi wao ambao tunaendelea kushirikiana nanyi Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Serikali. Nami nataka nitumie nafasi hii kuwahakikisha kwamba salamu hizi nitazifikisha kwa Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais ili waendelee kuchapa kazi yao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya mwisho ya miaka mitano, binafsi napenda kukushukuru wewe binafsi na timu yako ya Bunge. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenu hasa katika kuchangia mambo yote muhimu ambayo tuliyafikisha mbele yenu na kwa kitendo chenu cha kupitisha bajeti zote zilizopita zile nne. Bajeti zote zimefanya kazi yake na nyie wenyewe mmeona matokeo ya bajeti hizo kwa miradi mikubwa na mingi yenye thamani ya kutosha, ambayo pia inaendelea kutumika na wananchi. Ni matumaini yangu kwamba kwa *spirit* hiyo hiyo, basi mtaniunga mkono pia kwenye bajeti hii kwa kuipitisha kwa kishindo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja hii ya Waziri Mkuu imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 80. Kati yao Waheshimiwa Wabunge 62 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa 18 walichangia kwa njia ya maandishi. Nawashukuru sana

Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia hoja ya Waziri Mkuu. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda ninaomba uridhie nisiwataje majina, kwani tayari majina yao yameingia kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejibu hoja nydingi zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge kupitia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri hapa mbele yetu jioni hii. Aidha, kutokana na ufinyu wa muda pia, hoja nyiningine zitajibowi kwa maandishi na kutolewa ufanuzi kwa kina na Waheshimiwa Mawaziri wakati wa kuhitimisha bajeti za kisekta.

Mheshimiwa Spika, kupitia Waheshimiwa Mawaziri, wamejibu karibu maeneo mengi ambayo tumeyakusudia kuyajibu leo hii. Nami ninayo maeneo machache sana ambayo nitayakamilisha ili kuweza kutosheleza mahitaji ya ushauri, maeneo ambayo yanahitaji ufanuzi kwenye mambo muhimu ambayo inabidi yatolewe leo ili yasaidie pia kuongoza katika upitishaji wa bajeti yetu ambayo tunayo leo.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo kubwa ambalo limezungumzwa wakati wa michango yetu ilikuwa ni suala la maafa. Suala la maafa yaliyojadiliwa hasa ni kutokana na uwepo wa mvua nydingi sana msimu huu ambazo zimenesha na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombini mbalimbali zikiwemo barabara, nyumba za wananchi, miundombini ya taasisi zinazotoa huduma za jamii na pia imesababisha vifo. Haya niliyaeleza nilipokuwa nawasilisha hoja yangu siku ya mwanzo na kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba Serikali inaendelea kuchukua za kurejesha hali hiyo, ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini za uharibifu wa miundombini mbalimbali na pia kuainisha mahitaji ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kwamba tutafanya hivyo baada ya msimu wa mvua kukamilika au kwisha ili sasa tathmini ziweze kufanywa na kujuu kiwango halisi cha mahitaji kwenye maeneo hayo yaliyoharibika ili tuweze kufanya urejeshi wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeweka kwenye mipango yake ya utekelezaji wa suala la urejeshaji wa hali ya miundombinu kwa vipindi nya muda mfupi, muda wa katni na muda mrefu kwa kuzingatia mahitaji husika. Aidha, Kamati za Maafa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji zitaendelea kusimamia suala zima la kuzuia, kuijandaa kukabilina na maafa na kurejesha hali pale ambapo wana uwezo napo.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo uwezo umewazidi kiasi, basi, taratibu za kawaida kufika Ofisi ya Waziri Mkuu inayoratibu maafa itaambiwa na yenye we itachukua hatua stahiki ili kushirikiana na Mikoa, Wilaya, Kata, pamoja na Vijiji kwenye maeneo husika. Baada ya tathmini katika kila eneo Wizara za Kisekta zitaendelea kushughulikia athari zilizo jito keza kwa rasilimali zilizopo kwa kuzingatia mipango na bajeti ambayo tumejjipanglia.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutumia nafasi hii kuelekeza Viongozi na Watendaji wote kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya, mpaka Vijiji kusimamia ipasavyo upangaji na utekelezaji wa mipango na matumizi ya ardhi katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na Vijiji. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanatambua maeneo salama kwa ajili ya makazi na shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji, biashara pia na shughuli za uwekezaji ambazo zipo kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusisitiza kuwa Wakala wa Barabara Nchini, *TANROADS* na *TARURA* kuendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara za madaraja na barabara zetu ili kuchukua hatua kwa wakati na hivyo kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kwenye maeneo yetu. Aidha, wananchi wote wachukue tahadhari kwa kuhama sehemu za mabondeni na kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa zinapotolewa na mamlaka hiyo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa zinazotolewa na mamlaka za hali ya hewa, itatusaidia pia kuchukua tahadhari kabla ya maafa haya kutokea. Kwa sasa

tunaendelea kushirikiana na wananchi wa Mkoa wa Pwani, eneo la Wilaya ya Rufiji na Kibiti kuititia Mheshimiwa Mbunge ambaye pia tunaye hapa, Mbunge wa Rufiji, kuona namna ya kuweza kusaidia yale maeneo yaliyopata athari hasa kwenye mafuriko yanayoisha sasa. Tunatambua kuwa mafuriko yamesambaa nchini kote, lakini tutaangalia wapi ambako yamezidi kiasi na athari kubwa zimejitokeza kama vile Rufiji ambako pia kumejitokeza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi kuhakikisha kwamba maeneo haya tunaendelea kuyasimamia vizuri. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuomba Mungu, mvua tunazitaka, lakini pale ambapo kuna madhara yanajitokeza, basi tuendelee kushirikiana kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo napenda nilizungumzie ni lile ambalo Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama amelizungumza. Yeye amezungumzia Tume ya Uchaguzi, mimi nataka nizungumzie uchaguzi wenyewe utakaofanyika mwaka huu mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba mwezi Oktoba mwaka huu nchi yetu itafanya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Hivyo, tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu Mwezi Oktoba, Serikali inatoa wito kwa Viongozi wa Vyama vyta Siasa na wadau wengine wa uchaguzi kuzingatia katiba, sheria, kanuni na miongozo iliyopo katika kuendesha shughuli za uchaguzi katika Mfumo wa Vyama Vingi vyta Siasa.

Mheshimiwa Spika, lengo hapa ni kuhakikisha tu kwamba nchi yetu inaendelea kulinda na kuenzi tunu yetu ya amani, umoja, upendo na mshikamano wa Kitaifa, kama tulivyoachiwa na waasisi wetu wa Taifa hili. Nami nataka niendelee kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba uchaguzi ujao utakuwa wa huru na wa haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano kama ilivyokuwa na watangulizi wake itaendelea kulinda amani hiyo, mshikamano wetu na demokrasia yetu tuliyonayo katika nchi yetu. Kwa hiyo, niwasihi viongozi na wanachama wa vyama vyote vyaa siasa na wananchi kwa ujumla kuendelea kulinda sasa amani ile na kuendeleza mshikamano katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu ili kla mmoja apate haki yake ya kuchagua na kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba mwaka huu wa 2020 yanaendelea vizuri. Hivi sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaijiaandaa na awamu ya pili ya maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura yanayotarajiwa kuanza wakati wowote ule mwezi huu. Baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kufanya majadiliano na wadau, maazimio mengi yamekubalika na yamefikiwa. Sasa ni jukumu la Tume kutekeleza makubaliano yale. Lengo la majadiliano yale ilikuwa ni kuwezesha Tume kujipanga, kupata vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya tahadhari dhidi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu ya *Covid 19*.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza ratiba ya uchaguzi kwa kuzingatia matakwa ya katiba na sheria. Kwa sasa bado ratiba haijatangazwa. Nalisema hili kwa sababu tumeona kwenye mitandao watu wakitamka Ratiba ya Tume ya Uchaguzi. Hiyo iliyotoka kwenye mitandao siyo sahihi. Wananchi wenyewe sifa za kugombea nafasi mbalimbali waendelee kujitokeza, nanyi Waheshimiwa Wabunge mliomo ndani ya Bunge hili, nami naungana nanyi na pia nawaombea sana na ninaendelea kuwaombea muweze kurudi tena baada ya uchaguzi ujao wa mwaka huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo pia ningependa nilizungumzie ambalo limezungumzwa sana na viongozi wetu au Waheshimiwa Wabunge hapa ndani ni homa kali ya mapafu (*Corona*).

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, nami naungana nanyi kueleza kwamba hali ya ugonjwa huu

Duniani ni mbaya na kwamba wote mnakubaliana nami kuwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona umekuwa na athari kubwa kijamii lakini pia na kiuchumi Duniani kote. Aidha, katika kipindi hiki tumeshuhudia changamoto mbalimbali kutokana na hatua zinazochukuliwa na baadhi ya nchi katika kukabiliana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maambukizi ya virusi vya Corona kuingia nchini kwetu na hata kabla ya kuingia nchini, Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli alilitangazia Taifa kuwa ugonjwa huu ni hatari na Watanzania tujiandae na tahadhari kadhaa zilanza kuchukuliwa ndani ya Serikali ili kukabiliana na ugonjwa huu pindi utakapokuja kwa wakati huo. Lakini baada pia ya ugonjwa huu kujitokeza nchini, Serikali pamoja na mambo mengine, tulanza kujipanga vizuri kuanza kukabiliana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza tuliunda Kamati za Kitaifa, moja ya Kamati ya Kitaifa inayoratibu mapambano yote ya virusi vya UKIMWI ikisaidiwa na Kamati ya Makatibu Wakuu na Kamati ya wataalam. Kamati hizi ni za Kitaifa kwamba zinasimamiwa pia na Serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, jukumu mojawapo la Kamati hizo ni kuwezesha nchi kupunguza madhara makubwa ya Kijamii lakini na kiuchumi ambayo yanaweza kusababishwa na ugonjwa huu wa homa kali ya mapafu.

Mheshimiwa Spika, upande wa kijamii tunaendelea kutoa elimu na upande wa kiuchumi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameeleza ameunda timu ya wataalam, wachumi, wanaendelea kufanya mapitio ya athari zinazoweza kujitokeza katika kipindi hiki kufuatia tatizo hili. Tunajua biashara nyingi zimezorota na zinaendelea kuzorota lakini pia shughuli za kiuchumi nyingi nyingine zimeanza kusimama na kwa hiyo lazima tathmini ifanyike hatimaye Serikali itatoa muelekeo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, elimu kuhusu namna ya kujilinda dhidi ya maambukizi ya virusi vya Corona inaendelea kutolewa kote nchini katika sehemu mbalimbali pamoja na kuwahusisha kwa karibu zaidi viongozi wa dini, wadau mbalimbali wa sekta na wataalam wenyewe wa Sekta. Niendelee kusitiza Wizara, Mikoa, Wilaya ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutoa elimu kwa jamii yetu kupitia watendaji wa Serikali walioko kwenye maeneo hayo na wananchi wote wapate kujua nini namna gani wanaweza kujilinda na maambukizi ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia leo tarehe 6 Aprili, tunao wagonjwa 24, mpaka asubuhi ilikuwa wagonjwa 22 lakini baada ya vipimo vya waliochukuliwa vipimo jana na kufikishwa kwenye maabara zetu mchana huu tumepata taarifa kwamba wagonjwa wawilli wameongezeka, mmoja Tanzania Bara na mmoja Zanzibar na kufanya wagonjwa wote kuwa 24. Na hao ndiyo wamethibitika kuwa na ugonjwa huo. Kati ya wagonjwa hao, watatu wamepona na kuruhusiwa kutoka katika hospitali na mmoja amefariki dunia wakati wagonjwa 18 wanaendelea vyema na matibabu.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kitaalam yanaonesha kuwa virusi vya Corona vinaweza kusambaa endapo mtu anagusa majimaji kama mafua, mate na makohozi ya mtu alie na virusi hivyo na kisa kujigusa kwenye mdomo, macho au pua. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imeendelea kuwafuatilia watu wote ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa karibu sana na wagonjwa hao. Hadi sasa watu 685 walikuwa wanafuatiliwa ambapo watu 289 wamemaliza siku 14 za kufuatiliwa na vipimo vyao vimethibitisha kuwa hawana maambukizi ya virusi vya Corona. Watu wengine 396 waliobaki wanaendelea kufuatiliwa ili kujiridhisha kuwa iwapo wana maambukizi ya virusi hivyo basi waweze kujitenga kwa kukaa kwenye maeneo maalum yaliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na maambukizi ya virusi vya Corona ni pamoja na kudhibiti mipaka yetu, kufanya ukaguzi au *screening* kwa

wageni wote wanaoingia nchini kutoka nje pamoja na kuwaweka katika uangalizi wa siku 14 kwenye maeneo maalum. Aidha, ndege za nje zinazoingia nchini zimeshajifuta zenyewe kwa sababu kwenye nchi wanakotoka wamefunga mipaka na kwamba hakuna kuingia wala kutoka kwa ndege.

Mheshimiwa Spika, pia, ndege zetu nazo tumezizua kufanya safari za nje, kwa hiyo ndege zetu sasa zinafanya safari za ndani pekee. Tumezuia wafanyakazi kwenda nje ya nchi, tumeimarisha mipaka, sambamba na kuhakikisha wasafiri wote wanaoingia nchini wanalazimika kuwekwa chini ya uangalizi wa lazima kwa siku 14 kwa lengo la kudhibiti mienendo ya wasafiri nchini chini ya ulinzi kwa masaa 24.

Mheshimiwa Spika, nimetoka kuzungumza leo mchana huu na Wakuu wa Mikoa wote tena, nilizungumza nao wiki iliyopita lakini pia leo nimefanya tathmini ya kazi hiyo inavyoendelea na nimepata taarifa ya kila Mkuu wa Mkoaa namna ambavyo wamechukua jambo hili kwa umakini mkubwa na kila mkoa umeshatenga maeneo haya na hasa kwenye wilaya zilizoko pembezoni kwenye mipaka yetu ambako abiria wengi sasa wanatamani kuingia kuitia barabara. Maeneo yote yameimarishwa, lakini pia tumetenga na maeneo ya kuhifadhi, kuwatenga hawa wote wanaoingia nchini kwa siku 14 na ujumbe huu utakapofika naamini wao hawatakuja tena nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi zote jirani zimefunga mipaka yake, hawaingii wala hawatoki kwa hiyo, *automatically* hatuwezi kupata mtu ye yeyote anayeweza kuja. Hata hivyo, wale wote wanaokuja wanaendelea kuwekewa kwa siku 14 na kufuatiliwa afya zao na tumeimarisha ulinzi wa maeneo hayo ili kuzuia hao walioko kwenye ulinzi huo kutoka au watu wengine kuingia kwa maana ya kuja kufanya mawasiliano na walioko pale ndani.

Mheshimiwa Spika, vilivile kutokana na umuhimu wa kuwatenga watu wanaofuatiwa, Serikali imeagiza mikoa yote nchini kutenga maeneo maalum ambayo leo wametoa taarifa na uangalizi kuimarishe na waimarishaji wote na

wafuatiliaji wa afya zao wote wapatiwe vifaa maalum ili kuendelea kufanya kazi hiyo bila kuwa na athari zozote zile za maambukizi kwao.

Mheshimiwa Spika, hatua hii ni muhimu katika kudhibiti kuenea zaidi kwa maambuzi ya virusi nya Corona na kati ya wagonjwa hawa, walio wengi ni wale waliotoka nje yaani watu wa Mataifa ya nje lakini na Watanzania ambaao walisafiri kwenda nje ya nchi na kuja hapa ndani na maeneo haya yaliyotengwa yatatumika na kila mmoja bila kujali wadhifa wake na nalitamka hili kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza hali iliyoko kule visiwani.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikuwa na Waziri ambaye alitakiwa kwenda kwa matibabu, alikataa baadaye akaenda Mnazi mmoja kwa matibabu na baadaye akatakiwa kwenda kujitenga bado alikataa, lakini Serikali ilichukua hatua na ikamtoa na kumpeleka sehemu ya kutengwa, kwa sasa yuko eneo la kutengwa. Na narudia kutamka hili ya kwamba maeneo haya ya kutengwa yamewekwa kwa madaraja kadri ya uwezo wa anayetengwa. Tumetafuta mabweni ambayo watu wanalala bure, kwa hiyo, asiyekuwa na uwezo wa kulipa atalala huko. Tumetafuta maeneo ambayo yanaweza kulipiwa lakini ya hadhi tofauti tofauti kwa hiyo yeyote anayehitaji kwenda lakini yote yameteuliwa na yanasisimamiwa na sio maeneo mengi, ni machache ili kurahisisha usimamizi na kwa hiyo kila mtu atakwenda eneo hilo kulingana na uwezo wake. Tumetafuta watu ambaao watatoa huduma ya chakula ilia pate chakula kwa gharama ambayo anaweza kuimudu na maeneo haya yana ulinzi kama ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kila mmoja anayetakiwa kujitenga ameenda maeneo ambayo yameandaliiwa rasmi kwa gharama ambazo ye ye anaweza kuzimudu. Tunafanya hili ili kuondoa manung' uniko yaliyokuwa yamejitokeza awali kwamba watu walikuwa wanapelekwa maeneo ya gharama kubwa wakiwa hawana uwezo. Kwa hiyo, tumeimarisha hilo na sasa malalamiko haya yamepungua.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaimarisha maabara mbalimbali nchini ili ziweze kutoa huduma za upimaji ikiwemo maabara zilizopo kwenye mikoa na mikoa hiyo ni kama vile Arusha tunayo maabara inaweza kupima sasa vipimo vyote vya Kanda ya Kaskazini, Dodoma, hapa katikati ya nchi, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani pamoja na Tanga. Maeneo haya yote yana maabara na kwa hiyo itarahisisha kupeleka vipimo kwa umbali mfumo na kupata majibu kwa haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na vipimo vyote ni lazima ithibitishwe na Mganga Mkuu wa Serikali na atakayetoea taarifa ni Waziri wa Afya pekee. Kwa hiyo, natambua mchango wako Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani juu ya watu kutoa Taarifa kiholela, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, kila mmoja anatamka anavyotaka. Tumetoa maelekezo kwamba Taarifa zote za ugonjwa huu zitatolewa na Waziri wa Afya. Kama ni lazima atatoa Waziri Mkuu, kama ni lazima sana, basi atatoa Makamu wa Rais au Rais mwenyewe. Utaratibu huu utasaidia kuleta taarifa za uhakika zilizothibitishwa na watoaji hao ndiyo ambao watahusika. Kwa hiyo, tutalisimamia hili ili tuondoe utamkaji holela wa kila mmoja kadri anavyojisikia.

Mheshimiwa Spika, vipimo hivi pia vinapimwa na hospitali zote za Rufaa, Kanda, za Mikoa nazo zinaratibiwa kutoa huduma za upimaji sambamba na maeneo ya mipakani. Shughuli hizi za upimaji zinafanyika kwa usimamizi wa maabara kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii kwa lengo la kuthibitisha ubora na vipimo hivyo kuratibiwa na utoaji wa matokeo pia nao umeratibiwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia imeendelea kushirikiana kwa karibu na Shirika la Afya Duniani, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika katika kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu na kwa hiyo tunabadilishana mawazo lakini pia tunapeana mbinu mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, yako malalamiko ya baadhi ya Watananzia wakitaka tuchukue hatua ambazo zinachukuliwa na nchi nyingine. Lakini nataka niseme kwamba watu lazima tutambue kwamba nchi hizi zina mazingira tofauti. Tanzania ina mazingira tofauti na nchi nyingine ambazo watu wengi wanazilinganisha na umuhimu ni kwamba Taifa lazima tujipange tuhakikishe kwamba tundhibiti maambukizi kusambaa nchini na hatua tulioiflikia sasa tunafurahi kwa sababu tunaona tunaanza kupata ushirikiano na wananchi, pindi ikionekana kuna mtu ametoka nje ameingia nchini bila kupidia kwenye vituo vyta uhifadhi tunapewa taaarifa na sisi tunachukua hatua za kuwafuata popote walipo na pale ambako kuna mtu ana hisiwa kuwa na tatizo la Corona ili kuitaka Serikali iweze kuthibitisha basi wananchi wanatupigia kwa namba ile 199 na Serikali inachukua hatua ya kuwafuatilia na kuwafanyia vipimo na ikithibitika tunawatenga mahali rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nieleze tu kwamba nchi yetu iko makini na Serikali inafanya kazi hiyo kwa umakini na tutaendelea kuwahusisha pia wadau mbalimbali ambao watasaidia pia kuungana nasi katika kukabiliana na pambano juu ya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na maandalizi kadri ya hali ilivyo kulingana na mazingira tuliyonayo kama ambavyo tumeyaeleza lakini Serikali inaendelea pia kufanya tathmini za kila wakati kuhusu changamoto zinazoweza kusababishwa na ugonjwa huu wa Corona na namna ambavyo tunaweza kuzitatua. Tunajua kuna changamoto za kiafya ambako wananchi wetu wengi wanapata madhara haya. Lakini pia kuna changamoto za kiuchumi ambayo nimeeleza mwanzo na Waziri wa Fedha ameeleza yote haya ni yale ambayo tutaendelea kuyafanyia tathmini. Na tathmini hizi zinafanywa na zile Kamati tatu ambazo tumeziteua. Moja, Kamati ya Kitaifa ambayo inasimamiwa na Waziri Mkuu, ya pili Kamati ya Makatibu Wakuu ambayo inasimamiwa na Makatibu Wakuu Viongozi wa Bara na Visiwani pamoja na Kamati ya Wataalam ambao pia kuna madaktari kutoka pande zote mbili ili kuweza kubadilishana.

Kwa hiyo, kadri tathmini inavyofannywa, tukipata matokeo tunachukua hatua. Hatuwezi kwenda na hatua zote tunaweza tukaleta mkanganyiko ndani ya nchi. Muhimu zaidi ni kujiridhisha kwamba maambukizi haya hayaendelei.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunaendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali na Serikali kushirikiana na wadau wengine imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa huu ili kuweza kumudu kupambana dhidi ya maambukizi. Vilevile Serikali imeendelea kupokea michango ya mtu mmoja mmoja kutoka Taasisi mbalimbali kwa lengo la kuunga mkono mapambano dhidi ya ugonjwa huu. Wiki mbili zilizopita nilipokea misaada kutoka kwa wadau mbalimbali yenyе thamani ya bilioni 1.8 na tarehe 8 wadau kadhaa wamejitokeza kwa hiyo, tutapokea tena misaada hapa Dodoma kwa kila ambaye ameamua kuchangia watakuja watachangia pale Ofisi ya Waziri Mkuu na tutawatangaza rasmi kwa mchango wao na michango hii yote inayochangwa na wadau hawa itatumika kama ambavyo imekusudiwa. Tunaendelea kuratibu kwa kupata vifaa mbalimbali ili kuwezesha watendaji wetu au wataalam wetu kufanya kazi hiyo bila kuwa na madhara wakati wote wanapohudumia ndugu zetu ambao wamepata madhara hayo.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusisitiza kuwa viongozi wa mikoa na wilaya waendelee kusimamia kwa karibu, Kamati za Maafa ziendelee kushirikiana kwa pamoja na madaktari wetu kuhakikisha kwamba wanasaidia kupambana dhidi ya maambukizi haya na kama ambavyo nimewaeleza, nimezungumza na Wakuu wa Mikoa, tumewasitisiza na kuwapata muelekeo wa namna ya kufanya kazi zao kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa suala hili ni mtambuka nitoe wito kwa waajiri, wafanyakazi, wafanyabiashara, wavuvi, wakulima, wasafirishaji na wananchi wote kwa ujumla kuchukua tahadhari zaidi kwani sote tunao wajibu wa kujilinda na kuwalinda wengine ambao wako kwenye mazingira hatarishi. Kadhalika maeneo ya

huduma kama vile masoko, hospitali, vituo vya mabasi na vyombo vya usafiri kuepuwa misongamano isiyokuwa ya lazima na kuchukua tahadhari ikiwemo kutumia vifaa vya kinga. Haya ni mambo ambayo pia tumeyatolea msisitizo na pia tumewaagiza Wakuu wa Mikoa kusimamia, kila mmoja kwenye mkoa wake kupitia wilaya zake na wananchi nao waelimishwe ili waweze kujua njia zote sahihi za kujikinga na maambukizi.

Mheshimiwa Spika, ugonjwa huu hadi sasa umeonesha kutokuwa na dawa na unaleta madhara makubwa Duniani. Hata hivyo, tukiangalia hali ilivyo nchini mwetu hatuna bdi pia kila mmoja kuchukua tahadhari ya kutosha na tunaendelea kuwatahadharisha wananchi wote kwamba ni muhimu kufuata maelekezo ya wataalam wetu, madaktari wetu na maelekezo ambayo tunayatoa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kushukuru sana vyombo vya habari kwa namna ambavyo wanafanya kazi yao katika kuelimisha wananchi wetu. Pia niwashukuru wasanii ambao pia wameanza kutunga hata nyimbo za kufikisha ujumbe wa kuchukua tahadhari huku wakitoa elimu kwa wananchi namna ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona. Lakini pia tuendelee kuzingatia miiko ambayo tumeitoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, fursa ambayo tumeitoa kwenye maeneo machache ni kuwezesha kupata huduma lakini fursa hiyo isitumike vibaya kama vile kuendesha shughuli za kidini, tunataka tu siku za Ijumaa, Jumamosi kwa Sabato na Jumapili kwa wale wanaokwenda kwenye ibada za Jumapili na sio makongamano ya Kidini, hiyo tumezuia. Tunasema watu wakasali na watumie nafasi hiyo kuliombea Taifa. Lakini pia wanapokuwa huko, wazingatie ile miiko yote ya kukaa umbali na tunesema kama nyumba ni ndogo basi wengine wapate nafasi ya kukaa nje kwa nafasi ile ile ili mradi ule muda unaotumika kwa sala au swala utumike huo na watu waondoke waende maeneo yao. Tutaendelea kutathmini hali hiyo kadri siku zinavyokwenda tukiona maeneo hayo

yana madhara makubwa, tutakuja kutamka vinginevyo kwa kushirikiana na viongozi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala la usafiri tulidhani tukiacha watu wasafiri kutoka eneo moja mpaka lingine linaweza kusaidia na tumeelekeza mabasi yote yasijaze abiria, watu wakae kwenye viti, wasafiri wafike, inaweza kutusaidia zaidi na wakiwa kwenye mabasi kila mmoja azingatia. Tumeanza kuona baadhi ya wasafirishaji wanajali na wengine waendelee kujali na kwa kufanya hivyo itatusaidia zaidi kujikinga na maambukizi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ambacho tunaendelea kufanya tathmini ya hali ilivyo, Serikali inasisitiza wananchi kuweka umuhimu wa kufuatilia haya ambayo pia tunahitaji yafanyiwe kazi na watu wote kila mmoja aweze kuzingatia sheria na milango ambayo tumeitoa na tahadhari za kitaalam ambazo pia zimetolewa na watu wetu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapokea hoja, kwenye eneo hili nataka niendelee kuwahakikisha kwamba Serikali itaendelea kupokea ushauri wenu na ushauri huo tutauangalia kwa kupitia Kamati zetu za Tathmini ambazo tatu zimeundwa ili tuweze kuchukua hatua kadri tunavyokwenda. Lakini tunashukuru sana kwa michango yenu na ndio hasa mijadala yetu hapa kwenye awamu hii ilichukua nafasi kubwa. Kila aliyechangia anazungumza suala la Corona na anazungumzia pia suala la mradi.

Kwa hiyo, tumelichukua hili kama jambo muhimu na ni jambo la Kitaifa, lenye madhara ya Kitaifa na tumeona namna ambavyo tumeshirikiana wote bila kujali utofauti wetu kiitikadi, kidini, kisiasa lakini tumeendelea vizuri na sisi tumepokea mawazo yenu tutahakikisha tunayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hii kuwahakikisha Watanzania kwamba Serikali imeendelea kuwa makini nayo na kuchukua tahadhari zote na tunaratibu vizuri. Hoja nyingine ilikuwa ni hoja ilijojadiliwa na baadhi ya Wabunge kuhusu Ofisi ya Msajili wa Vyama Siasa kwamba ihakikishe

inasimamia mwenendo wa vyama vya siasa kwa kuendelea kuchunguza na kufuatilia mienendo ya vyama hivyo ili vizingatie sheria, kanuni, taratibu na weledi kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili Serikali imepokea ushauri wa Kamati lakini pia Waheshimiwa Wabunge. Serikali inaahidi kuufanya kazi kwa kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kusimamia utekelezaji wa sheria ili kuhakikisha kwamba vyama vyote vya siasa vinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba, sheria na kanuni zilizokubalika kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia mwaka huu 2019/2020, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilichunguza na kuvitaka baadhi ya vyama vya siasa viliviyotuhumiwa kuvunja sheria kufuata utaratibu. Maelekezo ya msingi yallitolewa na Msajili, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba maelekezo yale yatazingatiwa. Katika kuhakikisha kwamba vyama vya siasa vinakidhi na kutekeleza matakwa ya sheria zinazosimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ofisi inaendelea kufanya uhakiki wa vyama vya siasa kuhusu utekelezaji wa masharti hayo na matakwa mengine ya kisheria ili vyama hivyo viweze kufuata sheria hiyo ikiwemo na Sheria ya Gharama za Uchaguzi hasa kipindi hiki tukielekea kwenye chaguzi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni ile inayosema Serikali iangalie upya taratibu za utoaji wa vibali vya kazi na ukaazi kwa wataalam kutoka nje ikiwemo kuzingatia wataalam ambao hawana elimu rasmi lakini wana ujuzi katika sekta kama vile ukataji wa vito sambamba na kupunguza għarama za vibali vya kazi ili kuvutia wawekezaji. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde ameitolea ufanuzi hoja hii lakini naomba niseme machache juu ya hili kwamba utoaji wa vibali vya kazi kwa raia wa kigeni unazingatia matakwa ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008. Sera hiyo inabainisha kuwa ajira za wataalam wa kigeni hulenga zaidi katika kuziba pengo la ujuzi adimu na teknolojia. Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kuzingatia vigezo muhimu vyenye kuhusisha elimu, ujuzi na

uzoefu wa kazi husika katika utoaji wa vibali nya kazi kwa wageni ambao wanaingia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama za vibali nya kazi, Serikali inaendelea na kukusanya maoni kwa lengo la kuifanyia mapitio sheria husika ambapo masuala ya ada pia yanaweza kuangaliwa. Hata hivyo, changamoto kubwa kwa wawekezaji si kiwango cha ada bali ni muda mrefu ambao umekuwa ukitumika kuomba kibali hicho hadi kutolewa. Tumefanya maboresho ili pia vinapoombwa vibali hivi viweze kutolewa kwa muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya utoaji vibali nya kazi ili kurahisisha utoaji wa vibali hivyo kwa kipindi kifupi sana. Hivi sasa kazi ya kuweka miundombinu stahiki inaendelea na utaratibu wa kuzindua mfumo huo utafanya siku za karibuni ili mfumo huo uanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ilikuwa ni Serikali iboreshe miradi ya umwagiliaji pamoja na miundombinu yake ili kuongeza uzalishaji wa chakula hapa nchini. Ni kweli kwamba nchi yetu tunategemea sana mvua badala ya kuimarisha umwagiliaji katika kilimo na kwa maana hiyo mwaka ambako hakutakuwa na mvua nchi yetu inaweza kuingia kwenye baa la njaa. Serikali inatambua tulikuwa na Taasisi ya Umwagiliaji ambapo awali ilikuwa chini ya Wizara ya Maji. Hatua ya kwanza tumeiondoa kutoka Wizara ya Maji tumeipeleka Wizara ya Kilimo, Wizara ambayo inahusika na suala la kilimo ili iweze kuiratibu kwa ukaribu. Bado Tume ipo na inaendelea kufanya kazi yake, tumefanya mabadiliko kadhaa ndani ya Wizara ya Kilimo ikiwemo na kuondoa Wakurugenzi saba ambao awali walikuwa wanaratibu kutokana na matatizo mbalimbali yaliyojitokeza kwenye Tume hiyo na sasa tumeunda timu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumefanya maboresho ya ufunguzi wa ofisi zake ambapo awali ilikuwa ipo Makao Makuu peke yake na kwenye Kanda. Sasa tumefungua ofisi za mikoa 26 ambazo zitakuwa na Maafisa wa Umwagiliaji

Iakini tumepeleka Maafisa Umwagiliaji 34 kwenye ngazi za Wilaya na kwenye Wilaya ambazo zina miradi ya umwagiliaji na wanaendelea kufanya kazi yao ili waratibu kwa ukaribu miradi hiyo chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya wakishirikiana na Afisa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuhakikisha kila mradi wa umwagiliaji uliopo katika Halmashauri, unapata msimamizi mtaalam ambaye ni kutoka Tume ya Umwagiliaji. Tayari wataalam wa umwagiliaji wamenza kupelekwa maeneo yote na kazi zimeanza. Hatua hizo zinalenga kuiwezesha Tume hiyo kusimamia ipasavyo shughuli za umwagiliaji nchini ili kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 475,056 za sasa hadi hekta 1,000,000. Malengo yetu ifikapo mwaka 2025 tuwe tumefikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, nikwi nahitimisha hoja yangu, hayo ndiyo machache ambayo yamejitekeza, yapo mengine machache kama vile eneo la ushirika ambalo lilichangiwa na Mheshimiwa Mbunge kutoka Mkoa wa Kagera alipokuwa anaonesha kutoridhishwa na ushirika uliopo Mkoani Kagera. Nikiri kwamba ushirika huu toka awali haukuwa na mwelekeo mzuri. Ushirika baadaye iligeuka na kuwa ni maeneo ya watu wanaopata nafasi ya kuongoza kuwa ni maeneo ya kula.

Mheshimiwa Spika, tulichofanya ni kufanya mapitio ya ushirika huo na kufanya maboresho lakini pia kufanya uhakiki wa kina katika kila ushirika kuona ushirika ulikuwa na nini na maboresho yake na hatimaye kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa ushirika. Kwa sasa, baada ya uhakiki wa maeneo yote ya Vyama Vikuu vya Ushirika na kubaini kwamba kulikuwa na ubadhifuru mkubwa ikiwemo na *WETCO* -Mkoani Tabora, NCU - Mkoani Mwanza, *KNCU* - Mkoani Kilimanjaro lakini pia *KBCU* ya kule Kagera.

Mheshimiwa Spika, pia hapa karibuni tumeenda kwenye mkonge; maeneo hayo tumefanya uhakiki na kugundua kwamba zipo mali nyingi za ushirika zimetoweka au zimechukuliwa na watu bila utaratibu na kukatisha tamaa wakulima kuijunga kwenye ushirika huo. Baada ya hatua hii,

tumeanza kusimamia ushirika huu kurudi kwenye nafasi yake. Kwa hiyo, tumeendelea kuboresha ushirika huo ikiwemo na kusimamia Tume ya Ushirika ambayo inaratibu ushirika.

Mheshimiwa Spika, upo ushirika kwenye maeneo mengi; upo ushirika kwenye mazao ya kilimo ambapo pia kuna Vyama Vikuu vya Ushirika vya Mazao ya Kilimo lakini kuna ushirika wa fedha ambao unasimamiwa na taasisi za fedha, wote upo chini ya Tume ya Ushirika. Kwa sasa tupo kwenye mjadala na wadau wa kuiondoa Tume ya Ushirika kutoka Wizara ya Kilimo ikae ama Ofisi ya Waziri Mkuu au Ofisi ya Rais ili iweze kufanya kazi ya kusimamia ushirika wote ulipo katika Wizara zote ikiwemo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha na maeneo mengine na kupata mafanikio makubwa zaidi badala ya kuweka kwenye Ushirika tukiwa tunajua kuna wana ushirika waliojiwekea fedha za akiba na kukopa kwenye sekta ya fedha. Hayo ni malengo ya kuboresha ushirika kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, sasa ushirika wa mazao ambao tulioupata hapa ni kwamba kazi yao wao ni kusimamia biashara ya mazao lakini pia ushirika huu unatakiwa usimamie kuanzia maandalizi ya kilimo mpaka masoko yake. Kasoro zote zilizojitokeza zinaendelea kurekebishwa ili ushirika huu uwe na tija kwa wakulima na tumeanza kuona manufaa kwenye maeneo mengi ambayo ushirika huu unaanza kusimamiwa, masoko ya mazao mengi yaanza kufikiwa vizuri pamoja na kasoro hizo lakini tunaendelea kuimarisha. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao pia ni Wajumbe wa Ushirika kwenye maeneo yenu au mnao wana ushirika wenye malalamiko kwenye maeneo yenu, endeleeni kuwa na matumaini kwamba mwisho wa zoezi la kuimarisha ushirika huu, tutakuwa na ushirika ambao utakuwa unaringiwa na wakulima wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna sekta ya ajira ambayo ilizungumzwa vizuri kwenye hoja yangu nilipokuwa nawasilisha. Naomba tu nifanye marejeo ni kwamba Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa anaingia madarakani moja ya kilio cha Watanzania ilikuwa

ni kukosekana kwa ajira. Alipokuja na kauli mbiu ya kuboresha uchumi kuititia viwanda; moja kati ya mkakati ni kufungua milango ya ajira kwenye viwanda vingi vinavyojengwa. Leo hii tunashuhudia viwanda vingi vinavyojengwa nchini vinatoa nafasi za ajira za Watanzania bila kujali elimu. Wapo wanaoajiriwa wasiokuwa na elimu kabisa, elimu ya kati mpaka elimu ya juu na ndiyo malengo yaliyokuwepo ya uanzishwaji wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia ajira tumeifungua kwa kuanzisha miradi mingi ya kimkakati. Miradi yote ya kimkakati imetengeneza ajira kwa kuajiri vijana wanaosaidia kufanya kazi lakini wataalam, bado kuna wajasiriamali, wafanyabiashara na wenyewe makampuni wamepata ajira kuititia miradi hii mikubwa. Hata ile ya ujenzi wa vituo vya afya, hospitali, miradi ya maji nayo pia imetengeneza fursa za ajira kwa wale ambao wapo kwenye maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la ajira ni pana na ni endelevu kama nilivyosema wakati nawasilisha hoja. Hata hivyo, tunachofanya pia, tumeweka programu ya kuwapa ujuzi Watanzania wasiokuwa na ujuzi ili waweze kuajirika kwenye sekta mbalimbali lakini pia waweze kujajiri kwa kutumia ufundi walionao.

Mheshimiwa Spika, pia tumetoa fursa za Ofisi za Serikali kushiriki kikamilifu katika kuboresha ajira hizi kwa kutengeneza mifumo itakayowapatia mtaji vijana au makundi mbalimbali ili nao pia waweze kujajiri kwa kuanzisha biashara mbalimbali au miradi mbalimbali ambayo itaweza kuwapatia vipato. Katika kuhakikisha tunahamasisha eneo la ajira, tumetoa fursa kwa kuzungumza na taasisi za fedha kutoa mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali ili wawe na mitaji ya kuanzisha biashara zao ikiwa ni sehemu mojawapo la ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo la ajira ni sehemu ya ajenda yetu, ni eneo endelevu na tunaendelea kuweka mikakati kadiri siku zinavyokwenda kuhakikisha kwamba tunawatoa vijana wengi kwenye maeneo ya kukaa na

kucheza *pool* bila sababu kwa kukosa ajira na kila mmoja ashiriki kwenye maeneo haya. Leo hii tumeanza kushuhudia vijana wengi nchini wameachana na kucheza *pool*, kila mmoja anafanya kazi yake na kauli mbiu ya "Hapa Kazi Tu" imesaidia kuwafanya vijana hawa kushiriki kikamilifu kwenye shughuli mbalimbali za ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa nahitimisha naomba nieleze suala la ziara za Viongozi wa Kitaifa ambazo zimefanyika nchini kote kwamba Serikali yetu tuliweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunawafikia wananchi. Tulikuwa tunaweka msisitizo wa kila mtumishi wa Serikali lazima ajenge tabia ya kuwapokea, kuwasikiliza na kuwashudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano iliweka juhudzi za kipekee za kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya umma kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika kuwashudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hado Februari, 2020, ziara mbalimbali zimefanyika zikihusisha viongozi wa Kitaifa, Mawaziri katika maeneo mbalimbali Tanzania Bara lakini pia hata Visiwani. Lengo la ziara hizo zilikuwa ni kukagua miradi ya maendeleo na shughuli mbalimbali za kiuchumi na jamii; kuzungumza na watumishi wa umma; kusikiliza malalamiko na kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali kwa viongozi na watendaji husika ili waendelee kuwashudumia Watanzania kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ziara hizi zimeleta tija sana kama ifuatavyo. Moja, tumeongeza pia hata nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma katika ngazi mbalimbali. Watumishi wameongeza ari ya kuwatumikia wananchi, kusikiliza malalamiko, kero na kutoa ufanuzi lakini kubwa zaidi kuwashudumia wananchi bila ya urasimu. Hili litaendelea kusimamiwa wakati wote ili kujenga nidhamu ya utendaji ndani ya nchi, hasa ndani ya Serikali ya kuwashudumia Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mbili, tumeongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya huduma za jamii ikiwemo miradi ya elimu, afya, maji pamoja na miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na umeme. Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi kwamba Serikali yetu imeyafanya haya na tunaendelea kufanya haya ili kuleta ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, tatu, tumeongeza kwa kasi ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kuu na mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na uhimizaji wa matumizi ya mashine za kielektroniki pamoja na mwitikio wa wafanyabiashara, wafanyakazi na wananchi kulipa kodi na ushuru kwa hiyari bila shuruti. Naona sasa Watanzania wengi wanapenda kulipa kodi kwa sababu kodi ile inaratibiwa vizuri na inarudi kwao kwa kuwajengea miradi. Kwa hiyo, ari imeongezeka na tunaamini ari itazidi kuongezeka ya kila mmoja kujua kwamba wajibu wake ni kulipa kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna ongezeko la uzalishaji na tija ya mazao mbalimbali ya kilimo cha biashara na chakula katika maeneo mengi. Pia sekta ya mifugo na uvuvi imepata mabadiliko makubwa. Vilevile na tunaendelea kuwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula na kuongeza mapato ya kuchochea maendeleo ya viwanda. Pia tunaendelea kuimarika kwa hali ya usalama, amani na utulivu nchini pamoja na kuongezeka kwa kasi ya mshikamano ndani ya Taifa ili pia tuweze kufanya kazi hiyo kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, najua tuna kazi kubwa ya kuititia bajeti yetu na mimi naomba nihitimishe kwa kusema kuwa sote tumekuwa tukifua tililia kwa karibu mjadala huu kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu. Aidha, wakati wa kuwasilisha hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nilitumia nafasi hiyo kueleza kirefu mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi cha takribani miaka hii minne na tunaingia sasa wa tano. Hivyo, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kote nchini kwa ujumla kuwa llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 imetekerezeka vema chini ya Jemedari wetu, Rais wetu

mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Naomba tu niendelee kwa kusema kuwa tutaendelea kuwahudumia Watanzania na Watanzania waendelee kuiamini Serikali yetu, Rais wetu na wasaidizi wa Mheshimiwa Rais kuwa tupo kwa ajili yao na tutaendelea kuwatumikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwezi huu wa Aprili una matukio makubwa kidogo. Moja tarehe 7 Aprili, 2020 yaani kesho tutaadhimisha miaka 48 ya Kumbukumbu ya Kifo cha Hayati Mzee wetu Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa kwanza wa Zanzibar. Pia tarehe 12 Aprili, 2020 tutaadhimisha miaka 36 ya Kumbukumbu ya Kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Hayati Edward Moringe Sokoine.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Watanzania tuendelee kuwakumbuka viongozi hawa. Kesho itakuwa ni siku ya dua maalum kwa ajili ya kumuombea baba yetu Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Kwa hiyo, kila mmoja kwa dhehebu lake atumie nafasi hiyo kumuombea Mzee wetu Rais wa kwanza wa Zanzibar. Pia itakapofika tarehe 12 Aprili, 2020, nako pia familia inaandaa dua. Kwa hiyo, kila mmoja kwa dhehebu na imani yake aendelee kumuombea aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine na tuendelee kumuomba Mungu aendelee kuweka roho zao mahali pema peponi, Amina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Mawaziri, viongozi wateule wa Serikali na watendaji wote kutekeleza wajibu wetu ipasavyo. Tufanye kazi kwa bidii zaidi, tuache mazoea, tuchape kazi kwa lengo la kuwa hudumia wananchi wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wakristo wote duniani wataendelea na kipindi cha toba ambacho ni muhimu katika imani kuelekea sikukuu ya Pasaka. Niwasihii kuwa maisha mnayoishi katika kipindi hiki yalingane na maisha yetu ya kila siku. Kadhalika kuelekea kumalizika kwa kipindi hiki, niwatakie Watanzania wote kheri ya Pasaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwezi huu pia tuna Mfundo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani nao unatarajiwa kuanza wakati wowote ule kuanzia katikati ya mwezi huu. Napenda kutumia fursa hii pia kuwatakitia Waislamu wote nchini mfungo mwema na wenyewe mafanikio ili kila atakayefanya ibada hiyo, aifanye kikamilifu na kama inavyoagizwa katika mafundisho ya Quraan Tukufu basi naamini kila mmoja takuwa anafuata imani hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha Makadirio ya mapato na matumizi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge letu kama ilivyowasilishwa katika hoja yangu siku ya tarehe 1 Aprili, 2020.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwa utamaduni uleule na tabia ileile ya ushirikiano wa dhati na kwamba kama ambavyo mmekuwa mkipitisha bajeti zote nne zilizopita, naamini pia pamoja na bajeti hii ya tano inayolenga kuhudumia Watanzania wote, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtaniunga mkono kwa kuipitisha kwa kishindo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono kweli kweli, asanteni sana. Tumeshuhudia hoja ikiungwa mkono hasa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana, tunakushukuru sana kwa kupitia masuala mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameyaongea kwa siku karibu nne mfululizo kupitia hoja uliyoitao hapo kabla ukisaidiana na Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Waheshimiwa Manaibu Waziri, Mawaziri wengine na ulipohitimisha wewe mwenyewe. Sisi kama Wabunge

tunaridhika sana na maelezo ya kutosha ambayo Serikali imeyatoa. (*Makofî*)

Sasa meza yangu haina mambo ya sera yale. Kwa hiyo, naendelea sasa kwamba tunahitaji uamuzi wa Bunge kuhusu kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Wabunge waliopiga kura ni wengi, mahudhurio ni mengi kabisa, ninayo yote ya ndiyo na kadhalika na wale wa *abstain* pia.

Kwa kuwa utaratibu wetu siyo wa kutaja nani amefanya nini, majina yote ninayo na ni siri yangu na kura zote ninazo hapa. Baada ya kuzijumlisha na kuziweka sawa, waliosema ndiyo wameshinda (*Makofî/Vigelegele*)

Kwa kweli mahudhurio ya Waheshimiwa Wabunge ni mazuri mno kwa wale tulioko humu na wenzetu walioko katika kumbi mbalimbali. Ni Bunge ambalo katika miaka yote hii minne ni *record* kupata idadi za Wabunge kubwa kiasi hiki. Napenda kuwatia moyo Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuwa tunahudhuria vizuri namna hii.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 – Ofisi ya Waziri Mkuu yalipitishwa na BUnge kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.....	Sh. 4,195,076,000
Fungu 25 – Waziri Mkuu.....	Sh. 8,843,563,000
Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa.....	Sh. 24,751,706,000
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu.....	Sh. 19,145,347,000
Fungu 42 – Mfuko wa Bunge.....	Sh. 113,567,647,000
Fungu 61 – Tume ya Uchaguzi.....	Sh. 5,994,805,000
Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu.....	Sh. 13,676,606,000
Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyा.....	Sh. 9,033,345,000
Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.....	Sh. 2,788,708,000

MPANGO WA MAENDELEO

Fungu 27 – Msajili wa Vyama vya Siasa.....Sh. 2,000,000,000
Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu.....Sh. 27,214,000,000
Fungu 42 – Mfuko wa Bunge.....Sh. 8,218,610,000
Fungu 61 – Tume ya Uchaguzi.....Sh. 180,000,000,000
Fungu 65 – Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira
na Walemaavu.....Sh. 10,258,625,000
Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI
Tanzania.....Sh. 4,900,739,000

SPIKA: Basi, na mimi nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushirikiano mkubwa sana ambaao ametupatia miaka yote hii hadi sasa. Tutasema zaidi tutakapofika mwisho wa Mkutano huu. Itoshe kusema, mimi mwenyewe kama Spika, Ofisi ya Bunge kwa ujumla, wewe kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, umetupa ushirikiano wa hali ya juu kabisa. Kila tulipohitaji ushirikiano wa jambo fulani, usaidizi wa jambo fulani toka Serikalini Mheshimiwa Waziri Mkuu hakusita kutufungulia mlango. Tunakushukuru sana sana, sana na tunaomba uendelee hivyo kwa kipindi hiki na tunakuombea huko mbele. (*Makofi*)

Niwaambie wananchi wa Ruangwa kwamba heshima ambayo mmepewa kwa Mbunge wenu kuwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ni heshima kubwa sana. Mtu ye yote huko Ruangwa kuchukua fomu eti anagombea, kwa kweli demokrasia nyingine nazo, kuna kitu kinaitwa aibu, lazima watu waone aibu. Kwa sababu hajawatumikia Ruangwa peke yake, amekwenda kila mahali, mpaka Kongwa amefika na kwenye Wilaya mbalimbali za nchi hii, ametutumikia Watanzania wote. Kama sisi wote tumeweza tiki, sasa ninyi wa Ruangwa mnapaswa kukienzi zaidi chema chenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuombea afya njema na kwa kweli umemsaidia sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ana kazi kubwa, ngumu lakini umemsaidia sana na tunaomba uendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nawashukuru pia Mawaziri wa Nchi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Maofisa wengine wote Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kuifanya, mwendelee hivyo hivyo na mboreshe zaidi.

Baada ya hayo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameellezea kwamba kesho ni Sikukuu, *Karume Day*. Naendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kadri mnavyoweza ni vyema mkabakia Dodoma; kusafirisafiri nyakati hizi ambazo tunaambiwa *Corona is real* siyo vizuri sana *ku-risk risk* hivi. Nyakati hizi siyo nyakati za mabadiliko. Kwa hiyo, anayeweza ni vyema akabakia kuliko kusafiri; na kama kuna watu muhimu maeneo huko, basi ni vyema wakaja Dodoma. (*Kicheko*)

Pia wakati wa Pasaka, wengine hawajawahi kula Pasaka Dodoma hapa, basi ni vizuri kujaribu kutumia Pasaka Dodoma. Najua mnahitaji kuwa karibu na wapiga kura lakini ni vizuri kuchukua tahadhari ili uchaguzi wa mwezi Oktoba mwaka huu tuweze kuuona ukienda salama, kwa sababu lazima tujikinge na *Corona* na basi tujaribu kuwasiliana na wapiga kura wetu kwa njia za kisasa kadiri iwezekanavyo.

Mwisho kabisa, Waheshimiwa Wabunge jana kama siyo juzi, nilikuwa naangalia mitandao kidogo, kulikuwepo na chombo kimoja kinamhoji ndugu yetu Bwana Tundu Lissu akawa anasema Spika ni muongo kutokana na yale ya majuzi ambayo nilishauri kwamba siyo vizuri sana kuweka mambo ya watu binafsi katika hotuba rasmi hasa kuhusiana na madai ambayo siyo kweli. Kwa hiyo, akasema Spika ni muongo. Nami nataka kumhakikishia tena; na hivi vyombo vyaa habari, Waandishi, siyo kila jambo analosema kila mtu mnalichukua kama ni jambo la maana; na hasa akiongea Spika ni vizuri kuwa na umakini kidogo.

Mheshimiwa Lissu anapenda sana mambo yake kujadiliwa kwenye *public*; mimi binafsi huwa nimekataa kwa muda mrefu sana, huwa sipendi, hujizua sana. Huwa nasema tu kwa sababu nimeshachokozwa na jambo fulani, vinginevyo siwezi kutangulia kusema jambo lolote kwa ndugu

yetu huyu. Sasa mtu akikulazimisha, ufanyeje? Kwa hiyo nina kila kitu hapa, nataka kumthibitishia tena na kuwathibitishieni mnaopenda kuandika habari za huyu bwana.

Posho zake zote amelipwa mpaka hiyo ya Juni, 2019 aliyokuwa anadai kwamba hajalipwa amelipwa. Sasa kama wewe mwenyewe kimahesabu unakanganyikiwa huko, usisingizie wenzako. Nasi tumesoma hesabu vizuri. Kwa hiyo, kutokua makini kusisababishe *everybody* akawa anahuksika na suala la kufanua jambo linalokuhusu wewe mtu mmoja.

Nanyi Wabunge mko hapa kwa mamia yenu, hivi nani hakuwahi kupata mshahara? Kama hukupata ni bahati mbaya fulani, ni jambo la kurekebisha dogo tu. Kwa nini yeye asipate? Kwa hiyo, mishahara yote tangu ameanza hapa iko. Sipendi sana kutaja *figures* lakini hebu afafanue, hizi zaidi ya shilingi milioni 200 ambazo tumemlipa kwenye mishahara peke yake, zilikuwa za nini? Kwa hiyo, anadai wapi? Sitaki kutaja *figure* mpaka ya mwisho.

Wakati mwingine mtu uwe na shukrani duniani hapa. Posho mbalimbali ni zaidi ya shilingi milioni 360; zilikuwa zinapita wapi kama siyo kwa Ndugai huyu huyu unayemtuhumu kwenye vyombo huko? Zilikuwa za nini? Hebu achanganue, atoke sasa!

Kwa ujumla katika kipindi ambacho amekuwepo hapa, amelipwa zaidi ya shilingi milioni 500 na zaidi, sitaki kutaja *figure*, lakini akitaka twende, nitazidi kufunguka zaidi. Pia akumbuke ana mikopo ambayo amechukua maeneo mbalimbali na yenye sitataja sana, lakini *data* zote ziko hapa. Ila kwa sababu hii ni mikopo, nimkumbushe huko Ubelgiji anakokaa, kuna hela anadaiwa hapa zaidi ya shilingi milioni 70 za kuititia kwenye Bunge hapa alizokopa kwenye mikopo mbalimbali. Kwa hiyo, anapomtuhumu Ndugai hapa, akumbuke na huku nako awe analeta hela, arudishe kwanza ili zilipe mikopo mbalimbali ambayo iko katika maeneo mbalimbali.

Syo vyema sana kupenda kuweka mambo ya mtu hadharani, syo utamaduni wetu, lakini mnapoweka kwenye hotuba za kambi, naye mwenyewe anapotokeza katika mitandao kudai mambo ambayo hayana kichwa na mguu, inakuwa haipendezi. Kwa hiyo, natumaini jambo hili litafikia mwisho.

Kwa Waheshimiwa Wabunge wote, hesabu zote za unadai nini na unafanya nini, *bytarehe* 30 mwezi wa Sita kila mtu hesabu yake itakuwa imekaa vizuri na hakuna atakayekuwa anadai shilingi *bytarehe* 30 mwezi wa Sita. Hiyo *ina-include* mtu yejote aliyeko Mahakamani, aliyeko wapi ambaye inabidi hesabu yake isifungwe kwanza vizuri kwa sababu ya michakato fulani fulani. Ila kwa wakati huo ina maana mpaka yale malipo yanayoitwaga *gratuity*yote yale yatakuwa yamekamilika.

Walio wengi kama wana hela, ni kidogo sana, kwa sababu mimi ndiyo nina... (*Kicheko*)

Eeh, ndiyo ukweli wenyewe. Madeni ni mengi sana. Huo ndiyo ukweli. Ni vizuri kila mmoja wetu akapiga hesabu yake vizuri, pamoja na madai uliyonayo, lakini na madeni, tukumbuke kulipa kwa sababu sisi ni viongozi. Kuwa na madeni makubwa ni pamoja na kukosa sifa ya kuwa kiongozi; kuwa na madeni ambayo hayalipiki wala huonyeshi, yaani mapato yako na matumizi havi-*balance* kabisa.

Kwa hiyo, syo tunaangalia tu bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mpango peke yake na kuikosoa; maana kuna mwingine akisimama hapa, ee Waziri Mpango, mbona bajeti ya ovyo! Sasa nami naangalia mafaili yangu, huyu naye mbona bajeti yake yeye mwenyewe imemshinda tena kwa mbali! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Tundu Lissu akumbuke kuna pesa ambazo tumekuwa tukimlipa hapa, pamoja na Wabunge wengine kama tunavyowalipa, zinahusu kuwalipa madereva. Sasa sisi tukianza kuchimba ni dereva yupi ulikuwa unamlipa? Lini? Kukuendesha kwenda wapi? Mafuta ya Jimbo; Jimbo

lipi ulilokuwa unalipwa wewe fedha hizi, wakati kuna ushahidi wa kila aina kwamba uko Ubelgiji? Posho za Jimboni zile za kutembelea wapiga kura; uliwatembelea lini? Kwa utaratibu upi?

Wanasema ukijua vyatia mbele na wenzako nao wanajua vyatia nyuma. Kwa hiyo, unaweza ukajikuta wewe huyo huyo uko kwenye matatizo mengine ya kutakiwa kurudisha tena mamilioni ya fedha za wapiga kura. Kwa hiyo, ukiona wenzako wamenyamaza, wametulia na wewe nyamaza, angalia habari ya *Corona* huko. Huko tena ndiyo kuna balaa la *Corona* huko. Tulia! Mitaa ya huko iko myeupe, watu wanashinda ndani, wewe angalia mambo ya huko.

Ukitaka kurudi nyumbani, njoo; matangazo tunasema kila siku, Oktoba hapa ndiyo ngoma yenye inachezwa. Karibu sana nyumbani. Haya mambo mengine, nashauri sana, hata ninyi wenzake msibebi sana hivi vitu, tuongee mambo mengine. Hivi habari ya mtu mmoja mmoja ana jambo lake ambalo *after all* siyo kweli; na kama ni kweli, basi ni kupita ofisini na kujaribu kuona kama kuna kitu cha kufuatilia kinachomhusu.

Hatuko hapa kumwonea mtu ye yole yule kuhusu kitu ambacho ni haki yake. Hilo jambo hatutafanya. Dhambi hiyo hatuwezi kuibeba hata siku moja hata iwe inamhusu nani. Mimi kama Spika wenu nitahakikisha haki ya kila mmoja wenu. Kama nilivyosema, *by tarehe 30 Juni, inshaallah*, Mwenyezi Mungu akituweka hai sote hakuna atakayekuwa anazungumza habari ya ooh, sikupata, nilipata na kadhalika. Itakuwa ni madeni tu na kusawazisha mambo mengine.

Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote amba mna madeni mbalimbali, *including* madeni miongoni mwenu kulipa. Eeh! Tuna faili la watu wamekopa bila aibu, utafikiri siyo viongozi, kwa wapiga kura wao, kwa nani, kwenye mabenki, kwenye SACCOS, kwa mtu mmoja mmoja; hatuwezi kwenda namna hiyo kama viongozi. Ni lazima turekebishe hii tabia ya kuchukua hela za watu na kuona kama ni jambo rahisi halafu hurudishi kwa sababu ni Mbunge, hapana.

Baada ya kusema maneno hayo; na kwa kuwa meza yangu sasa imekamilisha mambo yote, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho kutwa saa 8.00 mchana.

*(Saa 11.55 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano,
Tarehe 8 Aprili, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*